

CHUO KIKUU CHA NAIROBI

IDARA YA KISWAHILI

MAMLAKA NA ITIKADI KATIKA NYIMBO TEULE ZA TAARAB

TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA

SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI

NOVEMBA 2015

UNGAMO

Tasnifu hii ni matokeo ya juhudi zangu za utafiti na wala sio kazi ya mtu mwingine. Kazi hii haijawahi kuwasilishwa kwa mahitaji ya shahada ya uzamili katika chuo kikuu kingine.

MTAHINIWA

Makhulo Otsieno Evans

Sahihi.....Tarehe.....

Tasnifu hii imeandikwa na kutolewa ili kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Nairobi:

Prof.Rayya Timammy

Sahihi.....Tarehe.....

Dkt.Zaja Omboga

Sahihi.....Tarehe.....

TABARUKU

Kazi hii nawatabarukia babangu Sylvester Makhulo na mamangu Lilian Makhulo.

SHUKRANI

Kwanza, shukrani zangu za dhati ziwaendee wasimamizi wangu wa shahada hii. Kwanza ni Dkt.Zaja Omboga ambaye tathmini zake zilipevusha mawazo yangu hadi nikafahamu mambo niliyozamia kwa kina.Kisha wa pili ni Prof.Rayya Timammy ambaye mbali na tathmini zake zilizonipevusha akili alinipa vitabu mbalimbali vilivyonisaidia katika utafiti wangu.Pili, nawashukuru wazazi wangu Bw. Sylvester Makhulo na Bi. Lilian Makhulo kwa kujinyima mengi wakati nilipohitaji chochote kutoka kwao tangu nilipokuwa mwanafunzi wa chekechea.Pia nawashukuru babu yangu Bw.Anacet Oduor na nyanyangu Bi.Elizabeth Akoth kwa vile licha ya kutojua mengi kuhusu masomo walinipa motisha kila wakati nilipokutana nao.Isitoshe naushukuru sana usimamizi wa Chuo Kikuu cha Nairobi kwa ufadhili wake wa shahada hii.Bila ufadhili huo pengine ingenichukua muda mrefu kabla ya kuifanya shahada hii.Namshukuru pia Bw.Herman Manyora wa Idara ya Isimu na Lugha katika Chuo Kikuuu cha Nairobi aliyenisaidia kwa ushauri kuhusu nadharia niliyotumia katika kazi hii pamoja na kunipa vitabu vilivyonisaidia sana.

Namshukuru mkuu wa Idara ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Nairobi, Prof.John Habwe aliyenikumbusha kila mara kuwa nina uwezo mkubwa wa kiakedemia kila tulipokutana. Uelekezi wake wa awali kuhusu mada yangu ulikuwa muhimu sana.Aidha namshukuru Dkt.Iribemwangi wa Idara ya Kiswahili aliyenipa mwongozo muhimu baada ya kuwasilisha pendekezo langu.Maoni yake yakiwemo yale ya Dkt.Assumpta Matei yalinipa motisha ya kuiandika tasnifu hii nikiwa na mwelekeo ufaao. Pia nawashukuru wanafunzi wenzangu tuliosoma nao katika madarasa ya shahada hii wakiwemo Rosedama David, Francisco Gadhara, Otuchi Timmothy, Rita Magara, Rosemary Kamwanza, Indindi Henry, Biasha Salim, Hezekiel Gikambi na Machira Stephen ambaye safari yetu ya masomo naye ilianzia katika Bewa la

Kikuyu, Chuo Kikuu cha Nairobi mwaka wa 2008. Kutagusana nao kulikuwa na umuhimu mkubwa sana kwangu. Sitamsahau rafiki yangu Bw. Paul Wambo aliyenipa makala mengi kuhusu nadharianiliyotumia katika kazi hii. Shukrani zangu za mwisho ni kwa rafiki yangu wa tangu utotoni Bw. Vincent Wamunyolo kwa msaada wake katika mwaka wangu wa kwanza wakati nikisomea shahada hii.

VIFUPISHO

DCT- Diskosi Changanuzi Tunduizi

IAK- Isimu Amilifu ya Kimfumo

T.Y - Tafsiri Yangu

n.k – na kadhalika

MAELEZO YA ISTILAHU JINSI ZILIVYOTUMIKA

- Diskosi:** Ni njia maalum ya kuwasilisha sehemu fulani ya ulimwengu katika hali ya kijamii kwa namna ya kihalisia au kisaikolojia kupitia kwa kusema au kuandika.
- Mamlaka:** Mamlaka yanahusu mahusiano ya utofauti na hasa athari za tofauti hizo katika miundo ya kijamii. Ni njia ya watu binafsi, makundi au asasi kudhibiti wengine.
- Itikadi:** Ni imani, mitazamo, chukulizi, maadili ambayo huathiri namna watu binafsi au makundi yanavyofikiria pamoja na mitazamo yao. Kupitia kwayo, ukweli hujengwa na kufasiriwa.
- Hejemoni:** Ni njia ya udhibiti inayopatikana wakati akili za wanaodhibitiwa zinaathiriwa kwa njia kwamba wanakubali kudhibitiwa na kuishia kutenda mambo kwa wanaowatawala na kuwadhibiti kwa hiari.
- Udhibiti:** Ni udhihirishaji wa mamlaka ya kijamii unaosababisha hali ya kutokuwepo kwa usawa katika jamii hiyo.
- Uelekezi:** Istilahi katika isimu inayorejelea hali ambapo kitenzi katika kishazi kinahitaji yambwa ili maana yake kuwa kamilifu.
- Yambwa:** Nomino ambayo huja baada ya kitenzi elekezi ambayo yaweza kuwa ya mtendwa au mtendewa katika kishazi. Katika utafiti huu, yambwa tendwa ndiyo tuliyotumia lakini tumeipa jina, Lengo.
- Mtendaji:** Mhusika katika mchakato yakini anayetokeleza kitendo yakini na kitendo hicho kikamwathiri Lengo aliyempokezi wa athari ya moja kwa moja.

Lengo: Mhusika katika mchakato yakini ambaye huathiriwa moja kwa moja na kitendo au vitendo vya Mtendaji.

Mchakato yakini: Mchakato wa uelekezi ambao kitenzi katika kishazi kinaonyesha ufanyaji na utukiaji wa kitendo. Kwa hivyo kunakuwa na anayekifanya kile kitendo (Mtendaji) na anayeathiriwa moja kwa moja na kitendo kile (Lengo).

Mchakato wa kiakili: Mchakato ambao kitenzi katika kishazi chake kinahusu utendekaji wa matendo unaotokea katika ung'amuzi wa mtu binafsi. Kunakuwa na Mhisi anayetenda matendo hayo ya ung'amuzi na kisha matokeo ya vitendo vyake ni Finomena.

Mhisi: Mhusika katika mchakato wa kiakili anayeshiriki katika vitendo vya ung'amuzi au vya kisaikolojia kama vile kuwaza, kufikiria, kujuta kupenda, kuchukia, n.k.

Finomena: Kitu au mtu ambaye anaathiriwa na vitendo vya Mhisi katika mchakato wakiakili.

Mchakato wa: Mchakato ambao huonyesha uhusiano kati ya watu au vitu
kihusiano viwili. Kunakuwa na Mbebaji anayedhihirisha sifa au tabia fulani na kisha kunakuwa na Sifa ambayo ni sifa au tabia ya Mbebaji. Vitenzi vya kuwa, kuwa na, na kuwa mahali ndivyo vinavyohusika katika mchakato huu.

Mchakato wa : Mchakato unaohusu usemaji utambulishwao kwa kuwepo kwa kitenzi
kiusemi *sema* katika kishazi au vitenzi vingine vinavyohusiana na usemaji.

Mifano: sifu, tusi, kemea, hakiki, kejeli, laumu, ongea, zungumza n.k.

Msemaji : Mhusika katika mchakato wa kiusemi anayetoa kauli fulani. Iwapo kuna anayeambiwa maneno yale huitwa Mpokezi .

Kisemi: Ni kile kisemwacho na Msemaji katika mchakato wa kiusemi.

Mchakato wa: Mchakato unaohusu binadamu na huwa wa kisaikolojia na tabia za kitabia kisaikolojia kama vile; kupumua, kukohoa, kutabasamu, kuota na kuangalia.

Mtabia: Mhusika katika mchakato wa kitabia ambaye huwa na tabia kama za Mbebaji katika mchakato wa kihusiano au Mhisi katika mchakato wa kitabia.

Kiini/Mada: Sehemu ya kishazi inayosisitizwa sana kwa vile ndiyo iliyobeba lengo kuu la kile kishazi.

Kisemwacho: Sehemu ya kishazi inayofuata Kiini/Mada inayotoa ujumbe unaosisitizwa.

Mchakato wa : Huu ni mchakato unaoonyesha kuwepo kwa kitu au jambo. Kitenzi katika kidhanaishi mchakato huu ni *kuwa*.

IKISIRI

Utafiti huu ulihusu uchunguzi wa mamlaka na itikadi katika nyimbo za taarab za *Zilipendwa* ulioimbwa na Khadija Yusuf na *Utalijua Jiji* ulioimbwa na Afua Suleimani. Hili liliwezesha na kuwepo kwa malengo matatu. Kwanza, kuchunguza utunzi na maudhui tawala katika nyimbo hizi ili kubaini mafungamano ya masuala hayo na itikadi inayotawala. Pili, kuonyesha udhihirikaji wa mahusiano ya mamlaka katika nyimbo hizo na mwisho, kueleza mikakati ya kipragamatiki na mchango wake katika ujenzi wa mamlaka na itikadi katika hizo nyimbo. Sampuli lengwa ilitumika kuziteua nyimbo hizi mbili na matini zake zikaandikwa baada ya kanda za nyimbo hizo kusikilizwa. Baada ya kuandikwa, vishazi vyake vilichambuliwa kwa kutumia nadharia ya Diskosi Changanuzi Tunduizi (DCT) na mtazamamo wa Isimu Amilifu wa Kimfumo (IAK). Kutokana na uchambuzi huo, iligunduliwa kuwa itikadi ya ubabedume ndiyo inayotawala katika nyimbo hizo na kwamba mahusiano ya mamlaka hujidhihirisha vilevile katika nyimbo hizi. Muhimu zaidi ni kuwa maswala haya ya mamlaka na itikadi yanaweza kuonyeshwa kwa kueleza mikakati ya kipragamatiki katika nyimbo hizo. Utafiti huu utakuwa muhimu kuhusu namna ya kutumia vipengele vya kiisimu kuchanganua matini za lugha ya Kiswahili.

YALIYOMO

UNGAMO.....	ii
TABARUKU	iii
SHUKRANI.....	iv
VIFUPISHO.....	vi
MAELEZO YA ISTILAHU JINSI ZILIVYOTUMIKA	vii
IKISIRI	x
YALIYOMO.....	xi
SURA YA KWANZA:MSINGI WA UTAFITI	1
1.1 Usuli wa Mada ya Utafiti.....	1
1.2 Tatizo la Utafiti.....	5
1.3 Malengo ya Utafiti	6
1.4 Nadharia Tete.....	6
1.5 Uhalalishaji wa Mada	6
1.6 Upeo na Mipaka.....	7
1.7 Mapitio ya Maandishi	8
1.8 Msingi wa Nadharia.....	14
1.8.1 Diskosi Changanuzi Tunduizi	14
1.8.1.1. Historia ya Nadharia ya DCT	14
1.8.1.2 Kanuni za DCT.....	16
1.8.1.3 Diskosi na Mamlaka.....	17
1.8.1.4 Diskosi na Itikadi.....	19
1.8.2 Isimu Amilifu ya Kimfumo (IAK)	20
1.8.2.1 IAK: Ni nini? Madai yake ni nini? Inahusianaje na DCT?	20
1.8.2.2 Uelekezi na Umuhimu wake katika Diskosi	23
1.8.2.2.1 Mchakato Yakini	23
1.8.2.2.2 Mchakato wa Kiakili	24
1.8.2.2.3 Mchakato wa Kihusiano.....	25
1.8.2.2.4 Mchakato wa Kiusemi.....	25
1.8.2.2.5 Mchakato wa Kitabia.....	26

1.8.2.2.6 Mchakato wa Kidhanaishi	26
1.9 Mbinu za Utafiti	26
1.9.1 Ukusanyaji wa Data.....	26
1.9.2 Uchanganuzi wa Data.....	27
1.10 Hitimisho.....	27

SURA YA PILI:UTUNZI WA NYIMBO ZA TAARAB NA MAUDHUI

YANAYOTAWALA KATIKA NYIMBO HIZO 28

2.1 Utunzi wa Nyimbo za Taarab	28
2.2 Maudhuiyanayotawala katika Nyimbo za Taarab.....	32
2.2.1 Mapenzi	33
2.2.2 Umbea/Udaku.....	35
2.2.3 Ukwenza	36
2.2.4 Uasherati.....	37
2.2.5 Masimango/Malumbano kati ya Wanawake	38
2.2.6 Wivu/ Chuki	41
2.3 Hitimisho.....	41

SURA YA TATU:MAMLAKA NA ITIKADI KATIKA WIMBO ZILIPENDWA

ULIOIMBWA NA KHADIJA YUSUF 43

3.1 Muhtasari wa Wimbo <i>Zilipendwa</i>	43
3.2 Mamlaka na itikadi katika wimbo <i>Zilipendwa</i>	44
3.2.1 Mchakato Yakini	45
3.2.2 Mchakato wa Kiakili	49
3.2.3 Mchakato wa Kihusiano.....	53
3.2.4 Lugha ya mafumbo katika wimbo <i>Zilipendwa</i>	55
3.2.5 Hitimisho.....	58

SURA YA NNE:MAMLAKA NA ITIKADI KATIKA WIMBO UTALIJUA

JIJULIOIMBWA NA AFUA SULEIMAN..... 61

4.1 Muhtasari wa wimbo <i>Utalijua Jiji</i>	61
4.2 Mamlaka na itikadi katika wimbo <i>Utalijua Jiji</i>	62
4.2.1 Mchakato yakini	62
4.2.2 Mchakato wa kiakili	71

4.2.3 Mchakato wa kihusiano.....	74
4.2.4 Lugha ya Mafumbo katika wimbo <i>Utalijua Jiji</i>	77
4.2.5 Hitimisho.....	79
SURA YA TANO:MATOKEO, MAHITIMISHO, UMUHIMU WA UTAFITI HUU NA MAPENDEKEZO.	82
5.1 Muhtasari wa mambo ya kimsingi ya utafiti.....	82
5.2 Matokeo	83
5.3 Mahitimisho	86
5.4 Umuhimu wa Utafiti	88
5.6 Mapendekezo	89
MAREJELEO	90
VIAMBATISHO.....	95

SURA YA KWANZA

MSINGI WA UTAFITI

1.1 Usuli wa Mada ya Utafiti

Jamii ya Waswahili imekuwa na historia ndefu ya maingiliano na watu kutoka sehemu mbali mbali za ulimwengu. Baadhi ya wageni waliowahi kutagusana na Waswahili ni kama vile: Wagiriki, Waarabu, Wareno, Wachina, Waingereza, Wahindi, Waitaliano, miongoni mwa wengine. Kama anavyosema Askew, K.M. (2002), maingiliano mengine ya Waswahili na baadhi ya wageni niliotanguliza yalifanyika hata kabla ya majilio ya dini ya Uislamu. Kulikuwepo na biashara ya utumwa kati ya jamii ya Waswahili na wageni kutoka pembe mbali mbali za dunia wakati wa biashara hiyo maarufu kama biashara ya Bara Hindi. Kutokana na maingiliano hayo ya kibiashara na mengineyo kama ya kidini, utamaduni wa Waswahili ulipata athari kubwa ambazo bado zipo mpaka leo. Baadhi ya athari zilikuwa ni katika lugha ambapo lugha ya Kiswahili ilipata matumizi mapana, mitindo ya ujenzi wa nyumba kama za Uarabuni, ndoa kati ya Waswahili na wageni mbalimbali (Massamba, 2002). Pamoja na athari hizo, kulikuwa na athari nyingine muhimu zaidi katika nyimbo zao. Kitabu *Periplus of the Erythrean Sea* kilichoandikwa na Mgiriki asiyejulikana kiliweza kuonyesha maingiliano hayo pamoja na athari zake. Jamii ya Waswahili kama jamii zingine za Waafrika ilitumia nyimbo katika shughuli tofauti tofauti. Kulingana na Yego, E.K. (2011) sherehe za Waswahili ziligawika katika aina mbili kuu; sherehe za mivigha kama vile kuzaliwa, kupewa jina, jando, unyago, harusi na ndoa na kifo ambazo kila mtu alipitia katika jamii na sherehe za shughuli za kila siku kama kazi, mapumziko, michezo na nyinginezo.

Kuna aina nyingi za nyimbo katika jamii ya Waswahili. Hata hivyo zile zinazoshabikiwa sana kwa sababu ya umaarufu wake ni chakacha, lelemama na taarab. Nyimbo za taarab huimbwa mara nyingi katika sherehe za harusi kama nyimbo za harusi. Ujumbe wake huwa umejaa maswala ya mapenzi na hivyo huchukuliwa kwamba ni nyimbo za mapenzi. Ingawa hili ni kweli kwamba mapenzi ndilo swala kuu linalojitokeza katika nyimbo hizo, lugha inayotumika katika nyimbo hizo huwa ya kimafumbo mno. Hudhihirisha mahusiano ya mamlaka ya jinsia na itikadi ya jamii ya Waswahili. Kwa msikilizaji wa kawaida, usikilizaji wa nyimbo hizo bila kuzingatia lugha inavyotumika atadhani kuwa nyimbo za taarab ni za mapenzi tu bila kujua kwamba maneno katika nyimbo hizo yanaendeleza itikadi fulani na kuonyesha mahusiano ya kimamlaka katika jamii hasa kati ya wanawake na wanaume.

Kumekuwa na mijadala iliyozuka kuhusu ni ipi nafasi ya mwanamke katika jamii sio tu wa Waswahili bali pia ya Wafrika kwa ujumla. Kwa muda mrefu, mwanamke kutokana na itikadi ya ubabedume amekuwa akiwekwa pembeni katika masiala ya kijamii, kisiasa na kiuchumi. Wahakiki na watafiti wa fasihi ya Kiafrika pamoja, wasomi katika sayansi ya jamii na hata watunzi wa mashairi, tenzi, tamthilia, riwaya, hadithi fupi na kazi nyingine za fasihi kwa muda mrefu wamekuwa wakimsawiri mwanamke kama kiumbe duni. Kwa mfano, kwa kuzingatia *Utenzi wa Mwanakupona*, mwanamke amekuwa akisawiriwa kama mhusika mwenye nafasi ndogo katika jamii na anayestahili kumtumikia mwanamume kwa kumpikia, kumnyoa ndevu, kumpepea anapohisi joto mwilini, kumheshimu na kunyenyekea maana mwanamume anaweza kumnyima fursa ya kwenda ahera afapo, kumtosheleza kwa ngono miongoni mwa mambo mengine. Hata hivyo, kutokana na mabadiliko katika harakati za kujaribu kukinza baadhi ya mambo yaliyoonekana kama yanayomdhalilisha mwanamke katika jamii, mwanamke alianza

kusawiriwa vizuri kama anayeweza kufanya mambo wanayofanya wanaume mradi apewe nafasi. Wahusika wa kike kama Lanina katika *Kilio cha Haki* (Mazrui, 1984), Natala katika *Natala* (wa Mberia, 1997), Rukia katika *Dar es Salaam Usiku* (Mtobwa, 1998), Kazija katika *Utengano* (Mohamed, 1980) miogoni mwa wengine, wameonyesha kuwa mwanamke anaweza kubadilisha mahusiano ya kijamii kwa kukinza mfumo wa ubabedume. Hii ina maana kwamba nafasi ya mwanamke wa kiasia imekuwa ikichukua sura mbalimbali kutokana na mapito ya wakati.

Kumekuwa pia na tafiti nyingi kuhusu nyimbo za taarab kwa malengo ya kuonyesha nafasi ya mwanamke na itikadi ya ubabedume. Wasomi kama vile Fair, L. (2001) na Askew, K.M. (2002) wametumia mtazamo wa anthroplojia kueleza namna nyimbo za taarab zilivyochangia kuleta maendeleo ya kiuchumi, kisiasa na kijamii kule Zanzibar baada ya uhuru. Malengo makuu ya tafiti zao japo yalikuwa kuonyesha mchango wa nyimbo hizo katika maendeleo ya Zanzibar pamoja na kuonyesha kwamba nyimbo hizo hutumika kama nyenzo ya wanawake kuonyesha juhudi zao za kujikomboa kutoka kwa itikadi ya ubabedume, kazi zao haziwezi kufafanua kwa kina ni kwa nini mwanamke anajaribu kujikomboa. Zaidi ni kwamba upeo na mipaka yake ilihusu sana namna nyimbo hizo zilivyoleta maendeleo ya kiuchumi, kijamii na kisiasa. Nadharia na mawazo ambayo yamekuwa yakiongoza sana kuhusu itikadi ya ubabedume na hivyo kuonyesha nafasi ya mwanamke katika nyimbo za taarab yamekuwa ya ufeministi. Mwanamke amekuwa akionyesha kama anayetawaliwa na mwanamume katika mahusiano yao katika jamii iliyojaa itikadi ya ubabedume. Tafiti hizi kwa kiwango kikubwa zimekuja kuhimitisha kwamba mwanamke amedhibitiwa na mwanamume japo anajaribu kutumia fursa adimu anazopata ili kukinza kudhibitiwa huko katika masiala ya kijamii, kisiasa na kiuchumi. Zaja, J.O. (2008)

akichunguza namna mambo yanayostahili kuwa ya siri katika nyimbo za taarab yameanza kuwekwa wazi kupitia kwa utunzi, kurekodi na kusambaza nyimbo hizo na vile vile akiongozwa na mawazo ya ufeministi ameoonyesha kwamba mwanamke japo amewekwa pembeni, kushiriki kwake katika uimbaji, kurekodi na wakati mwingine utunzi wa nyimbo hizo pamoja na kuanika waziwazi mapambano yake ya siri ya mambo yanayomkera kama vile ukewenza, anatumia nafasi hiyo kukinza itikadi ya ubabedume bila ufahamu wa wanaume wanaowapa nafasi duni katika masiala ya kiuchumi, kisiasa na kijamii. Hata hivyo, mawazo yake yamejikita sana katika utunzi, uimbaji na kurekodi kwa nyimbo hizo ambapo wanawake wakiwa wahusika wanatumia fursa hizo kupinga itikadi ya ubabedume. Kwa upande wake, Yego, E.K. (2011) pia akiongozwa na nadharia ya ufeministi amechunguza namna nyimbo za taarab zinavyotetea nafasi ya mwanamke. Japo kuna ukweli kwamba nyimbo za taarab alizochanganua: *Kibiriti Upeleulioimbwa* na Mwanaidi Shaaban na *Tupendane Wabaya Waulizane* ulioimbwa na Mzee Yusuf zinaweza kuonyesha mapambano ya mwanamke kutetea nafasi yake, mwelekeo aliochukua kwamba mwanamke anapopika, kumpepea joto mumewe, kumtunza kwa kumpa maji ya kunywa na kumwogesha chooni miongoni mwa mambo mengine kuwa kunaonyesha mwanamume anamtegemea mwanamke katika maisha ni mahitimisho yasiyotambua mahusiano ya mamlaka yanayomfanya mwanamke kumfanyia mwanamume mambo hayo, swala ambalo kazi hii itataka kulifafanua na kuliweka wazi. Japo hajatafitia nyimbo za taarab, utafiti wa Matei, A.M. (2014) kuhusu mahusiano ya kijinsia katika riwaya *Unaitwa Nani?* (Wamitila, 2008) kwa kutumia nadharia ya Diskosi Changanuzi Tunduizi na mtazamo wa Isimu Amilifu wa Kimfumo unaohusu kuchunguza maswala ya kiisimu kama vile michakato ya uelekezi, muktadha, dhamira miongoni mwa maswala mengine ndio mtazamo unaoweza kufafanua kwa kina ni kwa nini mwanamke anafanya mambo anayomfanyia mwanamume. Hivyo basi, ingawa mtazamo wa

ufeministi umekuwa ukitawala katika mijadala inayohusu mahusiano kati ya mwanamke na mwanamume kwa kuangazia nafasi anazopewa mwanamke, kuna haja ya kuelewa ni kwa nini hali imekuwa hivyo. Mamlaka na itikadi yakiwa ni mawanda mapya katika fasihi ya Kiswahili ingawa Matei, A.M. (2014) ametumia kueleza mahusiano ya kijinsia katika riwaya ya *Unaitwa Nani?*, utumiaji wake katika utafiti huu unahalalishwa kutokana na kwamba kuna haja ya kutumia mawanda na nadharia inayoibua uelewa na milekeo mipya kuhusu swala zima la ubabedume ikizingatiwa kwamba lugha ni chombo muhimu kinachobeba itikadi za jamii pamoja na kuonyesha mahusiano ya mamlaka katika jamii hiyo (Fairclough, 1989).

1.2 Tatizo la Utafiti

Kumekuwa na tafiti nyingi kuhusu nyimbo za taarab. Tafiti hizo zimekuwa zikijita katika maswala ya maudhui, mabadiliko yanayokumba nyimbo hizo na uchanganuzi wa kintindo. Nyimbo za taarab pamoja na ukweli kwamba ni nyimbo za Waswahili zinazoimbwa kwa lengo la kuburudisha watu wakati wa sherehe za harusi, zimesheheni matumizi ya lugha yanayostahili kuchunguzwa kwa lengo la kubaini mahusiano ya mamlaka na itikadi inayotawala katika jamii ya Waswahili. Kama tulivyoona katika sehemu ya usuli wa mada, mtazamo wa ufeministi umekuwa ukitawala katika kueleza swala la ubabedume na mahusiano ya kijinsia katika nyimbo za taarab na hivyo basi hakujafanywa uchunguzi wa aina hii kuhusu nyimbo za taarab. Kuna haja basi ya kuchunguza swala hilo kwa mtazamo na mawanda mapya na ndipo kwa kutumia nadharia ya DCT na mtazamo wa Isimu Amilifu ya Kimfumo (IAK), utafiti huu unanua kuonyesha kwamba lugha inayoonekana kuwa ya mapenzi na hivyo ya kawaida mno katika baadhi ya nyimbo za taarab imesheheni mahusiano ya mamlaka na itikadi ya ubademume

kuonyesha kuwa katika nyimbo za taarab kuna mahusiano ya mamlaka na itikadi ya ubabedume na yote haya yaweza kuonyeshwa kwa uchanganuzi wa kipragmatiki.

1.3 Malengo ya Utafiti

Kazi hii inaongozwa na malengo yafuatayo;

- (i) Kueleza utunzi wa nyimbo teule za taarab na maudhui yanayotawala katika nyimbo hizo kwa lengo la kubaini mafungamano yake na itikadi inayotala katika nyimbo hizo.
- (ii) Kuonyesha udhihirikaji wa mahusiano ya mamlaka katika nyimbo teule za taarab.
- (iii) Kueleza mikakati ya kipragmatiki katika nyimbo teule za taaraba nna mchango wake katika ujenzi wa mamlaka na itikadi.

1.4 Nadharia Tete

Kazi hii inatumia nadharia tete zifuatazo:

- (i) Utunzi wa nyimbo teule za taarab na maudhui yanayotawala katika nyimbo hizoni mambo yanayosababishwa na itikadi ya ubabedume.
- (ii) Mahusiano ya mamlaka hudhihirika katika nyimbo teule za taarab.
- (iii) Mikakati ya kipragmatiki inahusika pakubwa katika ujenzi wa mamlaka na itikadi katika nyimbo teule za taarab.

1.5 Uhalalishaji wa Mada

Motisha ya kuchagua matini za nyimbo za taarab kwa utafiti huu ni kwamba mojawapo wa njia zinazochangia kutokuwa na usawa katika mahusiano ya mamlaka ni lugha inavyotumika katika matini. Pamoja na kwamba nyimbo za taarab kama kazi yoyote ile ya fasihi huakisi ukweli fulani

katika jamii pia zinaendeleza itikadi ya ubabedume kwa njia isiyokuwa ya wazi na bila ufahamu huo, itachukuliwa kwamba nyimbo hizo ni za mapenzi ilhali itikadi ya ubabedume ndiyo motifu inayotawala katika nyimbo hizo. Mikakati ya kipragmatiki hivyo basi inaweza kufafanua mahusiano hayo ya mamlaka katika jamii kwa kuchunguza matini za nyimbo hizi teule za taarab. Pia, hakuna kazi nyingine katika lugha ya Kiswahili iliyotumia nadharia ya DCT na mtazamo wa IAK kuchanganua nyimbo za taarab maana tafiti nyingi zilizotangulia zimekuwa zikitafiti kuhusu maswala ya maudhui, mtindo na mabadiliko katika utunzi na uimbaji wa nyimbo za taarab hasa kwa kutumia nadharia ya ufeministi (King'ei, 1992, Traore, 2004, Yego, 2011, Mnemuka, 2012). Hivyo basi utafiti huu pia utaleta mabadiliko ya namna matini za fasihi zinavyoweza kuchambuliwa hasa na walimu wa somo la fasihi katika shule za upili na vyuoni nchini Kenya kutoka uchambuzi wa maudhui na mtindo hadi uchambuzi wa kiisimu ambao tumetumia.

1.6 Upeo na Mipaka

Kazi hii inalenga kuonyesha namna mahusiano ya mamlaka na itikadi katika jamii ya Waswahili hujitokeza katika nyimbo za taarab. Inatumia mihimili miwili ya itikadi na mamlaka katika nadharia ya DCT kwa kuchota mawazo ya Fairclough, N (1989, 1995), van Dijk, T (1995, 2001) na Wodak, R (2001). Utafiti huu pia unatumia mtazamo wa IAK wa Halliday, M.A.K (1985, 2004, 2014) kwa uchanganuzi wa kiisimu utakaokuwa muhimu kueleza mahusiano ya mamlaka yanavyojitokeza katika nyimbo za taarab. Umahususi zaidi upo katika uelekezi katika vishazi na michakato yake mitatu mikuu: yakini, kiakili na kihusiano. Michakato mingine ya kidhanaishi, kiusemi na kitabia ina mafungamano makubwa na michakato hii mitatu tunayochunguza na kwa hivyo hakuna haja ya kuichunguza. Isitoshe, utafiti huu pia unachunguza maudhui yanayotawala

katika nyimbo teule za taarab pamoja na utunzi wa nyimbo hizo kwa lengo la kuelezamafungamano kati ya maswala hayo na itikadi ya ubabedume. Isitoshe, mikakati ya kipragmatiki inayoweza ujengaji wa mamlaka na itikadi katika nyimbo hizi itachunguzwa kwa lengo la kuyafafanua mahusiano hayo. Pia kazi hii haitachunguza nyimbo zote za taarab kwa vile nyimbo za taarab zipo katika migao mbalimbali kama vile kimaeneo, kiutunzi, kiwakati, kimtindo, kimaudhui na kifalsafa. Tunatumia nyimbo mbili: *Zilipendwa* ulioimbwa na Khadija Yusuf na *Utalijua Jiji* ulioimbwana Afua Suleimani kutoka Zanzibar wote wakiwa wakati huo waimbaji katika bendi ya *East African Melody*, nyimbo ambazo maudhui yake yanahusu mapenzi na kwa kiwango kikubwa ndoa na ukewenza. Hata hivyo, urejelezi mwingine utafanywa kutoka katika nyimbo zingine za taarab katika tapo lili hili na kazi nyingine za fasihi kushadidia maelezo fulani kutapokuwa na haja ya kufanya hivyo.

1.7 Mapitio ya Maandishi

Udurusu wetu wa yale yaliyoandikwa kuhusu somo hili unakusudia kutekeleza malengo kadhaa ya kimsingi. Kwanza ni kuonyesha fafanuzi anuwai za dhana za kimsingi katika utafiti huu-*taarab, mamlaka na itikadi* kwa nia ya kuonyesha wajibu na majukumu ya nyimbo za taarab katika kuibusha maudhui yanayoendeleza ubabedume. Swala hili la fafanuzi litatusaidia baadaye kutathmini ufaafu wa wahusika katika nyimbo tulizozichagua hasa katika kumulika wanavyoshirikishwa katika misingi ya nafasi wanazozichukua katika nyimbo na jinsi nafasi zao zinavyoweza kutumiwa kama misingi ya kufasiri itikadi na mamlaka katika uendelezaji wa ubabedume. Pili tunataka kuonyesha jinsi waimbaji, wanawake, kama wahusika wanavyoendeleza mamlaka na itikadi kwa kujua au kutojua, jinsi lugha yao inavyoibuka na jinsi mahusiko yao katika uimbaji yanavyojenga mahusiano kidato miongoni mwa wanawake na

wanaume katika misingi ya kuaminika au hata kutoaminika. Kuaminika huku kutafungamanishwa na ukunjufu, uhalisia na kuaminika kwa maongezi ya wahusikamaneno/lugha katika nyimbo. Tutafanya hivi kama njia ya kuweka misingi mwafaka tutakayoitumia hatimaye kupima mawazo makuu yanayojitokeza katika nyimbo tulizochagua, jinsi mawazo hayo yanavyoibusha itikadi na mamlaka, jinsi mawazo hayo yanavyolandana na matukio na mtirirko wa matukio hayo na hatimaye yanavyochangia utimilifu na ubainifu wa itikadi, mamlaka na ubabedume kama ujumbe wa kimsingi. Tatu, udurusu huu unakusudia pia kumulika jinsi maswala ya usawiri wa wanawake, taswira za kitamathali na nafasi ya wanawake katika harakati za kijamii yalivyoshughulikiwa. Nne, tunalenga kuonyesha katika udurusu huu jinsi swala la ubabedume lilivyopewa nafasi za pembeni na ilhali ndilo swala la kimsingi, na kwa hivyo kwa nini linafaa kupewa kipaumbele na pumzi mpya za kuendeleza harakati za wanawake. Taarab ni neno la Kiarabu lenye maana ya “furaha” kulingana na kamusi ya Kiarabu ya *Al Faraid Al Durriya* na linatokana na neno la Kiarabu *tariba* lililo pia na visawe vingine kama *yatiribu* na *taraba* (Khatib, 1992, Askew, 2002). Hii ina maana kwamba nyimbo za taarab za Kiswahili ambazo ziliimbwa mwanzo kule Zanzibar zililetwa huko na Waarabu wakati wa utawala wao katika pwani ya Afrika ya Mashariki wakati wa utawala wa Sultan Seyyid Barghash (Khatib, 1992). Nyimbo za taarab ni mashairi simulizi yanayoimbwa katika Kiswahili hasa na wanawake kama waimbaji na wachezaji na wala sio watunzi. Hata hivyo haina maana kwamba wanawake hawatungi wala wanaume hawaimbi. Hali kwamba wanawake mara nyingi huimba nyimbo hizo zilizotungwa na wanaume ni muhimu sana katika ufafanuzi wa swala la mamlaka na itikadi katika jamiii ambazo nyimbo hizo hutokea. Zaja, J.O. (2008) anasema kwamba wanawake wanapopewa nafasi ndogo za kuimba nyimbo zilizotungwa na wanaume na ambao hutunga kuendeleza ubabedume, kinachotokea ni kwamba wanawake wanaishia kuwekwa

pembeni, kupewa majukumu duni na kwa hivyo bila wao kujua wanaendeleza ubabedume; mfumo wa jamii ambapo jinsia ya kiume inapewa mamlaka katika masiala ya kijamii, kijinsia na kiuchumi huku jinsia ya kike ikipembezwa katika maswala hayo. Hali ingawa ni hiyo, wanawake wanatumia fursa finyu kama hizo kuteta na kukinza maswala hayo maana kama Askew, K.M. (2002;126) anavyosema:

Wakati mwingine ndani ya mapenzi yanayopatikana katika nyimbo za taarab, kuna sehemu ya uhakiki wa jamii, uchukuaji wa misimamo ya kisiasa, mijadala ya kijinsia, malumbano ya utambulisho na usuluhishaji wa migogoro. Mojawapo wa sifa zinazopatikana sana katika nyimbo hizo ni utumiaji mwingi wa jazanda, urejelezi usio wa moja kwa moja na usambamba. Jazanda hufanya wimbo kuwa silaha inayosheheni mamlaka inayotumika sana katika kuzua mijadala ya mahusiano ya kijamii (T.Y).

Kutokana na maelezo haya, ni wazi kwamba mahusiano ya mamlaka na itikadi ni maswala yaliyo katika nyimbo nyingi za taarab lakini hufichwa katika matumizi ya lugha ya mapenzi. Vile vile, kuna harakati za mapambano katika nyimbo hizo. Mamlaka katika utafiti huu yana maana ya uwezo wa mtu au kundi la watu kudhibiti matendo au mawazo ya mtu binafsi au kundi la watu na hupatikana katika matumizi ya lugha (Fairclough, 1989). Kwa upande wake itikadi ni mseto wa maadili na imani zenye udhabiti na mshikamano katika jamii. Fairclough, N (1995). Itikadi nayo ndio huongoza watu namna wanavyotumia lugha na hivyo kudhihirisha mahusiano ya mamlaka. Kwa mfano, katika wimbo *Utalijua Jiji* kuna sehemu ya mshororo: *Kuishi na mume kazi*. Msemaji wa maneno hayo akiwa mwanamke, amefunzwa na jamii yake yenye ubabedume kwamba kuishi na mume ni sawa na kufanya kazi. Sio ajabu mwanamke akimfanyia mwanamume mambo kama kumpikia, kumwogesha, kumpepea ahisipo joto na kumpa mapenzi ya kumridhisha miongoni mwa matendo mengine.

Kutokana na haja ya kueleza nafasi ya mwanamke katika jamii ambayo ni zao la mahusiano ya mamlaka na itikadi, watafiti mbalimbali wamezua mawazo mbalimbali. Zaja, J.O. (2008) amechunguza nyimbo tatu za taarab: *Tutabanana Hapa Hapa* ulioimbwa na Mwanahawa Alley, *Nani Zaidi* ulioimbwa na Zuhura Shaaban na *Mtie Kamba Mumeo* ulioimbwa na Khadija Kopa kwa lengo kuu kubaini namna mambo yanayostahili kuwa siri katika nyimbo hizo hufanywa kuwa ya wazi kutokana na kuimbwa, kurekodiwa na kusambazwa kwa nyimbo hizo. Katika kazi yake, amehitimisha kwamba uimbaji wa nyimbo za taarab ni njia ya kudumisha na kuendeleza mapambano ya wanawake dhidi ya ubabedume na pia wanawake wanapopewa majukumu ya kuwapembeza katika nyimbo hizo, wanatumia fursa hizo kukinza majukumu hayo. Mawazo yake yakiwa yanatokana na mtazamo wa ufeministi yameonyesha kwamba swala la ubabedume linajitokeza katika nyimbo zataarab na wanawake wanajizatiti kukinza nafasi ndogo wanazopewa katika jamii. Japo mahitimisho yake yanatusaidia kuendeleza mjadala kuhusu swala zima la itikadi ya ubabedume na mahusiano ya mamlaka, upeo wake ni tofauti na wetu kwa kuwa sisi tunatumia nyimbo *Utaliyua Jiji* na *Zilipendwa* tofauti na alizotumia. Isitoshe, tunajikita sana katika uchambuzi wa kina wa kiisimu kwa kuangalia michakato ya uelekezi katika vishazi vya nyimbo hizo kwa malengo ya kubaini ni nani aliye na mamlaka katika muktadha upi na kwa nini na hilo linatokea likiongozwa na nini. Mwelekeo huu ni tofauti na wake kwa kuwa amejikita sana katika utunzi, kurekodi na kusambazwa kwa nyimbo hizo. Mwisho ni kwamba sisi hatutumii mtazamo wa ufeministi ambao ametumia bali tunatumia mawanda mapya kabisa ya nadharia ya DCT kufafanua mahusiano ya watu katika jamii na itikadi inayosababisha mahusiano hayo kuwa yalivyo.

Yego, E.K. (2011) amechunguza nafasi ya mwanamke inavyotetewa katika nyimbo za taarab: *Kiberiti Upele* ulioimbwa na Mwanaidi Shaaban na *Tupendane Wabaya Waulizane* ulioimbwa na Mzee Yusuf.Malengo yake yalikuwa kuonyesha mitazamo mizuri kuhusu mwanamke, kuonyesha namna wanawake wanavyojaribu kujinasua kutoka kwa minyororo ya utamaduni na kupinga kasumba kwamba mwanamke ni mnyonge.Japo ni kweli kwamba mwanamke katika nyimbo alizochanganua na nyimbo ambazo tunachanganua hukiinza baadhi ya mahusiano yake na mwanamume na kuonyesha juhudi za kujikomboa kutoka kwa ubabedume,nadharia ya ufeministi ambayo ametumia imesababisha mahitimisho yaliyopotoka.Kwa kudai kwamba mwanamke anapomfanyia mwanamume mambo kama kupika vyakula,kumpelekea maji bafuni, kumpepea anapohisi joto,kumfurahisha kwa maneno matamu na kumtosheleza kingono huwa anadhihirisha kuwa mwanamume anamtegemea sana ili aishi ni madai yasiyokuwa na uelewa wa ni kwa nini mwanamke anamfanyia mwanamume mambo hayo yote.Kwa hivyo,kwa kutumia nadharia ya DCT tunalenga kueleza ni kwa nini mwanamke anamfanyia mwanamume mambo hayo yote.Kama tutakavyohitimisha ni kwamba,mwanamke kwa kufanya mambo hayo hafanyi kuonyesha kuwa anamtegemea mwanamume bali analenga kuingia katika uhusiano wa mamlaka unaodhibitiwa na mwanamume ili aweze kunufaika kutokana na faida za kiuchumiambazo mfumo wa ubabedume umempa mwanamume.

Matei, A.M. (2014) amechunguza mahusiano ya kijinsia katika riwaya ya *Unaitwa Nani?*, ametumia nadharia ya DCT na mtazamo wa IAK kama tunavyotumia katika kazi yetu, akiongozwa na malengo ya kuchunguza namna maana zinavyojenga mahusiano ya mamlaka kati ya wanaume na wanawake, uteuzi wa msamiati na mikakati mingine ya diskosi inayotumika na wasemaji wa kike na wa kiume kudumisha na kukinza mahusiano ya mamlaka na kuuliza iwapo

mamlaka na utambulisho wa kijinsia ni mambo yaliyotambulishwa wazi katika riwaya hiyo. Ameweza kubaini kuwa katika riwaya hiyo, mahusiano ya kijinsia yapo na yamemsawiri mwanamke kama Mbebaji wa Sifa zinazomwonyesha kama mnyonge, mwovu, mtegemezimiongoni mwa mambo mengine yanayotokana na itikadi ya ubabedume. Upeo wake ulikuwa kuchunguza michakato mitatu mikuu ya uelekezi kwa mujibu wa Halliday, M.A.K. (1985,2014) yaani yakini,kiakili na kihusiano na kwa ufupi michakato mingine ya kidhanaishi,kitabia na kiusemi. Pia alichunguza dhamira na uteuzi wa msamiati yote haya yakilenga kuonyesha mahusiano ya mamlaka kijinsia. Mahitimisho yake yalikuwa kwamba lugha katika riwaya ni chombo kinachotumika kuendeleza kutokuwepo kwa usawa wa mahusiano ya kijinsia ambapo mwanamke katika jamii anasawiriwa kama asiyekuwa na mamlaka akilinganishwa na mwanamume. Tofauti ya kazi yetu na yake hata hivyo ni kwamba malengo yetu ni kuonyesha kuwa kuna mamlaka katika nyimbo teule za taarab yaani *Utaliujua Jiji* na *Zilipendwa* na kwamba kuna itikadi ya ubabedume inayotawala katika nyimbo hizo. Hatulengi vilevile kuchunguza swala la mahusiano ya kijinsia alilozamia sana kwa kuchunguza mikakati ya utambulisho wa kijinsia bali tunalenga kufafanua mahusiano ya mamlaka na namna yanavyotokana na itikadi ya ubabedume. Tunafanya hivyo kwa kuchunguza michakato mitatu tu ya uelekezi na sio yote sita, kuchunguza maswala yanayotawala katika nyimbo teule za taarab na kufafanua lugha ya mafumbo ilivyotumika kuendeleza mahusiano ya mamlaka na itikadi ya ubabedume na hivyo kufikia mahitimisho tofauti na yake.

Kwa ufupi, kazi yetu inanua kuonyesha namna swala la ubabedume limekuwa likiwekwa pembeni ambapo limekuwa likitajwa tu katika tafiti zilizotangulia bila uelewa kwamba ndilo swala la msingi linalotawala katika nyimbo nyingi za taarab. Mtazamo wa ufeministi ambao

umekuwa ukitawala umekuwa ukilenga kuonyesha nafasi ya mwanamke bila uelewa kwamba nafasi hiyo ya mwanamke inatokana na itikadi ya ubabedume na mahusiano ya mamlaka katika jamii. Kwa kutumia nadharia ya DCT, tunalenga hivyo basi kuleta pumzi na mawanda mapya katika kuelewa swala zima la ubabedume kwa kuchunguza kwa kina namna mahusiano ya mamlaka kati ya wanawake na wanaume yanavyozungukia swala hilo katika nyimbo teule za taarab na kwa kufanya hivyo pia tutazua mawazo mapya ya kuendeleza harakati za wanawake.

1.8 Msingi wa Nadharia

1.8.1 Diskosi Changanuzi Tunduizi

Kazi hii inalenga kutumia vigezo viwili vya DCT: mamlaka na itikadi kuchanganua nyimbo *Zilipendwa* ulioimbwa na Khadija Yusuf na *Utalijua Jiji* ulioimbwa na Afua Suleimani. Mtazamo wa IAK utatumika pamoja na nadharia ya DCT kufafanua mahusiano ya kijamii kiiisimu.

1.8.1.1. Historia ya Nadharia ya DCT

Kwa mujibu wa van Dijk, T. (2001: 352), “DCT ni mbinu ya uchanganuzi inayolenga kuchunguza mamlaka ya kijamii, udhibiti na kutokuwa na usawa unavyoanza, kuendelezwa na kukinzwa katika matini na usemi katika miktadha ya kijamii na kisiasa” (T.Y). DCT ilianza baada ya kuwekewa msingi na Isimu Tunduizi iliyokuwa ikichunguza matumizi ya lugha katika muktadha (Bloor, M. na Bloor, T. 2004). Tofauti ni kwamba wakati huo, muktadha uliochunguzwa ulikuwa mfinyu mno maana ulihusu masiala ya sintaksia sana. Meyer, M. na Wodak, R. (2001) wanadai Isimu Tunduizi kama ilivyoendelezwa na Chomsky, N. (1957) ilihusu sana masiala ya umatini na hivyo matumizi ya lugha hayakuwepo. Zaidi ni kwamba katika

hali ambapo lugha na matumizi vilipoangaziwa ilikuwa katika pragmatiki kuhusu umilisi wa kipragmatiki na isimu jamii ya msemaji, sentensi na vipashio vya sentensi. Baadaye zilifuata tafiti za kina Labov, W. (1972) na Hymes, D. (1972) kuhusu mabadiliko ya lugha na miundo ya mawasiliano bila hata kuangazia hadhi za jamii na mahusiano ya mamlaka. Baadaye Hodge, R. na Kress, G. (1979) na Fowler et.al (1979) walikuja kuweka msingi wa nadharia hii. Waliendeleza kazi ya Halliday aliyekuwa amekuza IAK kwa kuchunguza maswala ya matini na muktadha. Wawili hawa waliona bora kuita taaluma hiyo DCT kwa sababu ililenga kuchunguza matumizi ya lugha kwa kina ili kubaini itikadi, mahusiano ya mamlaka, chukulizi na maswala mengine ya kijamii. Mawazo ya Althusser, L. (1971) na Foucault, M. (1977) yaliingizwa katika nadharia hii hasa maswala ya lugha na mahusiano yake na itikadi na mahusiano ya mamlaka. Kazi za wataalamu hao ziliimarishwa baadaye na Wodak, R. (1989, 1996), Fairclough, N. (1989, 1996) na van Dijk ((1986, 1991). Kwa mujibu wa Meyer, M. na Wodak, R. (2001), DCT ilipata umaarufu baada ya kongamano lililofanyika Amsterdam mnamo mwaka 1991 ambapo wataalamu hao walihudhuria. Kuanzia hapo majarida ya van Dijk hasa *Discourse and Society* (1990) yalianza kusambazwa kueneza nadharia hii. Vitabu kama *Language and Power* (1989), *Critical Discourse Analysis* (1995) na *Language as Social Practice* (1997) vya Fairclough na vingine vya Wodak na van Dijk viliweka mihimili mizito ikiwemo kutunga kanuni za kimsingi za nadharia hii.

Malengo makuu ya DCT ni kuchunguza mahusiano kati ya lugha, mamlaka na itikadi, mahusiano kati ya diskosi, utambulisho na mabadiliko ya kijamii na wajibu wa diskosi katika utoaji na udumishaji wa utousawa (T .Y kutoka Weiss, na Wodak, 2003). Wodak, R. (2001) anatumia mtazamo wa kihistoria kujaribu kueleza diskosi na jamii, mamlaka na itikadi. Anadai kwamba

mamlaka na itikadi ni mambo yanayotangulia kuwepo kwa matini na hivyo ni vyema kuchunguza historia ya utamaduni wa jamii fulani ili kuona itikadi fulani na mahusiano ya mamlaka yalivyokuwa na yanavyoendelezwa mpaka leo. Van Dijk, T. (1995, 2001) anatumia mtazamo wa utambuzi wa kijamii kueleza namna diskosi na mamlaka yanavyostahili kuchunguzwa. Anadai kwamba udhibiti hutokana na kundi fulani kudhibiti mfumo wa mawazo wa kundi lingine. Hivyo basi, mamlaka yaweza kuwa ya aina mbili: ya kutumia nguvu na ya kudhibiti mfumo wa mawazo na maarifa. Fairclough, N (1989, 2000) anadai kwamba lugha ndiyo nyenzo kuu inayotumika kujenga, kudumisha na kuonyesha mabadiliko katika mahusiano ya mamlaka katika jamii. Lugha kwa mujibu wake hutumika kwa njia inayochora utambulisho fulani pamoja na kudhihirisha na kukinza mamlaka. Kwa mujibu wake lugha huathiriwa na itikadi iliyopo. Uelewa wa historia ya nadharia ni muhimu katika kuleta uelewa kwamba matumizi ya lugha katika nyimbo za taarab kwa mfano hayalengi kufanya jukumu la mawasiliano tu bali ndani yamo kunadhihirishwa mahusiano ya mamlaka na itikadi ya ubabedume. Kwa hivyo, maneno, *Malighafi nimejaza, haitaji tochi hiyo* katika wimbo *Zilipendwa* yananaweza kuchanganua mahusiano yaliyopo kati ya mke na mume na itikadi inayotawala katika jamii hiyo kwamba mwanamke mzuri wa kutamanika na mwanamume ni yule wa makalio makubwa na hilo ndilo linalofanya mahusino kati yao kuwepo. Swala hili nzima huwa ni zao la utamaduni na huweza kuendelezwa kupitia kwa asasi mbalimbali, nyimbo za taarab zikiwemo.

1.8.1.2 Kanuni za DCT

Hodge, R. na Kress, G. (1993), Fairclough, N. (1995), Wodak, R. (1996) na van Dijk, T. (1998) wamekuja kukubaliana kwamba zifuatazo ndizo kanuni za nadharia hii; lugha ni tendo la kijamii ambalo linafasiri ulimwengu, diskosi au lugha kama tendo la kijamii haliwakilishi tu na

kuonyesha matendo ya kawaida ya kijamii bali pia hujumuisha matendo mengine maalum kama vile mamlaka, utawala, udhibiti, chukulizi za maonevu, upinzani n.k.,waandishi na wasomaji wanatofautiana katika uteuzi na upataji wa matini na njia za kuzifasiri matini hizo,elementi za kiisimu na miundo hazifungamani na mifumo yoyote na zina umuhimu hata kama uteuzi ni wa ung'amuzi au wenye ung'amuzi bwete, mahusiano ya mamlaka hutolewa, kuendelezwa na kutolewa tena kupitia diskosi, wazungumzaji na waandishi wote huwa katika matendo ya utoaji maoni mahsusi yenye msingi wake katika malengo mahsusi yenye kuhusishwa na kuhusiana, diskosi huwa ni ya kihistoria kwa sababu matini hupatikana katika muktadha wa jamii, itikadi, wakati na mahali mahsusi na DCT haifasiri matini tu bali huyaeleza pia.

1.8.1.3 Diskosi na Mamlaka

Mamlaka ni kipengele muhimu sana katika DCT kwa sababu diskosi inaangaliwa kama sehemu muhimu sana ambapo utousawa wa mamlaka hudhihirika,kuendelezwa na kusisitizwa kwa njia wazi au fiche (van Dijk, T.1993).Fairclough, N. (1989) anasema kwamba lugha ni chombo kinachotumika kudhihirisha mahusiano ya mamlaka katika jamii.Hivyo kwa kuchunguza matumizi ya lugha ya diskosi fulani tunaweza kuelewa namna mahusiano ya mamlaka yanavyojidhihirisha.Mamlaka yanaweza yakawa ya kutumia nguvu au kudhibiti mfumo wa mawazo wa watu.Tazama ubeti ufuatao wa wimbo *Zilipendwa*.

*Sijanuna sijakereka, vitendo vyake vilinitosha
Zilipendwa kwangu zilipendwa, " long time" nimemfurusha
Nichanganyie nichekicheki, nachichitisha na mtu unatisha
Hujatulia hujabebewa, u limbukeni unachekesha.*

Katika ubeti huu, Msemaji wa kauli “*long time*” *nimemfurusha* ambaye ni mwanamke ana mamlaka akilinganishwa na mwanamume, mpenzi wake wa zamani katika mchakato huo yakini kwa vile aliweza kumfurusha mpenzi huyo.

Mamlaka hutokana na ushawishi, matumizi ya ujanja, mikakati mingine ya kubadilisha akili za watu kwa manufaa ya mtu mwingine. Mamlaka na hata kudhibitiwa kwa kundi fulani la watu kunaweza kutokea bila wanaotawaliwa kujua kupitia kwa matendo ya kawaida katika jamii ambayo huja kuzoeleka na kuchukuliwa kama ukweli kupitia kwenye matini na usemi.

Katika mfano huu kutoka wimbo *Utalijua Jiji* unaonyesha hilo:

Mwenzangu huna ujuzi, rudi tena kajifunze
Bibi acha upuuzi, kuishi na mume kazi

Katika kauli hiyo kwamba *kuishi na mume kazi*, mke wa pilianamfahamisha mke wa kwanza kwamba kuishi na mume si jambo rahisi kwa vile inabidi mke ajibidiishe ndio afaulu kumdhibiti mumewe. Asipofaulu kumfanyia mambo kama vile kumpikia vizuri, kumfurahisha na kumwonyesha mapenzi yaliyonoga, basi mumewe atamtoroka na kwenda kwa mwanamke mwingine. Ufasiri wa kauli ni kwamba mke ana jukumu kubwa la kudumisha mahusiano yake na mumewe ila mume ni sawa na mfalme anayekaa na kutaka ahudumiwe na asipohudumiwa vizuri anaweza kuvunjilia mbali mahusiano yake na mke wake.

Madai ya Foucault, M. (1980) kuhusu mamlaka kwamba yanaweza kutokea upande wowote uwe wa mwenye mamlaka makubwa au machache yatakuwa muhimu katika kazi hii pia hasa katika uchanganuzi wa wimbo *Zilipendwa* ambapo mwanamke anakinza ubabedume kwa kuonyesha kwamba anaweza kufanya mambo yanayodhaniwa kuwa himaya ya wanaume pekee.

1.8.1.4 Diskosi na Itikadi

Itikadi ni mseto wa maadili na imani zenye uthabiti na mshikamano katika jamii. Fairclough, N. (1995) anasema kwamba itikadi ni njia muhimu ya kuanzisha na kudumisha kutokuwepo usawawa mahusiano ya mamlaka. Lugha ni zao la itikadi. Hii ina maana kwamba lugha hufanywa au kukarabatiwa kukuza na kuendeleza matakwa ya wanaotawala kwa kufanya mawazo hayo yaonekane kama halisi na yanayotokana na hali za kawaida katika maisha. Kwa mfano, katika kiitikio cha *Zilipendwa*:

Mwenyewe nawatengeza, shoga sina shida hiyo
Malighafi nimejaza, haitaji tochi hiyo.

Mwanamke katika kauli hiyo anatumia mwili wake mzuri hasa makalio makubwa kwa jazanda ya *malighafi* kuhalalisha kwa nini anapendwa. Hapa, uhusiano wa mwanamume na mwanamke unatokana na namna mwanamke alivyoumbika ili aweze kumpendeza mwanamume. Mwanamke tayari ameshalichukua hilo kama jambo la kawaida kutokana na mfumo wake wa mawazo kudhibitiwa na itikadi ya ubabedume.

Katika nyimbo za taarab kuna matumizi ya sitiari kama vile: *Mwanamke nyonga* katika wimbo wa Khadija Kopa mwanamke anafasiriwa kama kiuno na makalio makubwa: sehemu za mwili wa mwanamke ambazo wanaume wanapenda katika mahusiano ya mapenzi na wanawake. Katika sitiari kama hiyo, mwanamke anasawiriwa kama chombo cha mwanamume cha kumridhisha kingono. Lengo la DCT ni kufichua itikadi fiche kama hizo na mahusiano ya mamlaka katika lugha kwa kufafanua maana za lugha za kimaumbo, sitiari na analogia zinazotumika katika lugha.

1.8.2 Isimu Amilifu ya Kimfumo (IAK)

Sehemu inaeleza IAK ni nini, mawazo yake makuu, dhana ya uelekezi, umuhimu wake na michakato yake ambayo ni muhimu katika uchanganuzi wa diskosi.

1.8.2.1 IAK: Ni nini? Madai yake ni nini? Inahusianaje na DCT?

IAK ni mtazamo wa kiisimu ulioasisiwa na Michael Halliday. Madai makuu ya IAK kama Halliday (2004:23) anavyodai ni kwamba,“Lugha ni malighafi ya kujenga maana na maana hupatikana katika uteuzi wa mitindo fulani maalum. Ili msikilizaji aweze kupata maana hujaribu kufahamu kile ambacho msemaji alinuia kukisema au kuelewa maana ya vipengele vya kiisimu vilivyoteuliwa na msemaji” (T.Y).Kulingana na Bloor,B na Bloor,T (2004:2),“IAK inasisitiza umuhimu wa muktadha wa kijamii katika uzalishaji na uendelezaji wa lugha kihistoria na kimaana katika matukio ya diskosi.Haihusu tu uchanganuzi wa maneno na sentensi kama matawi mengine ya kiisimu bali pia huchunguza matini yaliyo katika kiwango zaidi ya sentensi”(T.Y).IAK hueleza uamilifu wa lugha ambao Halliday (2004) ameuaita *metafunctions* kuonyesha kwamba uamilifu huo ni zaidi ya jukumu la kawaida la lugha la mawasiliano.Tutaeleza uamilifu huo baadaye katika sehemu hii. IAK inasisitiza uamilifu wa lugha maanake muundo wa lugha unajidhihirisha katika kategoria za uamilifu na wala sio katika makundi ya aina za maneno kama nomino na vitenzi (Abdulaziz, M. 1996).Hivyo basi, nomino na vitenzi huelezwa kutokana ma uamilifu wake wa kisemantiki na wala sio kisintaksia.Kitenzi hasa ndicho muhimu katika kueleza jukumu la kishazi.Kishazi kwa kutegemea aina ya kitenzi kilichotumika chaweza kutumika kutekeleza majukumu kama kuonya, kukemea, kusifu, kuonyesha hisia fulani n.k.Hali hii basi inafanya dhana ya matendo ya kiusemi (Austin, J.L. 1962) kuhusiana sana na IAK.

Uchanganuzi wa aina hii unakuwa muhimu katika kufichua vishazi ambavyo kwa mtazamo wa sintaksia pekee vingeweza kuainishwa katika makundi sawa japo katika mtazamo wa semantiki-sintaksia vina tofauti za kimsingi kama mifano ifuatayo itakavyodhirisha. Mfano ni katika ubeti ufuatao kutoka kwa wimbo *Zilipendwa*:

*Nimeshapata mwingine, nampenda peke yake
Si mwembamba si mnene aloshiba kwa mamake
Nalicheza shebene shibe yangu shibe yake*

Mfano1.	<i>Na-</i>	<i>-penda</i>	<i>-m-</i>
Sintaksia	Kiima	kitenzi	Yambwa
Semantiki	Mtumaji	mchakato wa kiakili	Finomena

Mfano 2.	<i>Ni-</i>	<i>- meshapata</i>	<i>mwingine</i>
Sintaksia	kiima	kitenzi	yambwa
Semantiki	mtendaji	mchakato yakini	Lengo

Halliday, M.A.K. (1985, 2014) anaeleza uamilifu wa lugha ambao ndio msingi wa mtazamo wa IAK. Lugha ina uamilifu wa aina tatu; uamilifu wa kiitikadi, uamilifu wa kimahusiano na uamilifu wa matini. Uamilifu wa kiitikadi unahusu kutumia msamiati na sarufi ya lugha fulani kuweza kujenga mtazamo wa anayeitumia lugha hiyo, kueleza mambo, hali zake za ndani na nje n.k. Lugha katika uamilifu huu pia inatumika kutaja vitu na kuviweka katika kategoria. Mfano, ikiwa kuna kusema pia kunakuwa na kuboboja, kugugumiza, kunong'oneza, kujadiliana, kusengenya, n.k. Katika uamilifu huu basi, muhimu ni kwamba mwonoulimwengu wa wasemaji huwa umedhibitiwa na kanuni za msamiati na sarufi wanayoteua yaani, matukio au mambo

yanaelezwa kwa mtazamo wa itikadi inayotawala (Halliday 2014). Ili kubaini jukumu hili linavyodhihirishwa katika lugha, ni muhimu kutazama uelekezi na michakato yake katika vishazi.

Uamilifu wa mahusiano unahusu kueleza lugha kama malighafi ya kuwawezesha watumiaji wake kuanzisha, kujadili na kutekeleza majukumu yao katika jamii. Uamilifu huu humwezesha mtumiaji lugha kusema kauli, kuuliza maswali, kuomba au kurai, kuamrisha au hata kueleza hisia zake za ndani. Hivyo basi, jukumu hili hutekelezwa kwa kuchunguza dhamira (mood) katika kishazi.

Mfano ni kutoka katika wimbo *Paka Mapepe* wa Ashura Majaliwa ambao katika ubeti wake mmoja kuna maneno yafuatayo:

Bali nenda msukume, tena asikusakame
Mkomeshe akukome, abakie alalame

Katika sentensi niliyopigia mstari msemaji ametumia dhamira agizi kwa hivyo anadhihirisha wingi wa mamlaka kwa vile ana uwezo wa kumuamrisha msikilizaji wake.

Uamilifu wa matini ndio muhimu sana. Halliday (2014:30) anasema kwamba, “Kauli zote hulenga kujenga matini. Uamilifu wa mahusiano na itikadi huja pamoja ili kubuni matini. Matini nayo hujengwa kwa mualala na muumano” (T.Y). Halliday (2014) anasema kwamba Kiini/Mada (Theme) na Kisemwacho (Rheme) ni mambo muhimu katika kueleza jukumu la matini. Mfano: *Kama unaweza, mtie kamba mumeo mzuie*. Katika mfano huo *kama unaweza* ni Kiini cha ujumbe ule na sehemu inayosalia ndicho Kisemwacho.

1.8.2.2 Uelekezi na Umuhimu wake katika Diskosi

Miundo ya lugha kwa mujibu wa Halliday (1985), hupangiliwa kisemantiki kwa namna inayoonyesha michakato, wahusika au watendaji na hali nyinginezo ambazo hazipo katika uelekezi yaanivielezi, virai vielezi na virai vihusishi, vyote hivi vikiwa katika mfumo wa uelekezi. Kishazi ndicho kiungo muhimu katika IAK. Hivyo basi, uelekezi ni namna ambayo maana hujifunga kwenye kishazi na namna michakato mbalimbali hudhihirika katika lugha. Kwa maelezo mengine, uelekezi unahusu, ni nani anayefanya nini, anamfanyia nani: ni ipi nafasi au hadhi ya anayefanya au anayefanyiwa: ni nani anayehisi nini au ni nani ana sifa gani. Michakato kwa mujibu wa Halliday (1985:101), "Ni mambo yanayotendeka, yanayofanywa, hisia au hali ya kuwa" (T.Y). Kirai kitenzi ndicho kinachodhihirisha mchakato katika kishazi. Washiriki au watendaji ni viumbe vilivyo au visivyo na uhai, vinavyohusishwa na mchakato mzima katika kishazi na huwa ni virai nomino. Hali kulingana na Halliday (2014:176-177), "Ni mahali, namna, wakati au chombo kinachotumika kutekeleza mchakato fulani na huwa virai vielezi au virai vihusishi" (T.Y). Kwa kuteua msamiati unaotumika na hasa kitenzi kinachotumika katika kishazi, mahusiano ya kimamlaka tofauti tofauti huweza kudhihirika. Uteuzi wa vitenzi katika vishazi huonyesha viwango mbalimbali vya uakala/uajenti unaopewa watu au vitu na dhana kutegemea ni wapi walikowekwa katika mpangilio wa kishazi na uteuzi wa mchakato (Halliday 2004). Ni muhimu basi kuchunguza michakato sita ya uelekezi kulingana na Halliday: yakini kiakili, kihusiano, usemaji, kitabia na udhanaishi.

1.8.2.2.1 Mchakato Yakini

Huu ni mchakato ambao kitenzi katika kishazi kinaonyesha ufanyaji na utukiaji wa kitendo. Kunakuwa na kitendo hicho kutokana na juhudi za mmoja wa Washiriki. Halliday

(2004:179) anasema ,“Mtendaji huwa ni mtu au kitu kinachofanya kitendo na kuathiri mkondo wa matukio na huwa na mamlaka akilinganishwa na Lengo anayekuwa mpokezi kitendo au anayeathiriwa kutokana na utokeaji wa kitendo hicho”(T.Y). Lengo anaweza kuwa Mfaidi au Mwachiriwa wa kitendo.Mfano:*Kama unaweza umtie kamba mumeo mzuie*.Katika mfano huo, mwanamke aliyeolewa kama mke wa pili ambaye ndiye sauti katika wimbo wa *Mtie kamba mumeo* uliyoimbwa na Khadija Kopa huyundiye Mtendaji, *umtie* ni mchakato yakini ilhali mke wa kwanza ni Lengo. Uchunguzi wa mchakato yakini hivyo basi katika utafiti huu ni muhimu kwa sababu katika uelekezi, mtu au kitu kinachofanya kitendo kinasemekana kuwa na mamlaka makubwa kuliko kitu au mtu anayepokea athari ya kitendo hicho.

1.8.2.2.2 Mchakato wa Kiakili

Huu ni ni mchakato wa kuhisi.Kwa mujibu wa Halliday (2014:197), “Kishazi cha “kiakili’ kinahusu utendekaji wa matendo unaotokea katika ung’amuzi wa mtu binafsi” (T.Y).Hivyo basi, huwa kuna Mhisi ambaye anahisi na Finomena ambacho ndicho kitu au mtu anayeelekezewa hisia hizo.Finomena ni kitu kinachohisiwa, kufikiriwa au hata kutakiwa. Mfano:*Nimeshapata mwingine, nampenda peke yake*.Katika kishazi kilichopigiwa mstari, Mhisi ni mwanamke aliyemfusha mpenzi wake wa kiume anayeakilishwa na mofu {na-} ilhali *-penda* ni mchakato wa kiakili na Finomena ni mwanamume mwingine mpya aliyemchukua anayeakilishwa na mofu {-m-}.Katika mchakato wa kiakili,Mhisi hana mamlaka ya moja kwa moja kwa Finomena kama yale ya Mtendaji kwa Lengo katika mchakato yakini .Kwa vile mchakato huu unahusu utambuzi wa wasemaji katika lugha kuhusu ulimwengu wao wa ndani na nje, unatumika kujenga utambulisho, imani, misimamo na itikadi; maswala ambayo utafiti huu unachunguza.

1.8.2.2.3 Mchakato wa Kihusiano

Ni mchakato wa kuonyesha hali ya kuwa na hali ya kuwa na kuwa mahali (Halliday: 2014). Mchakato huu huonyesha uhusiano kati ya watu au vitu viwili. Vitenzi vinavyoonyesha mchakato huu ni vitenzi vya kuwa, kuwa na na vya kuwa mahali k.v ni, kuwa n.k katika njeo iliyopo na iliyopita. Katika mchakato huu kuna mshiriki wa kwanza ambaye ni Mbebaji na ndiye mwenye sifa, uhusiano au kuwa mahali fulani. Pili kuna mshiriki wa pili aitwaye Sifa ambaye huwa ni sifa inayohusishwa na Mbebaji, mahali aliko au uhusiano unaotaka uonyeshwe.

Mfano: *Usitazame gauni japo ndiyo mavazi yake*

Tofauti wewe huoni, hana haiba ya kike

Katika kishazi nilichopigia mstari kutoka katika wimbo *Paka Mapepe* mwanamke anayesutwa na mwenzake ni Mbebaji, *hana* ni mchakato wa kihusiano na *haiba ya kike* ni Sifa. Halliday (2014:210) anasema kwamba mchakato huu ni muhimu kueleza sifa za watu pamoja na kuwatambulisha. Tutachunguza matumizi ya sitiari katika nyimbo za taarab ili kueleza mchakato huu ulivyo muhimu.

1.8.2.2.4 Mchakato wa Kiusemi

Ni mchakato wa usemaji utambulishwao kwa kuwepo kwa kitenzi *sema* katika kishazi au vitenzi vingine vinavyohusiana na usemaji. Mifano: sifu, tusi, kemea, hakiki, kejeli, laumu, ongea, zungumza n.k. Kunakuwa na Msemaji ambaye ndiye anayesema jambo, Mpokezi ambaye ndiye huambiwa jambo kisha Kisemi ndicho kisemwacho. Mfano: *sikuambiwa yupo, nimeambiwa wako*. Katika kishazi hicho kutoka wimbo *Zilipendwa*, Msemaji ni mwanamke anayemweleza mwenzake aliyechukuliwa na mpenzi wake wa zamani, *sikuambiwa* ndio mchakato wa kiusemi na *yupo* ndicho Kisemi. Kazi hii haitatumia mchakato huu katika uchanganuzi wake wa matini kwa

sababu kama ilivyotangulizwa katika sehemu ya 1.6 , mchakato huu na miwili inayofuata ina mwingiliano na michakato mitatu iliyoelezwa hapo juu.

1.8.2.2.5 Mchakato wa Kitabia

Huu ni mchakato unaohusu binadamu na huwa wa kisaikolojia na tabia za kisaikolojia kama vile; kupumua,kukohoa,kutabasamu,kuota na kuangalia.Kwa sababu hiyo basi una sifa yakini na sifa za kiakili.Mshiriki katika mchakato huu huwa na sifa kama za Mhisi katika mchakato wa kiakili au Mbebaji katika mchakato wa kihusiano na hivyo basi hatutauchunguza.

Mfano: *Unaniona natamba na mpenzi wangu sambamba*. Katika kishazi hiki kutoka wimbo *Zilipendwa, U (wewe)* ni Mhisi au Mtabia ilhali *-ona* ni mchakato wa kitabia.

1.8.2.2.6 Mchakato wa Kidhanaishi

Huu ni mchakato unaoonyesha kuwepo kwa kitu au jambo.Kitenzi katika mchakato huu ni *kuwa*. Halliday, M.A.K. (2014:256) akimnukuu Hassan, R. (1984:3) anasema kwamba mchakato huu haujitokezi sana katika diskosi ila hutumika sana katika usimulizi wa hadithi kuonyesha mahali pa tukio.Kunakuwa na Kidhanaishi (Existent) kama Mshiriki.Mfano, *Kulikuwa na upepo mkali leo*. Katika mfano huo, *kulikuwa* ni mchakato wa kidhanaishi ilhali *upepo mkali* ni Kidhanaishi.

1.9 Mbinu za Utafiti

1.9.1 Ukusanyaji wa Data

Utafiti huu ni wa maktabani.Sampuli lengwa itatumika ambapo nyimbo mbili za taarab *Zilipendwa* uliyoimbwa na Khadija Yusuf na *Utalijua Jiji* uliyoimbwa na Afua Suleimani zitateuliwa na kusikilizwa ili matini zake kuchanganuliwa kwa sababu zina utajiri wa maswala

tunayochunguza. Matini za nyimbo zingine za taarab zilizosikilizwa na kuandikwa zitatumika pia hasa pale ambapo kutakuwa na haja ya kutoa msisitizo. Mtafiti kisha ataziandika na kuzipiga chapa ili matini zake zitumike katika uchambuzi. Vitabu,majarida,makala yaliyochapishwa na tasnifu mbalimbali kuhusu nadharia ya DCT na mihimili yake ya mamlaka na itikadi , mtazamo wa IAK na dhana ya uelekezi na michakato yake, ,nyimbo za taarab na hasa kuhusu utunzi na maudhui, zitasomwa maktabani na mtandaoni.

1.9.2 Uchanganuzi wa Data

Vishazi katika matini za nyimbo teule vitabainishwa kwa kupigiwa mistari ili kuweza kufafanuliwa kwa kuchunguza michakato ya uelekezi ili kuelewa mahusiano ya mamlaka ambayo ni muhimu katika kueleza itikadi inayoyazalisha na kuyadumisha. Baada ya mahusiano hayo kubainika, ufafanuzi utafanywa kwa kutumia mawazo ya nadharia DCT kuhusu itikadi na mamlaka huku mifano michache ikitolewa kutoka kazi zingine za fasihi.Kila wimbo utachanganuliwa kivyake kwa misingi iliyo hapo juu katika sura ya tatu na na nne.

1.10Hitimisho

Katika sura hii tumejadili maswala ya msingi kuhusu utafiti wetu. Tumeleza usuli wa mada, nadharia tete, malengo, nadharia tunayotumia ya DCT na IAK, na vipengele vyake tunavyotumia, uhalalishaji wa mada, upeo na mipaka, maswala ya itikadi na mamlaka pamoja na mbinu za utafiti tutakazotumia katika utafiti huu. Yote haya tumeyafanya kwa lengo la kuweka msingi wa sura zinazofuata ambazo zitajikita kwenye msingi huu.

SURA YA PILI

UTUNZI WA NYIMBO ZA TAARAB NA MAUDHUI YANAYOTAWALA KATIKA

NYIMBO HIZO

2.1 Utunzi wa Nyimbo za Taarab

Uelewa wa utunzi wa nyimbo za taarab hauwezi kukamilika bila ufahamu wa historia yake kwa ufupi. Hivyo basi historia ya nyimbo za taarab inastahili kuelezwa kwa lengo la kufahamu ni kwa nini utunzi wake mpaka leo unahusishwa sana na wanaume licha ya wanawake kutunga nyimbo chache pia na kwa nini swala la ubabedume linajitokeza sana katika nyimbo hizo.

Askew, K.M. (2002:2-3) anasema, "Neno taarab linatokana na neno la Kiarabu *tarabun* lenye maana ya furaha, uridhikaji, kufurahishwa, burudani, muziki, uhusiano uliokamilika katika muziki" (T.Y). Hii ina maana kwamba lengo kuu la nyimbo za taarab kama asili yake ilivyo ni kuburudisha. Nyimbo za taarab ni mashairi simulizi yanayoimbwa kwa Kiswahili hasa na wanawake kama waimbaji na wachezaji ingawa wakati mwingine wanawake hutunga pia. Kwa mfano, nyimbo za Bi. Malika zilikuwa zikitungwa na mwanamke kwa jina Khulayta Said Muhashamy. Nyimbo za taarab kwa mujibu wa Timammy, R. (2002: 196) na Igobwa, S.E. (2007) huimbwa hasa wakati wa sherehe za harusi katika jamii za Waswahili. Utunzi na uimbaji wa nyimbo za taarab una historia ndefu maanake zilitumika kama nyenzo ya kuwasilisha masiala ya kijamii miongoni mwa wakaazi wa pwani ya Afrika Mashariki (Zaja, J.O. 2008). Hata hivyo, hii haina maana kwamba nyimbo za taarab zinaimbwa tu Afrika Mashariki. Kulingana na Khamis, S.A.M. (2005:133), nyimbo za taarab kando na kuwa maarufu Afrika Mashariki pia zinaimbwa maeneo mengi nje ya eneo kama vile Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Morocco, Angola, Libya, Yemen, Msumbuji, Bahrein, Uturuki, Misri, India, Saudia, Burundi,

Rwanda, Visiwa vya Ngazija na Dubai. Kabla ya nyimbo hizo kufika Zanzibar zilikoanzia katika eneo la Afrika Mashariki na baadaye kusambaa na kufika maeneo mengine kama Mombasa, Malindi, Lamu na Tanganyika (iliyoungana na Zanzibar mwaka wa 1964 kuunda jamhuri ya Tanzania). Kwa mujibu wa Ntarangwi, M. (2003:171), maingiliano ya kibiashara wakati wa biashara maarufu ya *Bahari Hindi* ndiyo yaliyosababisha aina hii ya nyimbo kuwepo katika pwani ya Afrika Mashariki. Kabla ya hapo, aina ya nyimbo ziiwazo *kinanda* zilikuwa maarufu hasa kwa kutumia ala iliyoitwa kibangala pamoja na ngoma mbili kule Mombasa na Malindi, Kenya. Matumizi ya *kibangala* na umaarufu wa nyimbo za kinanda ulififia baada ya majilio ya ala mpya ya muziki iliyoitwa udi na mtindo wa nyimbo za taarab wa Kiarabu. Kulikuwa na athari zingine za maingiliano hayo kama vile ndoa kati ya Wabantu waliokuwa wenyeji na wageni kutoka nchi zingine kama Omani, Uchina na Misri, kusambaa kwa dini ya Uislamu, kuwepo mijengo ya nyumbakule pwani ya Afrika Mashariki yenye miundo iliyofanana na ya Uarabuni pamoja na vita kati ya jamii kutokana na biashara ya utumwa (Masamba, D.P.M. 2002). Nyimbo za taarab kule Zanzibar zilichipuka katika robo ya mwishoni mwa karne ya kumi na tisa (1870 na kuendelea) wakati wa utawala wa Sultan Seyyid Barghash kama Sultan wa Zanzibar (Zaja, J.O. 2008, Yego, E.K. 2011).

Nyimbo za taarab zilianza kama muziki uliokuwa ukiimbiwa watu wa daraja la juu katika utawala wa Kisultani hasa Sultani, mabepari na viongozi wengine wa tabaka lile. Wakati huo, ziliimbwa kwa lugha ya Kiarabu huku ala za muziki zilizotumika zikiagizwa kutoka Misri na Uarabuni. Nyimbo hizo ziliimbwa tu katika kasri la Sultan na zilionyesha upeo wa raha na anasa za dunia hii zilizokuwa tu zikifurahiwa na tabaka la juu katika jamii. Mwanamuziki Muhammad Ibrahim mkaazi wa Zanzibar alitumwa na Sultan Barghash kwenda Misri kujifunza ala za muziki

za Kiarabu ili baadaye aje kutumia ujuzi ule katika uimbaji (Askew, K.M. 2002:2, Khatib, M.S 1992:1). Siti binti Saad aliyefahamika kwa lakabu ya Mtumwa na aliyeishi kati ya mwaka 1880 hadi 1950 ndiye aliyekuwa wa kwanza kuimba taarab kwa lugha ya Kiswahili. Kulingana na Igobwa, S.E. (2007), Siti aliweza kuimba kwa lugha za Kiswahili, Kihindi, Kigujarati na Kiarabu. Siti alianza kuimba nyimbo za taarab mwaka 1928 baada ya kujiunga na bendi ya *Nadi Ikhwani Safaa* iliyoongozwa na Lord Muhsin. Bendi hiyo ilikuwa ikimwambia Sultan Barghash. Wanawake wasiokuwa watumwa wakati huo hawakuruhusiwa kuimba nyimbo za taarab kwa sababu lilionekana kama jambo la aibu ila Siti aliimba kwa vile alikuwa mtumwa. Isitoshe, aliruhusiwa kuimba maanake kwa mujibu wa Igobwa, S.E. (2007), sauti na uimbaji wake ulilinganishwa na aliyekuwa bingwa wa nyimbo za taarab kule Misri, Umm Kulthum. Alikuwa mwanamke wa kwanza kuimba nyimbo za taarab kutoka Afrika Mashariki na zaidi ya yote kuimba nje ya mipaka ya Zanzibar maanake alikwenda India, Columbia na mataifa mengine. Baadhi ya nyimbo zake maarufu ni kama: *Uchungu wa Mwana*, *Waimbaji wa Juzi*, *Siweke Tamaa Mbele* na *Ela Kafa Ndugu Zangu*. Nyimbo zake zilichangia pakubwa katika ubadilishaji wa taarab kama nyimbo za tabaka la juu pekee na sasa kuwa nyimbo zilizotumbuiza umma mpana kule Zanzibar, Tanganyika na Kenya.

Siti alizitumia nyimbo zake kama chombo cha kupinga maswala ya kijamii kama vile utabaka uliokuwa ukiendelezwa na utawala wa Kiarabu pamoja na uwekwaji pembeni wa wanawake. Siti ndiye aliyekuwa mwanamke wa kwanza Zanzibar kuziimba na hivyo kuvunja kaida kuwa zilikuwa nyimbo za kutungwa na kuimbwa na wanaume tu. Kwa kuwatenga wanawake, itikadi ya ubabedume ilikuwa ikijitokeza bayana.

Mpaka leo, nyimbo za taarab hutungwa mara nyingi na wanaume na wanawake huwa waimbaji.Hata hivyo, haina maana kwamba wanaume hawaimbi nyimbo hizo wala kwamba wanawake hawazitungi. Wimbo mmoja unaweza kuwa na mtunzi, mpangaji wa vyombo vya muziki na mwimbaji.Ushirikiano huo katika nyimbo za taarab unadhihirisha mahusiano kama tutakavyoeleza baadaye.Watunzi wengi wa mashairi hayo huwa ni wanaume lakini wanawake ndio wanaoimba na kucheza jukwaani wanapowasilisha.Kwa mfano,katika bendi ya *Jahazi Modern Taarab*,Mzee Yusufu (ambaye ni mwanamume) ndiye hutunga mashairi ya nyimbo huku wanawake kama vile Khadija Yusuf, Leyla Rashid na Isha Ramadhani huimba.Katika *Zanzibar Star* mtunzi wa wimbo kama *Tutabanana Hapa Hapa* ni Haji Machano (ambaye ni mwanamume) kisha Mwanahawa Alley ndiye mwimbaji. Wanaume pia kando na kutunga huweza kuimba.Mzee Yusuf akiwa katika *East African Melody* na sasa *Jahazi Modern Taarab* huweza kutunga na kuimba nyimbo zake mwenyewe kama vile *VIP*. Nyimbo hizo zinapokuwa zikiimbwa, chukulizi zaweza kuwa wanawake ndio watunzi kutokana na malumbano yanayotokea katika nyimbo hizo.Malumbano hayo huhusu mijadala mikali kuhusu matabaka, jinsia na mahusiano ya kijamii na hutokana na tajriba za mtu binafsi na za kijamii.Huimbwa kama kauli kuhusu maadili ya kijamii na mahusiano.

Kauli kwamba nyimbo hizi hutungwa mara nyingi na wanaume na kuimbwa na wanawake inaonyesha majukumu mbalimbali wanayopewa watu katika jamii hii na hivyo kuzua mahusiano yamamlaka kulingana na jinsia zao.Wanaume wanapokuwa watunzi na kuwafanya wanawake waimbaji tu, katika nyimbo hizo wanazotunga, hutaka kuendeleza na kudumisha ubabedume na hivyo kuhakikisha kwamba mahusiano kati yao na wanawake yanasalia yale ya mwanamke kuwa mtegemezi wa mwanamume.Haji Machano,mtunzi wa nyimbo kama vile *Tutabanana*

HapaHapa na *Nani Zaidi* akihojiwa na Traore, A.L. (2004:77) kuhusu ni kwa nini aliitunga wimbo *Tutabanana Hapa Hapa*anasema:

Nimetunga kwa sababu kuna watu mpaka leo wanakataa kuolewa wawili,ushafahamu?Mimi ni Mwislamu.Kama mwanamume ana uwezo anaweza kuoia wanawake wawili watatu mpaka wanne.Madhali sisi tunafuata dini na wanawake kwa kiwango kikubwa wapo wengi.Tunavyoamini wanahitaji kuolewa.Sawa?Kwa hivyo ni vyema kuoia kwa *system* ile iliyoruhusiwa katika dini.Wawili,watatu mpaka wanne.Sasa kuna wanawake huwa wanakataa lakini hawana *legal* sawa sawa? Kwa hivyo ndo hawana sababu ya kukataa.Kwa hivyo nilijaribu kuwaambia wanawake wale wanaokataa kwamba wasikatae kukaa na wenzao.Wakiolewa na mwenzio kama wawili watatu wakubali tu kukaa naye muishi msikilizane *provides* Bwana anagawa kila kitu sawa sawa.

Nukuu hii inaonyesha kwamba wanaume wanatunga nyimbo kama hizi kwa lengo la kuendeleza ubabedume. Kwa hivyo wanawake wanaojaribu kupinga wanatungiwa nyimbo ili kukumbushwa kwamba ni bora kukubali swala hilo ambalo wanaume wanatumia dini ya Uislamu kulihalalisha.Vilevile wanawake wanajaribu kupinga swala zima na hivyo kunakuwa na mapambano ya kubadilisha mahusiano ya mamlaka ambayo yanaathiri maswala ya kijamii, kiuchumi nakisiasa.

2.2 Maudhuiyanayotawala katika Nyimbo za Taarab

Masuala yanayojitokeza katika nyimbo hizi wakati huwa ni matokeo ya tajriba za maisha, itikadi za jamii, mahusiano ya kijamii na mitindo ya maisha ya kila siku, mambo mabaya katika jamii kama uasherati, uvivu, tamaa, uongo, umbea na ujanja hushambuliwa katika jamii hii.Nyimbo hizi vilevile kutokana na maudhui yake huweza kuonyesha aina za mahusiano au hata matukio muhimu katika jamii hasa ya kihistoria yanayopaswa kukumbukwa.Kwa mujibu wa Zaja, J.O. (2008), nyimbo za taarab huwa na mikakati fiche inayotumika kuuliza, kuchanganua na kubadilisha mahusiano ya kijamii na kiuchumi.Mikakati hiyo inayaweka wazi mapambano ya

kisiri na kwa hivyo kushawishi na kuleta maswala ya mawanda ya umma ambayo yamefichwa lakini yenye umuhimu katika kuonyesha upembezaaji wa washiriki wa kijamii na makundi yanayokinzana.

Yafuatayo ni maudhui yanayotawala katika nyimbo za taarab hasa katika tapo hili la nyimbo za taarab zinazohusu mahusiano ya mwanaumena mwanamke katika jamii. Nyimbo teule katika utafiti na nyingine katika tapo lili hili zinachambuliwa kwa lengo la kubaini maswala yanayotawala humo.

2.2.1 Mapenzi

Haya ndiyo maudhui makuu yanayopatikana katika nyimbo za taarab za sampuli hii. Mtu anapokuwa anataka wa kumpenda hilo huwa kama maradhi ambayo yanastahili kutibiwa. Hutumika sitiari za tabibu au daktari wa mapenzi kama katika wimbo *Daktari wa Mapenzi* wa Mzee Yusuf kuonyesha kwamba mtu anapompata ampendaye basi shida yake ambayo ni sawa na ugonjwa huwa imepata tiba. Mwimbaji humsifu mpenzi wake, kujivunia na kutangazia wenzake anavyohisi kuhusu mpenzi wake. Vile vile anaweza kuonyesha kukerwa kwake na mpenzi hasa mapenzi yao yanapofika mwisho. Katika wimbo *Zilipendwa* mwimbaji anasema kwamba amepata mpenzi mwingine anayempenda.

*Nimeshapata mwingine, nampenda peke yake
Si mwembamba si mnene, aloshiba kwa mamake
Nalicheza shebene shibe, yangu shibe yake*

Katika ubeti huo, mwanamke anamsifu mpenzi wake mpya japo wimbo mzima umetungwa kumsuta mpenzi wake wa zamani aliyefanya penzi lao kutibuka. Mwanamke katika nyimbo hizi husawiriwa kama mtu anayestahili kuwa mjuzi wa mambo muhimu kuhusu mapenzi.

Anadhirisha hilo kwa kumfanyia mwanamume mambo kama kumpikia vyakula vitamu, kumpa ngono ya kuridhisha, kumpelekea maji ya kuoga bafuni na kumridhisha kwa kila njia. Ubeti wa mwisho katika wimbo *Utalijua Jiji* unadhihirisha hilo:

*Nami sifanyi ajizi, mpenzi ninamuenzi
Nampikia maandazi, na chai ya tangawizi
Wali wa nazi kwa ndizi, mavitus kama kazi
Kisha nampa dozi, impayo usingizi
Mwenzangu huna ujuzi, rudi tena kajifunze...*

Katika maneno haya yanayoonekana kuwa ya mapenzi, kunajitokeza swala la majukumu ya mke kwa mumewe. Mke anakuwa mtu ambaye ni sawa na mtumwa wa mumewe kwa namna anavyostahili kumwonyesha mapenzi kama ubeti huo unavyoonyesha. Ubabedume umemfanya mke kuamini kwamba mke asiyejua kumfanyia mume mambo hayo si kitu katika jamii na hivyo anastahili kurudi kujifunza iwapo anataka kujihusisha na mwanamume katika ndoa. Mwanamke hivyo basi anatumia kila njia kupata mahusiano na mwanamume hata kama ni kumtoa kwa mke mwenzake kwa lengo la kupata fursa ya kuhusiana naye maana kama inavyojidhirisha katika wimbo *Nani Zaidi*, kumpata mwanamume ni kama kupata mtindo wa sasa au “fesheni” kama neno hilo lilivyotumika katika ubeti wa tano:

*Hakuna cha peke yako, hususa hapa mjini
Kugawana na wenzako, siku hizi ni “fesheni”
Tutabana hapa hapa,
Hunipiku asilani, nipisheni niwe chini,
Nile kama moto wa kifuu.
Usijisumbue, cheo chetu ni kimoja.*

Mapenzi haya hata hivyo yanavyodhirishwa na wanawake kama asemavyo Zaja, J.O. (2008) sio mapenzi yanayotokana na swala la kisaikolojia (hisia za dhati za mapenzi) kama anavyostahili kuwa bali ni bidhaa anayotumia mwanamke kwa lengo la kupata faida za kiuchumi kutoka kwa mwanamume kama vile chakula, nyumba, makao na pesa. Basi mwanamke bila kujua kwamba

anaendeleza ubabedume hujivunia sana mambo yanayomleta karibu na mwanamume na kuwacheka wenzake wasio na sifa za tabia au mwili alizonazo.

2.2.2 Umbea/Udaku

Umbea ni maudhui mengine makubwa katika nyimbo za taarab. Ni nadra kupata wimbo wa taarab usiotaja swala hili. Katika wimbo *Umejuaje Kama Si Umbea* wa Mwanaidi Shaban, anasema;

*Umejuaje, umejuaje, umejuaje?
Umejuaje nimefanikiwa, umejuaje
Umejuaje kama si umbea umejuaje.*

Umbea ni tabia ya wanawake Waswahili. Timammy, R. (2002) akimnukuu Strobel (1975:9) anasema kwamba wanawake hushiriki katika masengenyo wanapokuwa katika kumbi za sherehe za harusi, ambako waimbaji wa nyimbo za taarab hualikwa kutuimbuiza hadhira katika sherehe ya kupamba; bibi harusi huletwa mbele ya umma jioni baada ya kufanya mapenzi kwa mara ya kwanza na mumewe baada ya kufunga nikaha.

Kwa kuwahusisha wanawake na tabia ya umbea, wanaume ambao wanatunga nyimbo kama hizi wanamsawiri mwanamke kama mtu ambaye kazi yake ni umbea kuhusu watu wengine na hasa wanawake wenzake kuhusu nguo wanazovaa, wapenzi wao walivyo, nani amempokonya nani mume, mwanamke asiyejua kumtunza mume na mengineyo. Hili linatokana na itikadi ya ubabedume ambapo mwanamume anatumia kila njia kumpepembeza mwanamke kwa kumshirikisha na mambo mabaya yasiyo na maana kama hili la umbea.

2.2.3 Ukewenza

Ukewenza ni swala lingine linalopatikana katika nyimbo hizo. Ingawa katika utamaduni wa Uswahilini ukewenza unakubaliwa kutokana na athari ya dini ya Uislamu inayoruhusu jambo hilo, hutokea malumbano kati ya wake wenza. Wengine hujisifu kujionyesha kwamba ni bora kuliko wenzao kwa waume zao. Husifia ubora wao kwa maswala ya mavazi, usafi, upishi na ujuzi wao katika maswala ya mapenzi kitandani. Mfano, katika wimbo *Tutabanana Hapa Hapa*, mwanamke wa pili aliyeolewa na mume wa mwanamke wa kwanza anamwonya kuwa atapambana naye maanake yeye ni mke mwenzake wake. Kuonyesha kwamba yeye ni bora zaidi anasema:

*Unajieti na nyongo kunitilia, huniwezi kwa lolote
Mambo yangu poa, kwa mapenzi hunipati
Raha nazijulia, penzi nampa lote
Yeye anafurahia, wewe hujui chochote
Mimi ninavyosikia, na kupika si yako hadhi*

Katika wimbo *Utalijua Jiji*, mkewe pili anamwambia mke wa kwanza kuwa ashampokonya mumewe na kwake hawezi kurudi tena. Hii ina maana kwamba amekwenda kwa mume huyo akijua ni mume wa mwenzake lakini hilo halijali bora apate sehemu yake. Na kwa kweli anaweza kuipata sehemu kubwa kulingana na wimbo kwa sababu anasifia namna ya kumtunza mume vizuri kuliko alivyokuwa akitunzwa na mkemwenza. Katika ubeti wa mwisho anasema:

*Wako nishamchukua, kwako harudi tena
Katamka waziwazi, kuwa hakutaki tena
Amenipa nafasi, nimwonyeshe ujuzi...*

Malumbano haya yanazua mambo mawili makuu. Kwanza, yanaonyeshakuwa wanawake wamekubali ukewenza maana jamii yao imewafanya kuamini kuwa sio jambo baya. Ndio sababu katika *Utalijua Jiji*, mwanamke ambaye ni sauti ya mwimbaji amemchukua mume wa mwenzake

na kumwambia kuwa amemchukua kutokana na kwamba mwenzake amekuwa akimdhulumu mume huyo. Hivyo swala la ukewenza wanawake wanalikubali. Katika *Nani Zaidi* pia hilo linadhihirika katika ubeti wa nne:

*Lala naye siku mbili, na kwangu alale mbili
Ukizidisha siku moja, cha moto utakiona.*

Pili ni kwamba wanaume wanasisitiza hilo swala la ukewenza ikizingatiwa kwamba nyimbo hizo nyingi ndio wanaozitunga. Wanawake wanaojaribu kupinga jambo hilo wanatungiwa nyimbo kama *Tutabanana Hapa Hapa* na wanaume kama Juma Machano kwa lengo la kuwakumbusha ni kwa nini wanastahili kukubali swala hilo. Mwanamke anayejaribu kukinza mahusiano kama haya anawenza kuepukwa na kutungiwa nyimbo za kumkejeli na hivyo atakuwa anatengwa na jamii.

2.2.4 Uasherati

Katika nyimbo hizi, wanawake na wanaume wasioridhika katika ndoa au uhusiano wa mapenzi hushambuliwa kwa kusutwa. Katika wimbo *Paka Mapepe*, mwanamke ambaye amejishindia mume wa mke mwenzake anamwambia mume huyo kwamba mke huyo aliyetotokwa ni mtu asiyetosheka tena hawezi kuaminika maanake anapenda wanaume wenye pesa. Hiki hapa kiitikio:

*Paka huyo paka paka mapepe paka
Umpe kuku na bata katu hatotosheka
Umpe japo steki huyo paka
Hatakushukuru huyo paka
Atakutoroka huyo paka
Akimwona panya huyo paka.*

Katika jamii hii na ya Afrika kwa ujumla, mwanamke ndiye anayesawiriwa kama mtu mwasherati kwa kuitwa majina kama vile malaya na kiruka njia. Itikadi ya ubabedume imetawala sana katika jamii hizi kiasi kwamba hata mwanamume anapokuwa na wapenzi wengi, sifa hiyo ya umalaya inahusishwa sana na wanawake. Kwa hivyo, nyimbo nyingi hujaribu kushambulia wanawake wanaokuwa na mpenzi zaidi ya mmoja lakini ajabu ni kuwa mwanamume ameruhusiwa kuwa na wanawake hadi wanne bila kusawiriwa vibaya ilhali mwanamke atasutwa. Mwanamume kama huyo mara nyingi husiwa kwa kupewa sitiari kama *simba* au *jogoo* ambazo ni kuonyesha uhodari wake katika mahusiano yake na wanawake. Hata hivyo katika wimbo *Zilipendwa*, mwanamke amemsawiri mwanamume kama mwasherati kwa kumuita *bakabakana* hivyo kutaka kukinza tabia kama hiyo miongoni mwa wanaume wanaoihalalisha huku wakiikemea miongoni mwa wanawake. Katika ubeti wa tatu anasema:

*Niliyajua kitambo, kama huyo baka baka.
Sasa kama kwako yuko, wengine anako anakokwenda.*

2.2.5 Masimango/Malumbano kati ya Wanawake

Masimango ni mojawapo ya mambo yanayotokea katika nyimbo za taarab. Masimango hayo hutumiwa kama njia ya kumdunisha mwanamke fulani ambaye anadhaniwa analeta ushindani wa mapenzi. Katika wimbo, *Utalijua Jiji*, mwimbaji anajisifu kuwa yeye ndiye bingwa wa mapenzi aliyetwaa mume wa mwenzake kwa sababu yeye anafaa kwa kila njia.

*Pokea chako kibomu shoga nakutumia
Hata ukinilaumu wako nishamchukua X 2
Penzi ulimdhulumu visa ukamfanyia
Chachanduvi tamu tamu wala hukumpatia X 2*

Mbinu kuu inayotawala katika masimango haya ni usambamba ambapo mwanamke anayetaka kuonekana bora anajiweka katika kundi fulani bora na kisha anamweka mwenzake katika kundi

baya na kutaka aonekane kama asiyefaa. Katika *Nani Zaidi* hili linajitokeza sana hata katika anwani yake ambapo mwanamke anayejiona bora kwa mwenzake anamuuliza nani zaidi katika ubora. Malumbano hayo yanahusu namna ya kumpata mwanamume na hivyo kinachoyasababisha ni itikadi ya ubabedume. Katika *Nani Zaidi* kwenye ubeti wa mwisho mwanamke huyo aneyejiona bora anasema:

*Mimi ndiye super beuty, ananipenda zaidi
Talakamimi sipewi kama kupewa ni wewe*

Katika Utalijua Jiji vilevile majigambo kama hayo yapo katika ubeti wa tisa:

*Usitake ushindani, hunishindi nakwambia
Mimi naletewa ndani wewe watanga na njia.*

Ushindani huo na ubishi vyote vinatokana na haja ya mwanamke mmoja kutaka kumpiku mwenzake ili aweze kupata mapendeleo kutoka kwa mwanamume. Pia unalenga kumdunisha mwanamke mwenzake na hata pengine kumwachia yule mume. Katika *Utalijua Jiji* kwa mfano, maneno yaliyo katika kibwagizo yanaweza kumkatisha mwanamke tamaa ya kumpata mume aliyepokonywa:

*Utamaliza mizizi, waganga na waganguzi,
Talasimu na hirizi, ongeza na vipodozi,
Kwake hupati nafasi, mimi ndiye yake pumzi.*

Ikizingatiwa kwamba ni mapambano ya wanawake kupata mume, inabidi mwanamke anayetaka kumpokonya mwenzake mume ajigambe kwa mambo anayoweza kufanya zaidi ya mwenzake kama vile kupika vyakula vitamu, kupendwa zaidi ya yule mwingine, kumpa mapenzi ya kumridhisha mumewe na zaidi ni urembo wa mwili. Yaelekea kwamba mwanamke mrembo sana na anayejua namna ya kumridhisha mumewe kitandani, yote haya yakiwa maswala ya kuendeleza ubabedume. Kinachojitokeza hapo basi ni kwamba mwanamke mwenye makalio

makubwa ndiye mwanamke bora zaidi ya mwenzake. Khadija Kopa katika wimbo wake *Kubali*

Matokeo anasema:

*Mwanamke nyonga, mwanamke kutingishika,
Kushikwa akashikika, mwanamke kuitika,
Bwana anapomwita, mwanamke kuvikata kata kata,
Mwanamke ninavikata katakata
Mwanamke nyonga, makalio majaliwa.*

Swala hilo la urembo wa mwili hutumiwa kama sumaku ya kumnasa mwanamume na hivyo basi mwanamke hujibidiisha kuhakikisha kwamba anajipodoa sana na anakuwa na makalio makubwa. Tabia ya wanawake wa sasa kwenda kufanyiwa upasuaji wa makalio leo hii katika bara la Afrika linatokana na swala zima hilo la kutaka kufurahisha wanaume ambao ndio huamua mwanamke wanayemtaka kwa kuorodhesha sifa za mwanamke mrembo na kwa sasa yule mwenye makalio makubwa ndiye anayetakiwa. Usawiri huu wa mwanamke kama mtu anayestahili kupigana na kulumbana na mke mwenzake kwa lengo la kumpata mume ni njia ya kumweka pembeni mwanamke katika mahusiano yake ya kijamii na hivyo kumfanya mwanamume mtu mwenye mamlaka au rasilimali muhimu ambayo wanawake wanapambana na kulumbana kiasi cha kukosna kwa lengo la kuipata. Ingawa wanawake ndio wanaolumbana sana kwa kushiriki katika masimango, wanaume pia husimangwa na waanwake. Na hatua kama hizi ni njia ya wanawake kujaribu kuyakinza mahusiano yao na wanaume kwa kuwaona kama wabaya na waovu vilevile. Katika wimbo *Zilipendwa*, mwanamke amemsimanga mwanamume aliyekuwa mpenzi wake kwa kumbeza kwa majina kama *bakabaka* kuonyesha yeye ni mwasherati na pia kwa kutumia sitiari kama punda, kondakta na karatasi katika ubeti ufuatao:

*Hapandi farasi mzoea punda
Noti si karatasi dereva si konda*

2.2.6 Wivu/ Chuki

Wivu /chuki ni swala lingine linalopatikana katika nyimbo hizi za taarab. Wivu huo hutokana na mafanikio ya mtu kisha akawa anaonewa wivu. Mara nyingi katika nyimbo hizo, wivu/chuki hutokana na malumbano miongoni mwa wanawake kujinyakulia waume wa watu. Katika wimbo, *Mtie Kamba Mumeo* uliyoimbwa na Khadija Kopa, anasema hivi katika ubeti wa tatu.

*Wenye chuki, na chuki zao
Wenye udhia, na udhia wao
Wakina nani?
Si hao waliopewa kazi
Kufuatilia ya wenzao
Lakini kwa hapa, watachoka wao*

Katika nyimbo hizi, wivu hutokea pale ambapo mwanamke fulani anampata mume kisha akawa anasemwa na wenzake hasa yule aliyekuwa na mume huyo kabla ya kuchukuliwa. Kwa hivyo, chuki katika nyimbo hizi ni zao la ubabedume ambapo mwanamume anakuwa chanzo cha wanawake wanaomtaka na wanaomkosa kugombana kama tulivyoona katika maudhui yaliyotangulia.

2.3 Hitimisho

Katika sura hii tumejadili utunzi wa nyimbo za taarab pamoja na maudhui yanayotawala katika nyimbo hizo. Kupitia kwa historia yake, tumeona kwamba nyimbo hizo zilitungwa mwanzo na wanaume na wanawake walikuwa waimbaji tena baada ya miaka fulani baada ya mwanzo wake kule Zanzibar. Wanaume wakitawala katika utunzi wa nyimbo hizo, tumeona kwamba itikadi ya ubabedume wanayotaka kuikuza na kuidumisha inatawala katika nyimbo hizo na si ajabu maudhui katika nyimbo hizo yanazungukia swala hilo zima. Maudhui hayo ya mapenzi, chuki, malumbano, ukewenza, umbea na mengineyo tumeona kwamba yanatokana na itikadi ya

ubabedume ambapo wanaume wanajipa nafasi kuu katika mahusiano yao na wanawake katika jamii. Inabidi wanawake wazue mikakati mbalimbali kama vile kusutana, kusengenyana na kuoneana wivu pamoja na kuonyesha uhodari wao wa kuwashughulikia wanaume ili wapate fursa za kujiendeleza katika maisha kwa vile kuhusiana na mwanamume vizuri kuna manufaa kwa mwanamke na hasa manufaa ya kiuchumi kama tutakavyoona katika sura ya tatu na hata ya nne. Katika sura ifuatayo tunachambua wimbo *Zilipendwa* ulioimbwana Khadija Yusuf kwa lengo la kubaini itikadi ya ubabedume inavyotokea na kuyafafanua mahusiano ya mamlakakwa kutumia michakato yakini, kiakili na kihusiano pamoja na kuchunguza lugha ya mafumbo ilivyotumika katika wimbo huo.

SURA YA TATU

MAMLAKA NA ITIKADI KATIKA WIMBO *ZILIPENDWA* ULIOIMBWA NA

KHADIJA YUSUF

3.1 Muhtasari wa Wimbo *Zilipendwa*

Wimbo huu umeimbwa na Khadija Yusuf akiwa katika bendi ya East African Melody kutoka Zanzibar. Wimbo huu unatumia sitiari ya *Zilipendwa* ambayo inakaribiana na *Zilizopendwa*; jina la aina za nyimbo za karne iliyopita za wanamuziki kama Issa Juma, Remmy Ongala, Daudi Kabaka, Fadhili Williams miongoni mwa wengine na makundi ya muziki kama Les Wanyika, Simba wa Nyika na mengineyo ambazo vijana au kizazi cha leo hakithamini sana kutokana na kutaka usasa. Mwanamke wa kwanza aliyetorokwa na mpenziwe kisha mpenzi huyo wa kiume akaenda kwa mwanamke wa pili, anafananishwa na nyimbo hizo za zamani ambazo kwa sasa hazina uzuri wala ubora wowote kwa kizazi cha leo. Mwimbaji anawakilisha sauti ya mwanamke wa kwanza aliyemtema mpenzi wake wa kiume kwa sababu ya kutokuwa mwaminifu katika uhusiano. Anamweleza mwanamke wa pili ambaye amependwa na mpenzi wake huyo wa zamani kujitahadhari naye maana haaminiki. Ila kwa upande wake, ashapata mpenzi mwingine anayemthamini na hivyo mwanamke wa pili aliyemchukua mpenzi wake wa zamani asiogope kutembea naye maana hana haja naye tena.

Katika wimbo huo, kuna mahusiano ya aina nne. Kwanza ni uhusiano kati ya mwanamkewa kwanza na mwanamke wa pili. Mwanamke wa kwanza anamshauri mwenzake kujitahadhari na mwanamume huyo kwa sababu si mtu wa kuaminika katika mahusiano yake na mwanamke. Kisha kuna uhusiano kati ya mwanamke wa kwanza na mwanamume aliyekuwa mpenzi wake. Uhusiano huo japo ulikwisha, ni muhimu sana hasa katika kueleza namna mwanamke

anavyoweza kumsawiri mwanamume katika jamii kwalugha ya mafumbo kama vile kumwita *zilipendwa* na *bakabaka*. Uhusiano mwingine ni kati ya mwanamke wa kwanza na mpenzi wake mpya ambaye katika wimbo huu anamsawiri vizuri kama wa kuaminika, mwenye umbo zuri na sifa nyingine muhimu za mume. Mwisho kuna uhusiano kati ya mwanamke wa pili na yule mwanamume aliyeachwa na mwanamke wa kwanza. Kupitia kwa malumbano, masuto na aina za mahusiano yaliyo katika wimbo huu, inabainika kwamba yanazungukia maswala ya mamlaka na itikadi na hivyo kwa kutumia michakato yakini, kiakili na kihusiano pamoja na kuchanganua lugha ya mafumbo, maswala hayo yanaweza kufafanuliwa.

3.2 Mamlaka na itikadi katika wimbo *Zilipendwa*

Mamlaka ni kipengele muhimu sana katika DCT. Katika nadharia hiyo, diskosi yoyote ile katika jamii hudhihirisha mahusiano ya mamlaka katika jamii maana kama anavyosema Foucault, M (1977), mamlaka yapo kila mahali na hupatikana katika mitagusano yote ya kijamii. Kulingana na Fairclough, N. (1989), lugha ni chombo muhimu katika utoaji, udumishaji na ubadilishaji wa mahusiano ya mamlaka katika jamii. Lugha kikiwa chombo cha kudhibiti watu fulani katika jamii (Fairclough, 1989:1), ni muhimu kuchunguza lugha katika matini za nyimbo za taarab ili kubaini namna mahusiano ya mamlaka yanavyojidhihirisha na kuonyesha kundi linalodhibiti lingine. Itikadi kwa upande wake ni mseto wa maadili na imani zenye uthabiti na mshikamano katika jamii. Fairclough, N. (1995) anasema kwamba itikadi ni njia muhimu ya kuanzisha na kudumisha utousawa wa mahusiano ya mamlaka. Lugha kwa hivyo ni zao la itikadi maana mazungumzo yoyote huongozwa na itikadi zilizopo katika jamii. Masiala haya yanajitokeza katika matini ya wimbo *Zilipendwa* na hivyo ni vizuri kuchanganua mahusiano ya mamlaka katika wimbo huo kwa kutumia michakato ya uelekezi kulingana na Halliday, M.A.K. (2014).

3.2.1 Mchakato Yakini

Katika sura ya kwanza sehemu ya 1.8 tulieleza dhana ya uelekezi na michakato sita ya uelekezi kwa mujibu wa Halliday, M.A.K. (kama hapo juu). Mchakato yakini tulishaeleza kama mchakato ambao kitenzi katika kishazi kinaonyesha ufanyaji na utukiaji wa kitendo. Kunakuwa na kitendo hicho kutokana na juhudi za mmoja wa Washiriki. Mshiriki/Mtendaji hutumia nguvu zake au juhudi kutekeleza kitendo hicho kisha kuna mpokezi (Lengo) wa kile kitendo au anayeathiriwa kutokana na utokeaji wa kitendo hicho.

Mchakato yakini ni muhimu katika kueleza mahusiano ya mamlaka kwa sababu Mtendaji katika mchakato huu hutumia nguvu au juhudi zake kuweza kutekeleza kitendo kinachoathiri Lengo. Mtendaji katika mchakato huu huwa na mamlaka makubwa kwa Lengo akilinganishwa na Mtendaji katika michakato mingine. Vitendo ambavyo Mtendaji wa mchakato huu huvitenda huwa vya kuonekana kama vile kupiga, kuchukua, kujenga, kukata, kufunga, n.k. Lengo kwa upande wake katika mchakato huu hana mamlaka. Lengo na Mtendaji huwepo iwapo kitenzi elekezi ambacho kinahitaji yambwa kinatumika. Mfano: *Nimemtapika sinahamu tena*. Kitenzi hicho kilichopigiwa mstari ni elekezi. Mtendaji ni msemaji (mwanamke) aliyemfurusha mpenzi wake wa kiume wa zamani aliyewakilishwa na mofu {ni} ya nafsi ya kwanza umoja ilhali mpenzi huyo wake wa zamani ndiye Lengo na amewakilishwa na mofu {m}. Ila katika kitenzi kisoelekezi, huwepo tu na Mtendaji na wala hakuna Lengo maana vitenzi elekezi hukamilika kimaana bila kuhitaji yambwa. Mfano: *Sijanuna sijakereka, vitendo vyake vilinitosha*. Katika mfano huo, mchakato yakini katika kitenzi *sijanuna* una Mtendaji aliyewakilishwa na mofu kapa ya umoja katika hali ya ukanushi, mwanamke aliyemtema mpenzi wa zamani ila hakuna Lengo.

Ifuatayo sasa ni mifano ya michakato yakini katika wimbo *Zilipendwa* ambayo inatuwezesha kufafanua mahusiano ya mamlaka katika jamii. Mfano wa kwanza ni katika ubeti wa kwanza:

*Zilipendwa zilipendwa sina haja naye tena.
Nimemtapika sina hamu tena.*

Katika kishazi kilichopigiwa mstari kuna mchakato yakini. Michakato yenye maana sawa na huu pia ipo katika ubeti wa mwisho:

*Zilipendwa kwangu zilipendwa, "long time" nimemfurusha...
Jeuri mwenzio kusudi, hutaki mwenziwe basi.
Sina haja ya shahidi, si mfupi si mzazi.
Nishamtoa moyoni.*

Mtendaji ni mwanamke ambaye ameonyesha uwezo wake wa nguvu za mwili au uwezo fulani wa kumtimua au kumwondoa mpenzi wake katika uhusiano wao. Katika mifano hiyo, mwanamke ni Mtendaji wa mchakato yakini na hivyo ana mamlaka makubwa kwa mwanamume aliyefurushwa, kutapikwa au kukataliwa ambaye ndiye Lengo. Mwanamke ameonyesha uwezo wa kufanya jambo ambalo katika jamii ya Waswahili au Kiafrika kwa ujumla sio la kawaida. Gramci, A. (1971) anasema kwamba kuna wakati ambapo kundi lenye mamlaka hulidhibiti lile lisilo na mamlaka katika jamii kupitia kwa mfumo wake wa mawazo na utawala (hejemoni), kundi linalotaliwa vile vile hujaribu kukinza udhibiti huo kwa kutaka kujikomboa kwa kuzua hejemoni kinzani. Mifano hii basi ni muhimu sana kuonyesha harakati za wanawake za kubadilisha mahusiano ya mamlaka katika jamii ambapo mwanamume kutokana na utamaduni na mihimili ya dini ya Kiislamu katika muktadha ambao wimbo huu umezaliwa amepewa uwezo wa kuwa na wake (wanne kwa mujibu wa dini ya Kiislamu). Tukizingatia maoni ya Foucault, M. (1977) kuwa mamlaka yanaweza kutoka upande wowote wa kundi linalotawala au kutawaliwa, mifano hii basi inaonyesha kuwa wanawake ambao hugandamizwa na itikadi ya

ubabedume wakawa watu wa kutumiwa na kutupwa na wanaume wameanza kukinza hali hiyo na hivyo kuibua mahusiano mapya ya mamlaka. Itikadi ya ubabedume ambapo wanaume kama Makuu katika riwaya ya *Utengano* ya Mohamed, S.A. (1980) anasema “*Sikiliza, dunia hii hayendi bila ya pesa. Unapokuwa ukii... unapokuwa kiongozi piga kelele. Taja kila kitu lakini unapopata nafasi ya kula, kula! Na mwanamke mwepesi wa kuliwa*” (uk.12) na hivyo kumwona mwanamke kama “kitu” cha kuliwa na wanaume watakavyo inakinzwa katika mchakato yakini tulioutoa.

Mchakato yakini mwingine upo katika ubeti wa pili:

*Sikuambiwa yupo nimeambiwa wako.
Kama umemchukua saizi yako.*

Katika kitenzi kilichopigiwa mstari, mwanamke anayeambiwa maneno haya ndiye aliyependa mpenzi wa kiume wa zamani wa msemaji katika wimbo huu. Hivyo, anayeambiwa katika mchakato huu ndiye Mtendaji na mwanamume huyo ndiye Lengo. Katika mchakato huu, mwanamke bado anazidi kusawiriwa kama mwenye mamlaka katika mahusiano yake ya mapenzi na mwanamume. Anaweza kumchukua mwanamume anayemtaka na pengine kumtema akitaka kwa hiari yake. Mwanamume katika muktadha huu hana uwezo wa kujiamulia anayemtaka ila mwanamke ndiye huamua mwanamume amtakaye. Japo, kauli hii huenda kwa ujumla iwe ni bezo kutokana na matumizi ya maneno kama vile *saizi yako* yanayoonyesha kuwa msemaji amejitokea katika kiwango au hadhi tofauti na msikilizaji wake, mchakato mzima unadhihirisha uwezo alionao mwanamke katika mahusiano yake na mwanamume.

Katika ubeti wa nne kuna mishororo ifuatayo:

*Hapandi farasi mzoea punda.
Noti si karatasi dereva sikonda.*

Mshororo wa kwanza ndio ulio na mchakato yakini kama tulivyopigia mstari kitenzi husika. Kitenzi *hapandi* ni mchakato yakini ambapo Mtendaji sio bayana lakini aweza kuwa mwanamke aliyemtwa mpenzi wa kiume wa mwenzake. Mpenzi wa sasa wa mwanamke huyo amelinganishwa na punda huku mpenzi wa anayemwambia maneno haya, mwanamke mwenzake aliyemkataa mpenzi huyo wa zamani akilinganishwa na farasi. Ulinganishaji huu wa mnyama mwenye thamani tofauti kwa kutumia kitenzi cha mchakato yakini katika kinyume unaonyesha kwamba uzuri au thamani na hivyo mamlaka ya wapenzi wa wanawake hawa ni tofauti. Muhimu pia katika kauli hii ni kwamba mwanamke ambaye ndiye mwimbaji wa wimbo huu ana uwezo wa kutumia lugha kuwasawiri wahusika katika jamii kulingana na mahusiano yao. Mwanamke ana uwezo wa kukweza wanaume akawaona kama farasi (watu wenye uzuri/thamani) na wengine akawasawiri kama punda (watu duni). Kauli hii hivyo basi ni kejeli kwa mwanamume, mpenzi wa zamani wa msemaji kuonyesha kwamba yeye si kitu cha thamani muhimu.

Kuna michakato yakini mingine katika ubeti wa sita:

*Na wala sitowafuata, awe wako uwe wake.
Yupo alonifumbata alofanya niridhike.
Msijibanze na kuta kivyangu yeye kivyake.*

Mchakato yakini wa kwanza ni *sitowafuata* ambapo Mtendaji ni mwanamke, mpenzi wa zamani wa mwanamume aliyempenda mwanamke mwingine. Lengo hapa ni watu wawili: mpenzi wa kiume wa zamani wa Mtendaji na mpenzi wake wa kike anayeambiwa maneno haya. Mtendaji hapa ana mamlaka ya kutumia dhamira agizi katika hali ya kinyume kuonyesha hana haja na kumfuatilia mpenzi wake wa zamani kujua anavyoendelea. Mwanamke katika kauli hii anaonyesha kwamba ni mwenye msimamo thabiti na maamuzi yake hayajutii. Sio mtu wa kutaka kufanya uamuzi akajutia. Msimamo kama huu wa mwanamke unaweza kulinganishwa na wa Lanina katika *Kilio cha Haki* (Mazrui, A. 1989) au Natala katika *Natala* (wa Mberia, K. 1997)

anayekataa kudhibitiwa na mfumo wa ubabedume. Katika mchakato yakini wa pili, *Yupo alonifumbata*, Mtendaji hayuko bayana ijapo katika muktadha huu ni mpenzi mpya wa mwanamke aliyemtema mpenzi wa zamani ilhali mwanamke huyo ndiye lengo. Kufumbata ni kushika katika kiganja na kukikunja, kushika kwa nguvu kwa mkono (Kamusi ya Karne ya 21, 2011:107). Katika mchakato huu, Mtendaji ambaye ni mwanamume amepewa uwezo wa kumtia mwanamke katika udhibiti wa aina fulani kiasi kwamba hana uhuru wowote maana kitu kinapofumbatwa hakina uwezo wa kujiondoa katika mikono ya aliyekifumbata isipokuwa kwa hiari ya aliyekifumbata. Hivyo basi, mchakato huu unampa mwanamume uwezo wa kumdhibiti mwanamke na kumfanya atakavyo. Lakini hii haina maana kwamba siku zote katika mahusiano ya mamlaka katika diskosi ya nyimbo za taarab mwanamume ndiye anayetawala katika mahusiano yake na mwanamke. Tayari tumeona hilo katika baadhi ya mifano hapo juu. Katika wimbo *Mtie Kamba Mumeo*, mwanamke anaonyesha kwamba ana uwezo wa kumdhibiti mwanamume akawa haendi popote. Anakuwa kama kitu kilichonaswa kwenye gundi ambacho kinaweza kuondolewa tu kwa hiari ya aliyekinasa. Katika ubeti wa nne wa wimbo huo, maneno yafuatayo yametumika:

*Bwana huyu kanigandia mie,
Wala hanipi pumzi.*

Mwanamke katika mchakato huo yakini anaonyeshwa kuwa ameteka makini ya mumewe kwa kila hali na hivyo anaweza kumfanya lolote.

3.2.2 Mchakato wa Kiakili

Kama nilivyotanguliza katika sehemu ya 1.8 katika sura ya kwanza, huu ni mchakato wa kuhisi. Kwa mujibu wa Halliday, M.A.K. (2014:197), kishazi cha “kiakili” kinahusu utendekaji

wa matendo unaotokea katika ung'amuzi wa mtu binafsi. Hivyo basi, huwa kuna Mhisi ambaye anahisi na Finomena ambacho ndicho kitu au mtu anayeelekezewa hisia hizo. Finomena ni mtu au kitu kinachohisiwa, kufikiriwa au hata kutakiwa. Mchakato huu unahusu utambuzi wa wasemaji katika lugha kuhusu ulimwengu wao wa ndani na nje, unatumika kujenga utambulisho, imani, misimamo na itikadi.

Katika wimbo *Zilipendwa* ifuatayo ni michakato ya kiakili. Kwanza ni katika ubeti wa tatu:

Niliyajua kitambo, kama huyo bakabaka.

Sasa kama kwako yuko, wengine anao anakokwenda.

Kuna mchakato wa kiakili katika kitenzi *niliyajua* ambapo msemaji ambaye pia ndiye Mhisi ni mwanamke aliyemtema mpenzi wake wa zamani wa kiume katika uhusiano wake ilhali Finomena ni mambo aliyoyajua kuhusu mpenzi huyo kwamba si mwaminifu katika mahusiano yake. Kwa kutumia kitenzi katika njeo iliyopita, Mhisi anatumia mbinu ya kihistoria kama anavyopendekeza Wodak, R. (2001) kama njia ya kuelewa mambo yanayotokea sasa. Hivyo basi mwanamke amesawiriwa kama mtu mwenye utambuzi wa kuelewa mazingira yake na uhusiano wake na mpenzi wake na wala sio mtu wa kuhadaiwa na porojo za mwanamume. Japo ni mchakato wa kiakili ambao hauonyeshi uwezo wa mamlaka kati ya Mhisi na Finomena kama ilivyo katika Mtendaji na Lengo katika mchakato yakini, Mhisi hapa anadhihirisha uwezo fulani kwamba anafahamu ukora na ujanja wake mwanamume huyo. Alijua kuwa mpenzi wake huyo wa zamani sio mwaminifu na amemwita jina "bakabaka" na pia kusema kuwa "wengine anao anakokwenda". "Wengine" katika muktadha huo ni wanawake anaohusiana nao kando na yule aliye naye. Hivyo basi, Mhisi katika mchakato huu ambaye ni mwanamke anadhihirisha kwamba wanaume ni watu wasioaminika katika mahusiano yao ya mapenzi na wanawake. Uelewa wake

wa wanaume unachangia kujenga imani ya wanawake kuhusu wanaume na hivyo kuonyesha itikadi inayotawala katika jamii yao.

Katika ubeti wa tano wa wimbo huu, kuna mchakato mwingine wa kiakili:

*Kama huko ndio kupata, chukua ufaidike.
Halafu usije juta, ukifika mwisho kwake.*

Mchakato wa kiakili upo katika kitenzi kilichopigiwa mstari. Mhisi katika mchakato huu ni mwanamke aliyechukua mpenzi wa zamani wa msemaji ambaye anampa ushauri kuhusu mpenzi huyo wa zamani. Finomena ni *ukifika mwisho kwake*. Msemaji anaonyesha kwamba Mhisi awe na tahadhari kuhusu uhusiano wake na mwanamume aliyekuwa mpenzi wake kwa sababu atakuja kuathiriwa kiakili kwa kujutia uhusiano huo. Pia ana hakika kwamba uhusiano huo utakuja kufika kikomo maana mwanamume huyo kama alivyoitwa kwa sitiari *bakabaka* si mtu wa kuaminika. Kupitia kwa utambuzi wa mambo kama haya, mwanamke anaonyeshwa kwamba ni mtu anayefahamu tabia za wanaume katika jamii yake ila yeye hawezi kukubali kutumiwa hivyo. Na pengine kwa tahadhari kama hii kwa mwenzake wa kike, huu waweza kuwa mkakati wa kupambana na hadaa za wanaume kwa wanawake. Kama Askew, K.M. (2002) na Fair, L. (2001) wanavyosema, nyimbo za taarab zinatungwa kwa lengo la kuwa matukio ya kijamii ambayo wanawake kama “watunzi” hujiingiza katika mijadala ya kujaribu kubadilisha maswala kama ya utabaka, jinsia na mahusiano ya kijamii pamoja na kuingiza uelewa wao na wa kijamii katika nyimbo hizo wanazozimba kama kauli za kibinafsi kuhusu maadili na mahusiano. Mfano huo wa mchakato wa kiakili unaafiki sana kauli hii ya wataalamu hawa. Ni mchakato unaokinza chukulizi za wanaume kuwaona wanawake kama malaya kana kwamba wao hujiingiza katika tabia hiyo peke yao. Kwa kumuita mwanamume huyo *bakabaka* mwanamke anaonyesha namna

anavyomwona mwanamume wa aina hii na hivyo anabomoa mtazamo na chukulizi za kumwona mwanamke kama mwasherati bila kumhusisha na mwanamume mwenye tabia iyo hiyo.

Pia kuna mchakato mwingine wa kiakili katika ubeti wa sita:

*Na wala sitowafuata, awe wako uwe wake.
Yupo alonifumbata alofanya niridhike.
Msijibanze na kuta kivyangu yeye kivyake.*

Mchakato huo wa kiakili, *niridhike*, umefungamana na ule yakini *alofanya*. Hapa, mpenzi wa kiume wa sasa ndiye mwenye mamlaka kwa sababu kwa kushiriki katika mchakato yakini kama Mtendaji na mwanamke huyu kama Lengo, anasababisha athari ya kiakili kwa mwanamke huyo. Uridhikaji huu una maana fiche ya kuonyesha kwamba mwanamke huyu anatoshelezwa kimapenzi na mumewe. Mwanamke hapa bila kujua, anaendeleza itikadi ya ubabedume ka vile kulingana na DCT, itikadi wakati mwingine huendelezwa bila ung'amuzi wa wanaoendeleza wanaoichukulia kama jambo la fahiwa ya kawaida (Fairclough, 1989:77). Kauli hii ni sawa na kauli ya mhusika Kaloo katika *Kifo Kisimani* (wa Mberia, 2000:3) anayesema: *Wanawake wa Butangi wasipomkatikia Mtemi, wamkatikie nani?* Katika kauli hii sawa na ile ya msemaji kusema anafanywa aridhike na mwanamume, mwanamke anaiendeleza itikadi ya ubabedume pasi kuwa na ufahamu huo. Anaonyesha kwamba kuridhika kwake kunategemea uwepo wa mwanamume sawa na Kaloo anayeamini kuwa wanawake hawawezi kucheza ngoma bila ya kuwa wanamchezea Mtemi Bokono ambaye ni mwanamume.

Isitoshe kuna mchakato wa kiakili mwingine katika ubeti wa tisa:

*Nimeshapata mwingine, nampenda peke yake.
Si mwembamba, si mnene aloshiba kwa mamake.*

Katika mchakato huo,Mhisi ni mwanamke aliyepata mpenzi mpya wa kiume ilhali Finomena ni mwanamume huyo.Ingawa hakuna uhusiano wa moja kwa moja ambao Mhisi anadhihirisha kwa Finomena,mchakato huu umeonyesha kuwa mwanamke ana mamlaka kwa kuzingatia mchakato yakini uliotangulia kwamba *nimeshapata mwingine*,ambapo ina maana kwamba mwanamke anaweza kujitafutia mpenzi anayemfaa kisha akampenda huyo pekee. Mwanamke pia anasawiriwa kama mwaminifu katika mahusiano ya mapenzi na mwanamume tofauti na mpenzi wake wa kiume wa zamani ambaye kila anapokwenda anajiingiza katika uhusiano wa mapenzi na mwanamke.Kwa njia moja au nyingine,mwanamke anajiheshimu na hayuko tayari kutumiwa na mwanamume yeyote kama chombo cha kumfurahisha.

3.2.3 Mchakato wa Kihusiano

Tulikwisha tanguliza mchakato huu katika sura ya kwanza pia katika sejemu ya 1.8 kwa kusema ni mchakato wa kuonyesha hali ya kuwa, hali ya kuwa na, na kuwa mahali (Halliday, M.A.K.: 2014:210). Huonyesha uhusiano kati ya watu au vitu viwili.Vitenzi vinavyoonyesha mchakato huu ni vitenzi vya kuwa, kuwa na na vya kuwa mahali kama *vileni, kuwa,n.k*.Vitenzi hivyo huwa katika njeo iliyopo na iliyopita.Katika mchakato huu kuna mshiriki wa kwanza ambaye ni Mbebaji na ndiye mwenye sifa, uhusiano au kuwa mahali fulani.Pili kuna mshiriki wa pili aitwaye Sifa ambaye huwa ni sifa inayohusishwa na Mbebaji, mahali aliko au uhusiano unaotaka uonyeshwe. Halliday (kama hapo juu) anasema kwamba mchakato huu ni muhimu kueleza sifa za watu pamoja na kuwatambulisha.

Ifuatayo ni mifano ya mchakato wa kihusiano katika wimbo zilipendwa:

*Zilipendwa zilipendwa sina haja naye tena.
Nimemtapika sina hamu tena.*

Katika ubeti huu wa kwanza, matumizi ya kitenzi cha kuwa katika hali ya kinyume, *sina*, yanaonyesha sifa za Mbebaji katika mchakato huu ambaye ni mwanamke aliyemkataa mpenzi wake wa zamani na kumchukua mwingine. Kwa kusema hana haja naye tena na pia hana hamu tena na mpenzi huyo wa zamani anadhihirisha kuwa ni mwenye msimamo thabiti na maamuzi yake hawezi kuyasikitikia. Na hilo analisisitiza kwa kutoa ithibati ya ni kwa nini hamtaki mpenzi huyo wa zamani kupitia kwa mchakato mwingine wa kihusiano anaposema:

*Na mimi tayari mwingine ninaye.
Wasiwasi sina ooh yahe.*

Katika mchakato huo, Mbebaji bado ni huyo mwanamke na Sifa ni mwanamume mpya aliyempata aliyewakilishwa na mofu {ye} katika kitenzi *ninaye*. Katika diskosi hii yote, mwanamke kando na kuonyesha kuwa ana msimamo thabiti katika mahusiano yake na mwanamume pia anaonyesha kuwa ni mtu anayeweza kujitafutia mwanamume anayemthamini na kumpenda na wala sio wa kumwona kama kinyago tu cha kutumiwa na kutupwa.

Pia kuna mchakato mwingine wa kihusiano katika ubeti wa tisa:

*Nimeshapata mwingine, nampenda pekee yake
Si mwembamba si mnene aloshiba kwa mamake.*

Matumizi ya vitenzi, *si*, ambavyo ni vitenzi vya mchakato wa kihusiano katika hali ya kinyume yanaonyesha sifa za mpenzi mpya wa kiume wa msemaji ambaye ni mwanamke. Ametumia kikanushi hicho kuonyesha kuwa mpenzi wake ana umbo la kadri na ambalo ni zuri kwa mwanamume. Zaidi ni kwamba kinachojidhihirisha katika matumizi ya maneno hayo katika mchakato huu ni kuwa wanawake pia wanaweza kujichagulia wanaume ambao wanavutia na

wanaowatosheleza kingono maana kwa tathmini ya wanawake, wanaume wembamba kupindukia au wanene wanaweza kushindwa kutekeleza majukumu ya kitandani na mengineyo ipasavyo.

Isitoshe kuna mchakato mwingine wa kihusiano ambapo mwanamke aliyemchukua mpenzi wa zamani wa msemaji amelinganishwa na *limbukeni* katika ubeti wa kumi:

*Nichanganyie, nichekicheki.nachichitiza na mtu unatisha.
Hujatulia, hujapepewa, u limbukeni unachekesha.*

Mke wa pili aliyemtwa mpenzi wa zamani wa mke wa kwanza ndiye Sifa (*limbukeni*) na pia Mbebaji (*u* ambacho ni kitenzi cha kuwa *wewe ni* katika ufupisho).Mke wa kwanza ambaye tayari ametengana na mumewe wa zamani anadhihirisha kuwa na mamlaka zaidi kwa mke wa pili jinsi anavyotumia lugha kumsuta.Hapa Mbebaji anahusishawa na Sifa ya *limbukeni* ambayo kwa mujibu wa Kamusi ya Kiswahili Sanifu ya TUKI (2014:287) ni mtu anayeanza kutumia au kupata kitu kwa mara ya kwanza. Japo Mbebaji amesutwa na hivyo katika muktadha huu kudunishwa na mwanamke mwenzake aliye na mamlaka kumzidi,suto hili ni nasaha anayostahili kuitumia kama silaha katika harakati za kukinza tabia za wanaume wanaowatumia wanawake wanavyotaka bila jamii kuwashtumu kwa sababu jamii yenyewe ina misingi wa ubabedume.Hii ni njia ya wanawake kukinza mamlaka ya wanaume katika mahusiano yao na wanawake hasa wanapokuwa wanawatuimbia wanawake kama vyombo vya ngono kisha kuwatema na kuwaendea wengine.

3.2.4 Lugha ya mafumbo katika wimbo *Zilipendwa*

Nadharia ya DCT kulingana na Fairclogh,N. na Wodak, R. (1997) ina mhimili wake mkubwa katika madai kuwa lugha ni tendo la kijamii na kwa vile lugha ni chombo kinachobeba itikadi

(Fairclogh,N. (1989) ni vyema kuchunguza matumizi ya lugha ya kimaafumbo katika wimbo huu ili kubaini itikadi fiche. Matumizi ya istiari na jazanda ni makubwa sana katika nyimbo za taarab. Jazanda naistiari hizo kama Timammy, R. (2002: 82) anavyosema ni kwamba hata Waswahili wenyewe wanaweza kukosa kuelewa maana zake kwa sababu ya uzito wake wa maana.Pasi na watu kujua matumzi ya istiari hizo kwa vile watunzi watasema ni mbinu ya tasfida ya kuepuka kutumia lugha ya matusi, matumizi ya mbinu hizi hukuza, hudumisha na kuendeleza itikadi fulani katika jamii ya Waswahili pamoja na kujenga utambulisho wa watu katika jamii.

Jina la wimbo wenyewe ni la kimaafumbo.Istiari hii ya *Zilipendwa* kama tulivyosema hapo awali katika sehemu ya 3.1 ni kwamba inalinganisha mpenzi wa zamani wa mwanamke wa kwanza na nyimbo za zamani wakati wa wanamuziki kama Daudi Kabaka na Remmy Ongala.Istiari hii inayotumiwa na mwanamke wa kwanza inalenga kuonyesha kuwa mpenzi wake wa zamaniamepitwa na wakati.Ni mpenzi ambaye hamwafiki kwa sasa maana wana mitazamo tofauti kuhusu maisha na hata ashampata mpenzi mpya wa “kisasa”.Kuna istiari nyingine katika kauli: *kama umemchukua saizi yako* katika ubeti wa pili.Kauli hii ni bezo kutoka kwa mwanamke wa kwanza kwa mwanamke wa pili anayeambiwa kuwa ndiye anayemstahili yule mpenzi wake wa zamani.Kwa kusema hivyo, ana maana kwamba hadhi yake na mtazamo wake kuhusu maisha na uhusiano na mwanamume yule ni tofauti na ulivyokuwa hapo awali.Tabaka lake au nafasi yake kama mwanamke katika mahusiano yake na mwanamume imebadilika.Hilo linadhihirika zaidi anapotumia jazanda ya *farasi* na *punda* na ya *dereva* na *makanga* kulinganisha yeye na mwanamke mwenzake katika ubeti wa nne anaposema:

*Hapandi farasi mzoea punda.
Noti si karatasidereva si konda.*

Ulinganishaji huu unanuia kumsawiri au kumtambulisha mwanamke wa pili kama mtu duni akiwa pamoja na mpenzi wake kwa vile wanalinganishwa na *punda*, *karatasi* na *makanga* vitu au watu wa hadhi ya chini wakilinganishwa na *farasi*, *noti* na *dereva*. Mwanamke wa kwanza pia anatumia lugha kama nyenzo ya kuonyesha anavyowaona baadhi ya wanaume wasiowaheshimu wanawake kwa kuwasawiri kwa njia ya kuwadunisha na huu unakuwa mkakati wa kuweza kuhamasisha wanawake wengine kuhusu haja ya kutathmini mahusiano yao na wanaume katika jamii. Ili kufanya hilo liwe bayana zaidi, mwimbaji pia ametumia istiari ya *bure ghali* (ambayo pia ni methali) kuonyesha kuwa mpenzi wake huyo wa zamani si kitu mbele yake hata kidogo. Hivyo basi, mwanamke anatumia lugha ya kimafumbo kuweza kuonyesha kukerwa kwake na tabia za baadhi ya wanaume katika jamii na kwa kumsawiri anavyomsawiri inaonyesha kwamba anapinga tabia za wanaume kama hao na kuonyesha mahusiano mapya ambapo mwanamke anaweza kujifanyia maamuzi yake kuhusu uhusiano wake na mwanamume ikiwemo kumtema na kuchukua mwingine na pia kumdhalilisha hadi akaonekeana kuwa si kitu kinyume na kawaida ilivyo ambapo mwanamume siku zote katika jamii hii huwekwa mbele.

Kumetumika pia istiari ya malighafi katika kibwagizo cha wimbo huu:

Mwenyewe nawatengeza, shoga sina shida hiyo.
Malighafi nimejaza, haihitaji tochi hiyo.

Mwimbaji anapotaja *malighafi*, anaonyesha makalio yake na hivyo malighafi katika muktadha huu ni makalio ya mwanamke. Sitiari hii inamwonyesha mwanamke kama mtu ambaye anategemea ukubwa wa makalio yake kama nyenzo ya kumpata mwanamume na hata mahusiano yao yanategemea sana sehemu hiyo ya mwili. Kinachodhihirika basi ni kwamba itikadi ya ubabedume imetawala kiasi kwamba wanawake wamefanywa na wanaume ambao ndio wenye

kudhibiti mahusiano kati yao na wanawake katika jamii kwa kiwango kikubwa, kuamini kwamba mwanamke mzuri ni mwenye sifa nzuri kadhaa mojawapo ikiwa ni makalio makubwa. Wanawake hivyo basi, kwa kujua au kutojua, wanaendeleza ubabedume kwa kukubali kuwa uhusiano wao na wanaume unategemea ukubwa wa makalio yao. Mwanamke anasawiriwa kama chombo cha kumridhisha mwanamume kingono na huenda akiwa na umbo dogo la makalio ataachwa na mwanamume. Kuthibitisha kauli hiyo, katika wimbo uo huo, kuna ubeti unaosema; *Nimeshapata mwingine, nampenda peke yake*

*Si mwembamba si mnene aloshiba kwa mamake.
Nalicheza shebene shibe yangu shibe yake.*

Kucheza *shebene* hapo ni lugha ya tasfida yenye maana ya kushiriki ngono. Tunaona kwamba itikadi ya ubabedume imeathiri hata mikondo ya mawazo ya mwanamke na kumfanya kufikiri kwa njia watakayo wanaume. Ndio sababu Althusser, L. (1971) na Fairclough, N. (1989) wakasema kwamba mamlaka ya watu wanaotawala katika jamii (vyombo vya dola), huwafanya watu hao kuathiri hata mikondo ya mawazo ya watu wanaotawaliwa hata wasipotumia nguvu ila kutumia vishawishi vinavyoathiri mionoulimwengu, imani na mitazamo yao.

3.2.5 Hitimisho

Katika sura hii, tumechanganua maswala ya mamlaka na itikadi katika wimbo *Zilipendwa* iombwa na Khadija Yusuf. Tumeona katika wimbo huo mwanamke wa kwanza akimsuta mwanamume (mpenzi wake wa zamani) kwa kumwita majina ya kumdharau na kumdhalilisha kama vile *bakabaka* na *zilipendwa* ambayo yana maana fiche. Vilevile, tumeona mwanamke wa kwanza akimsifu mpenzi wake mpya kwa kusema alivyo na sifa za mwanamume

bora.Halikadhalika tumeona mwanamke huyo wa kwanza akimwonya kuhusu tabia za mpenzi wake kwa vile anajua tabia zake.

Kutokana na uchunguzi wetu kwa kutumia michakato yakini, kiakili na kihusiano pamoja na kueleza lugha ya mafumbo iliyotumika katika wimbo huo, tumebaini kwamba wimbo unadhihirisha maswala ya mamlaka na itikadi. Tumebaini kuwa matumizi ya lugha ya mafumbo ni mikakati ya kipragmatiki ambayo imetusaidia kugundua kupitia kwa michakato hiyo mitatu kwamba kwa kiwango kikubwa wimbo huo unahusu harakati za wanawake kuonyesha mapambano yao katika jamii iliyotawaliwa na itikadi ya ubabedume. Mwanamke katika wimbo huu ameonyeshwa kama Mtendaji ilhali mwanamume amekuwa Lengo hasa kwa kujikita kwa mchakato yakini ambapo matendo yake kama vile kumfurusha mpenzi wake yameonyesha mamlaka aliyo nayo.Hata katika mchakato wa kiakili,mwanamke kama Mhisi ameweza kuonyesha kwamba anayaelwa mambo yanayofanyika katika mazingira yake na uwezo wa kutambua pamoja na kubashiri mambo yanayomhusu.Uwezo huo unamfanya mwanamke kusawiriwa kama mhusika mwerevu na anayejua anachostahili kupata katika mahusiano yake na mwanamume.Hata katika mchakato wa kihusiano,mwanamke ameonyeshwa kama anayeweza kumsawiri mwanamume kwa njia ya kumdunisha na kumdhalilisha swala ambalo linabomoa itikadi ya ubabedume inayomkweza sana mwanamume.Uchanganuzi wa lugha ya mafumbo katika wimbo huu vilevile umeonyesha kwamba mwanamke kwa kutumia lugha ya mafumbo ambayo ina mafungamano makubwa na mchakato wa kihusiano,amemsawiri mwanamume kwa njia hai ya kumdhalilisha kwa kumwita majina kama *zilipendwa*, *punda*, *karatasi* na *bakabaka*. Tumeona kwamba uhusiano kati ya mwanamke na mwanamume unakitwa kwenye itikadi ya ubabedume ambayo humpa mamlaka mengi mwanamume. Hata hivyo, katika wimbo

huu,mwanamke amejaribu kukinza udhibiti wa mwanamume kwa kupinga baadhi ya mahusiano yake na mwanamume yakiwemo kukataa kutumiwa kama chombo cha kukidhi ashiki za wanaume hasa kwa kuangazia mchakato yakini katika wimbo huu.Hata hivyo, haina maana kwamba wanaume katika wimbo huu hawana mamlaka kwa vile, tumeona kwa mfano kwamba, mpenzi mpya wa mwanamke wa kwanza kupitia mchakato yakini ameweza kumfumbata mwanamke huyo na hiyo ni njia ya kumdhibiti kabisa.Vile vile,kupitia kwa istiari zilizotumiwa, wanawake kwa kutojua wameendeleza mfumo wa ubabedume kwa kuonyesha kwamba miili yao ndiyo muhimu katika mahusiano yao na wanaume hasa kwa kujivunia makalio makubwa na ujuzi wa ngono.Mwisho ni kuwa,mwanamume amezidi kusawiriwa kama mwenye mamlaka makubwa akilinganishwa na mwanamke ila hilo limefichwa katika kejeli zilizo katika wimbo huu ambazo zimeonyesha kwamba mwanamke ni adui ya mwanamke mwenzake.Hili limebainika hasa mwanamke wa kwanza anapomsawiri mwenzake kama limbukeni au mjinga katika mahusiano yake na mwanamume na wa hadhi ya chini maana kama mpenzi wake ni punda basi yeye pia ni punda.

Katika sura ifuatayo, tutaelezamuhtasari wa wimbo *Utalijua Jiji* ulioimbwa naAfua Suleimani kisha kuchanganua mahusiano ya mamlaka na itikadi katika wimbo huo kwa kutumia michakato yakini, kiakili na kihusiano kabla ya kuchunguza pia lugha ya mafumbo ilivyotumika katika wimbo huo.

SURA YA NNE

MAMLAKA NA ITIKADI KATIKA WIMBO *UTALIJUA JIJULIOIMBWA NA AFUA*

SULEIMAN

4.1 Muhtasari wa wimbo *Utalijua Jiji*

Wimbo huu unahusu swala la ukewenza ambapo mke wa kwanza anasutwa na mke wa pili katika malumbano ya kujipendekeza kwa mume. Mke huyo wa pili ambaye ni mwanamke wa mjini anamsuta mwenzake ambaye yamkini ni wa kutoka mashambani kuhusu ujinga wake wa kutojua namna ya kumtunza mume. Kutojua huko kumtunza mume vizuri ndiko kulikosababisha mumewe kumkimbilia mke wa pili. Kulijua jiji kuna maana ya kufahamu mambo yanavyofanyika hasa katika ndoa yaani, namna mke anavyostahili kumshughulikia mumewe. Kwa kuwa mke wa kwanza hakujua kumtunza mume, mke huyu wa pili anamweleza sababu ya kumchukua mumewe. Anahalalisha kitendo hicho kwa kusifia uhodari wake wa mapishi, urembo, uhusiano mwema pale nyumbani na kilele chake ni ujuzi wa kumzuga mume kwa mapenzi kitandani mambo ambayo mke wa kwanza alishindwa kuyafanya vizuri.

Maswala yanayojitokeza katika wimbo huu kama vile ukewenza, mabishano, kujipendekeza kwa wanawake kwa mwanamume, mivutano ya kutafuta nafasi ya kupendwa ni muhimu katika kuelewa mamlaka na itikadi katika wimbo huu. Kwa hivyo, utoaji wa muhtasari huu ni muhimu kwa sababu unatusaidia kuelewa mamlaka na itikadi yamejitita wapi katika wimbo ili tuweze kuyafafanua kwa kutumia michakato yakini, kiakili na kihusiano pamoja na lugha ya mafumbo.

4.2 Mamlaka na itikadi katika wimbo *Utalijua Jiji*

Katika sehemu hii tunachunguza mamlaka na itikadi kwa kufafanua michakato mitatu ya uelekezi huku tukuchota mifano kutoka kwa kazi nyingine za fasihi. Pia tutafafanua lugha ya mafumbo katika wimbo huo.

4.2.1 Mchakato yakini

Mchakato yakini tulishaeleza awali kama mchakato ambao kitenzi katika kishazi kinaonyesha ufanyaji na utukiaji wa kitendo. Kunakuwa na kitendo hicho kutokana na juhudi za mmoja wa Washiriki. Mshiriki/Mtendaji hutumia nguvu zake au juhudi kutekeleza kitendo hicho kisha kuna mpokezi (Lengo) wa kile kitendo au anayeathiriwa kutokana na utokeaji wa kitendo hicho.

Mchakato yakini ni muhimu katika kueleza mahusiano ya mamlaka kwa sababu Mtendaji katika mchakato huu hutumia nguvu au juhudi zake kutekeleza kitendo kinachoathiri Lengo. Mtendaji katika mchakato huu huwa na mamlaka makubwa kwa Lengo akilinganishwa na Mtendaji katika michakato mingine. Vitendo ambavyo Mtendaji wa mchakato huu huvitenda huwa vitendo vya kuonekana kama vile kupiga, kuchukua, kujenga, kukata, kufunga, n.k. Lengo kwa upande wake katika mchakato huu hana mamlaka. Lengo na Mtendaji huwepo iwapo kitenzi elekezi ambacho kinahitaji yambwa kinatumika.

Katika wimbo *Utalijua Jiji* kuna michakato kadha yakini ambayo inaweza kuchanganuliwa ili kufafanua maswala ya mamlaka na itikadi. Ubeti wa pili una michakato miwili yakini.

*Vituko vya makusudi, si bure wewe umerogwa.
Badala ya soda baridi, ama juisi ya chungwa,
Ushamba umekuzidi andazi wanywea togwa.*

Mchakato wa kwanza ni *umerogwa* ambapo Mtendaji ambaye ana mamlaka hajabainishwa waziwazi lakini Lengo ni mwanamke wa kwanza aliyemuudhi mumewe na sasa mumewe kachukuliwa na mwanamke mwingine. Msemaji ambaye ndiye mke wa pili aliyemtwa mume wa Mtendaji anambeza kwa kusema kuwa amerogwa na ndio sababu ameshindwa kumtunza mume kwa njia inayofaa. Kwa kutumia kauli ya kutendwa katika mchakato yakini huo, Lengo basi ananyimwa mamlaka maana ametendwa na Mtendaji, mchawi au mganga ambaye ana mamlaka ya ushirikina. Hata kama si huko kurogwa na mchawi au mganga, kauli hiyo kwa namna fulani inamsawiri mke wa kwanza kama asiye faa kitu kwa vile vitendo vyake ni vya kuchekecha tu: vitendo vya kutia aibu kama vile kunywa andazi togwa. inaonyesha kwamba Mchakato mwingine katika ubeti huo ni katika kishazi *ushamba umekuzidi*. Mke wa pili anatumia maneno hayo ili kusuta hali ya “kutoendelea” au “kutojua mambo” ya mke wa kwanza anayeshindwa kumtunza mume au hata yeye mwenyewe. Kwa mfano, badala ya kunywa andazi soda baridi au sharubati ya chungwa yeye ananywea togwa jambo ambalo ni la ajabu sana. Hali hiyo ya kutomaizi mambo yafanywavyo ndiyo inayomfanya asemwe kuwa amezidiwa na ushamba na msemaji anamsawiri kama mtu mpumbavu au mshenzi asiye fahamu namna mambo yanavyofanywa hasa majukumu ya mwanamke katika ndoa kama inavyojitokeza katika wimbo mzima. Malumbano ya namna hii kati ya wanawake katika muktadha wa ukewenza yanaongozwa na itikadi ya ubabedume ambapo mwanamume aliye na mamlaka ya juu kabisa katika jamii anakuwa kama mfalme au rasilmali muhimu inayofanya wanawake wadharauliane, kutusiana na kusutana kwa lengo la kumpata huyo mwanamume. Wanawake vilevile wanakuwa ni adui wao wenyewe kwa vile kusutana, wivu na malumbano miongoni mwao kama tunavyoona katika aya hiyo yanasababisha utengano miongoni mwao.

Katika ubeti wa nne pia kuna michakato yakini mingine.

Pokea chako kibomu, shoga nakutumia,
Hata ukinilaumu, wako nishamchukua.
Penzi ulimdhulumu, visaukamfanyia
Chachanduvi tamutamu, bwana hukumpatia.

Mchakato wa kwanza upo katika kishazipokea chako kibomu. Mtendaji katika wimbo huu ni mwanamke aliyemtwa mume wa mwenzake kwa madai kuwa hajui kumtunza. Kwa kusema pokea, Mtendaji huyu ana mamlaka kuliko huyo mwenzake anayepokea adhabu ya kumkosa mume kwa sababu huyu Mtendaji amemchukua. Mke wa kwanza ndiye Lengo katika mchakato huu maana amelazimishwa au amedhulumiwa na mwenzake kwa kufanyiwa kitendo hiki cha kupewa adhabu. Mchakato huo unakamilishwa kwa mchakato mwingine, shoga nakutumia ambapo Mtendaji na Lengo bado ni wale wale kama ilivyo hapo juu. Mtendaji, mwanamke aliyemtwa mume wa mwenzake ndiye anayemtumia mwenzake (Lengo) adhabu na hivyo bado anadhihirisha mamlaka makubwa maana ndiye mtendaji wa kitendo ilhali mwenzake ni mpokezi tu asiyekuwa na hiari yoyote. Kuna mchakato yakini mwingine katika ubeti huu katika mshororo wa pili, kipande cha pili: Wako nishamchukua. Katika kishazi hiki, Mtendaji bado ni mke wa pili aliyemtwa mume wa mke wa kwanza. Lengo ni mume wao ambaye amesawiriwa kama kitu ambacho kinaweza kuchukuliwa. Mwanamke akiwa Mtendaji anaonyesha kwamba ana mamlaka kwa kiwango fulani, kwamba anaweza kutumia maarifa au nguvu zake za mwili kuweza kumchukua mwanamume kutoka kwa mwanamke mwenzake. Japo hali ni hii, Zaja, O.J. (2008) anasema kwamba mwanamke anafanya juhudi za kupata mwanamume kwa kutumia mbinu zote ili anapokuwa naye aweze kufaidika kutokana na kuwa naye maana kuwa na mwanamume katika mfumo huu wa ubabedume ni sawa na kuwa na uwezo wa kupata faida za kiuchumi na nyinginezo ambazo yeye ndiye mmiliki. Kwa hivyo ingawa katika huu mchakato yakini

mwanamke anaonyesha kuwa anaweza kumchukua mwanamume na hivyo ana mamlaka kuliko mwanamume katika muktadha huo, mwishowe kinachotokea ni kwamba mwanamke huyo anafanya hivyo ili aweze kumpata mwanamume huyo, amdhibiti na kwa kufanya hivyo, aweze kufaidika kutokana na mahusiano yake na mwanamume maana mwanamume amepewa uwezo mwingi wa kiuchumi, kisiasa na kijamii ambao mwanamke anaweza kuufikia tu kupitia mahusiano yake naye. Jamii ya Waswahili au Waafrika kwa ujumla wamefanywa kuamini kuwa wanaume kuwa wanawake hawawezi chochote isipokuwa kwa msaada wa wanaume. Mwanamke mmoja katika hadithi fupi *Uteuzi wa Moyoni* ya Timammy, R. (2004) anakubali kuwa mwanamke hawezi chochote anaposema: “*Na watakaompa yeye wamekosa kazi! Hebu yeye aweze kufanyani? Wanaume hawakuweza kufanya lolote ataweza yeye?*” Kauli hii ni ya kumsuta Zena, mwanamke anayegombea kiti cha ubunge, eneo ambalo wanawake wamekubali kuwa ni la wanaume na hivyo anasutwa na wanawake wenzake kuwa hawezi kupigiwa kura kwa sababu yeye ni mwanamke na kuwa mambo anayotaka kufanya wanaume wameshindwa. Kinachozuka hapa ni kuwa wanawake wameamini kuwa wanaume ndio wenye uwezo katika maswala ya kisiasa hata kama hawawezi.

Mshororo wa tatu una michaklato miwili yakini lakini yote ina maana moja. Kwanza ni katika kishazi *Penzi ulimdhulumu* ambapo mwanamke aliyekimbiwa na mumewe akaenda kwa mke mwingine ndiye Mtendaji ilhali mume wake huyo ndiye Lengo. Hali ni hiyo katika mchakato wa pili ulio katika kipande cha pili cha mshororo: Visa *ukamfanyia*. Katika michakato hiyo yote, mwanamume ametendewa mambo mabaya na mwanamke aliye na mamlaka katika miktadha hiyo. Kinachotokea katika michakato hiyo kama mshororo wa mwisho katika ubeti huu ni kwamba mwanamke anastahili kumtendea mwanamume mambo yanayopasa kumfurahisha na

ngono ndio muhimu kabisa: *Chachanduvi tamutamu bwana hukumpatia*. Kama Zaja, O.J. (2008) anavyosema, wanawake huwafanyia wanaume mambo kama kuwapikia, kuwapa ngono na mambo mengine ya kuwafurahisha ili wafaidike kiuchumi. Hali hii basi inamtia mwanamke katika utumwa wa aina fulani maana anakuwa mtu wa kumfurahisha mume tu kupitia kwa matendo yake. Anakuwa kile ambacho Matei, A.M (2014) anasema ni usawiri wa mwanamke kisarufi na kiitikadi kama anayetegemea matendo ya mwanamume na hivyo nafasi yake katika mahusiano yake na mwanamume inakuwa iliyopembeza. Hali hii japo ni swala la utamaduni inaishia kuonekana kama utumwa wa aina yake. Utumwa huu kama Althusser, L (1971:60) anavyosema huwa ni njia ya kudumisha itikadi fulani na kwa muktadha huu ni itikadi ya ubabedume. Utumwa pia ni njia ya kudumisha mahusiano ya mamlaka kati ya mtawala na mtawaliwa ili mtawaliwa azidi kunyanyaswa au kutawaliwa (Foucault, 1977).

Ubeti wa tano wa wimbo huu pia umesheheni michakato yakini.

Bwana kapata wazimu, kashindwa kuvumilia.

Kwangu akatia timu, tiba nikampatia.

Nikampa vitu adimu, kwako hajajionea

Amri akasalimu, magoti kunipigia.

Huku ajilaumu, kwako kapotea njia.

Mchakato yakini wa kwanza katika ubeti huu ni katika kishazi, tiba nikampatia. Katika mchakato huu, mke wa pili aliyetwaa mume wa mke wa kwanza ndiye Mtendaji na mume huyo aliyemtwa ndiye Lengo. Mahusiano katika mchakato huu bado ni kama yale ya mchakato yakini wa mwisho katika ubeti uliotangulia ambapo mwanamke japo anasawiriwa kama mwenye mamlaka ya kumpa mwanamume *tiba* au *vitu adimu* kama anavyoviita katika mshororo wa tatu yaani mapenzi au ngono, tendo kama hili linamwonyesha mwanamke kama mtu anayemtendea mwanamume mambo kama haya ili aweze kumvutia na kumdumisha katika uhusiano

wake.Sababu ya kufanya mambo kama haya ya kumdhalilisha ni kutaka kupata faida za kiuchumi ambazo mfumo wa ubabedume umefanya mwanamume kuwa nazo.Pia katika ubeti huo kuna michakato miwili yakini katika mshororo wa nne, amri akasalimu,magoti kunipigia.Katika hii michakato yakini, kuna vitenzi virai *amri akasalimuna magoti kunipigia* ambavyo vina vitenzi *akasalimu* na kunipigia na vijalizo *amrina magoti* mtawalia.Mtendaji katika michakato hii ni mume ilhali mke wa pili ndiye Lengo.Japo mume ni Mtendaji ,vitendo vyake katika michakato hiivinaonyesha kwamba anamtii mkewe aliye Lengo na hivyo ni kama anamwabudu.Hali hii inaonyesha kwamba Lengo ana mamlaka kwa Mtendaji katika muktadha huu kiasi kwamba anaweza kumfanya kumpigia magoti ambayo ni ishara ya unyenyekevu.Hata hivyo,huu waweza vilevile kuwa mkakati fiche wa mume kumhadaa mke huyu kudhani kwamba yeye ameheshimiwa au kupewa hadhi muhimu katika mahusiano yake na mume wake ili aendelee kumfurahisha pale nyumbani.Hata hivyo jambo hilo linakuwa fiche sana kwa vile mke wa pili hawezi kulifasiri hivyo na badala yake anafurahi kwamba anaabudiwa .Asemavyo Fairclough, N. (1993:133), mahusiano kati ya diskosi,itikadi na mamlaka yaweza kuwa fiche kwa wanaohusika.Ufiche huo hutokana na maswala kama hayo kuonekana kama jambo “asilia” na “kubalifu” bila kuhusishwa na itikadi yoyote au kuonyesha kundi fulani linadhibiti lingine (Van Dijk,T. 1993:254).

Katika mshororo wa mwisho wa kibwagizo cha wimbo huu, kuna mchakato yakini.*Kwake hupati nafasi mimi ndiye yake pumzi*.Katika mchakato huu, Mtendaji ni mwanamke yule mshamba ambaye amenyang’anywa mume ilhali mume huyu ndiye Lengo katika mchakato huu.Kwa kutumia kitenzi hupati katika hali ya kukanusha, msemaji ambaye ndiye alimpokonya mke wa kwanza mume anadhihirisha kwamba ana hakika na jambo analosema na kwa hivyo ana

mamlaka kuliko huyo mke mwenzake. Kama tulivyosema hapo juu, mwanamke anapokuwa na mume ambaye ni nguzo ya uchumi kwa mwanamke yeyote, ni njia fulani ya mwanamke kupata haki yake. Kwa hivyo anapokuwa amepata huyo mwanamume, anatumia kila mbinu kujaribu kumthibiti mume wake ili awe naye pekee yake maana atapata faida zitokanazo na kuwa naye. Anapomwambia mwenzake kwamba hapati nafasi kwa mume yule, ni njia ya kumtenga na mume huyo. Njia moja ya mtu kudhibitisha kwamba mtu ana mamlaka kwa mwenzake au kundi fulani kwa lingine ni kulitenga katika kupata kitu au huduma fulani (Van Dijk, 1993:260). Hali hii ya kutenga watu, kwa mfano wanaume kutenga wanawake katika uandishi wa kazi za fasihi kulingana na Miller, C.L. (1990:250) kule Afrika Magharibi hadi miaka ya sabini kulifanya wanaume kuendelea kudhibiti wanawake kimawazo, kiuchumi na kwa kila njia. Basi mwanamke huyo anapokuwa amepokonywa mume na mke mwenzake na kuambiwa kuwa hatapata nafasi kwake, ni sawa na kumfungia nje ya njia ya kupata faida za kiuchumi zinazofungamana na kuwa na mume kwa sababu mahusiano yake na mume huyo yamekatizwa.

Ubeti wa saba vilevile una mchakato yakini katika mshororo wa mwisho... *bwana imemwisha hamu, kakutimua nyumbani*. Mtendaji hapa ni mume ambaye ameishia kumpenda mke wa pili na kumtenga yule wa kwanza. Mke huyo aliyetimuliwa ni Lengo. Mchakato huu unaonyesha kwamba mume ana mamlaka kwa vile ameweza kutumia mamlaka au uwezo wake kama ni wa kimwili au mwingine ule kumtimua mkewenyumbani. Althusser, L. (1971) akinukuu maneno ya Marx, K. (1867) akizungumza kuhusu mfumo wa ubepari anasema kuwa kila itikadi inapoanzishwa lazima iwe na nguvu za kuizalisha pamoja na kuwa na mahusiano ya kuendeleza itikadi hiyo. Kwa msingi huu, mume huyu ametimua mke wa kwanza nyumbani kwa sababu ameshindwa kudumisha yale mahusiano mazuri ya kumstarehesha mumewe na kulazimisha

mume huyo kutafuta mke wa pili anayeweza kumfanyia hilo. Itiakadi ya ubabedume ndiyo inayomwongoza mwanamume huyu kukatiza uhusiano na mke wa kwanza na kuanzisha uhusiano mpya na mke wa pili ili aendelee kufurahishwa na kustareheshwa.

Katika ubeti wa nane kuna mchakato mwingine yakini katika mshororo wa tatu. *Mimi naletewa ndani, wewe watanga na njia*. Katika mchakato huu, mume ndiye Mtendaji ambaye anadhihirisha uwezo wake wa kiuchumi kwa kumletea mahitaji mke wa pili aliye Lengo. Mke huyu wa pili anakuwa ni mpokezi wa matendo ya kiuchumi ya mwanamume. Kama tulivyosema hapo awali, mke humfanyia mume mambo kama vile kumpika vyakula vizuri, kumpa mapenzi mazuri na kumliwaza mume kwa njia nzuri kadri ya uwezo wake kwa kutegemea kwamba juhudi kama hizo zitamfanya apate faida za kiuchumi kama zinavyoelezwa katika sehemu hii ya wimbo. Utegemezi wa mke kiuchumi kwa mumewe unatokana na swala la utamaduni katika jamii hii ya Waswahili ambapo wanaume ndio wanaotafuta riziki huku wanawake wakikaa nyumbani kufanya kazi za nyumbani (Traore, 2004). Hali hii ya utamaduni wakati mwingine imefanya watu wakafasiri tenzi za Waswahili kama vile *Utenzi wa Mwanakupona* uliotungwa na Mwanakupona (1858) kwamba ni utenzi unaomdunisha mwanamke bila ufahamu kwamba hakuna swala la kudunishwa ila ni utadamuduni tu. Hata hivyo, leo hii kutokana na mabadiliko katika jamii ambapo wanawake sawa na wanaume wanaenda shuleni na wanaajiriwa baada ya kufuzu katika masomo yao, utegemezi wa wanawake kwa wanaume umeenza kupungua maanake wanawake pia wanaenda kazini na kukimu mahitaji ya jamii. Mabadiliko kama haya yanafanya mahusiano ya mamlaka kati ya mwanamke na mwanamume kubadilika. Katika wimbo *Zilipendwa* tuliochanganyua katika sura ya tatu tumeona mwanamke akidhihirisha mamlaka kwa kiwango fulani kiasi kwamba anakinza tabia ya ubabedume ya kufanywa chombo cha

mwanamume. Hili laweza kuwa limetokana na kupevuka kimawazo kutokana na elimu ya sasa na uwezo wa mwanamke kijikimu kiuchimi ikizingatiwa kwamba wimbo huo umetungwa miaka ya elfu mbili ambapo wanawake wamekuwa wakielimishwa kuhusu haki zao.

Ubeti wa mwisho wa wimbo huu una michakato kadha yakini. Katika mshororo wa kwanza kuna miwili: *Wako nishamchukua, kwako harudi tena*. Katika mchakato wa kwanza katika kitenzi *nishamchukua*, mwanamke aliyemtwa mume wa mwenzake ndiye Mtendaji ilhali mke huyo mwenzake ndiye Lengo maana ametendewa kitendo. Kwa kusema, *kwako harudi tena*, mwanamke huyo anaonyesha mamlaka kwa njia mbili: Kwanza dhidi ya mke mwenzake kwamba anaweza kuchukua mume wake na asifanye chochote na pili kwa mwanamume kwamba anaweza kuchukuliwa na mwanamke kutoka kwa mwanamke mwingine na mwanamume huyo akawa amedhibitiwa na mwanamke asiweze kuondoka akaenda kwingine. Ingawa hali yaonekana kwamba ni, kuwa mwanamke amedhibiti mume katika muktadha kama huo, udhibiti huo huwa ni wa muda tu maana mwanamke huyo akishindwa kumfurahisha mumewe basi mumewe anaweza kuondoka akaenda kwa mke mwingine bila mwanamke huyo kufanya lolote. Ili mwanamke huyo kuzidi kumdhibiti mumewe asiondoke, lazima afanye mambo anayoyasema katika mishororo kadha inayofuata:

*Amenipa nafasi, nimwonyeshe ujuzi
Nami sifanyi ajizi, mpenzi ninamwenzi
Nampikia maandazi na chai ya tangawizi
Wali wa nazi kwa ndizi “mavitus” kama kazi
Kisha nampa dozi, impayo usingizi.*

Katika ubeti huo, mwanamke kupitia kwa mambo anayomfanyia mumewe ambayo baadhi kama tuliyopigia mistari ni michakato yakini anakuwa Mtendaji huku mumewe akiwa Lengo. Mwanamke anasawiriwa kama mtu ambaye majukumu yake kwa mumewe ni kumpikia chakula

akala akashiba pamoja na kumridhisha kwa ngono na yote haya yanakuwa kama mtego wa kumpata na kumdhibiti mume kwa lengo la kupata faida za kiuchumi. Mahusiano ya mke na mume yamejengwa kwa msingi huo kwamba mume anamfaidisha mke kiuchumi lakini anafanya hivyo iwapo mke naye ni hodari wa kupika jikoni na kitandani. Swala hili linajitokeza sana katika nyimbo nyingi za taarab. Wimbo *VIP* wa Mzee Yusuf katika *Jahazi Modern Taarab* unadhihirisha hilo kwa kina kwa kuonyesha nafasi na majukumu ya mwanamke na mwanamume. Mwanamume anapotoka kazini anampata mkewe nyumbani, anamvua koti na kumpigia magoti kisha maneno ya wimbo huo yanamsawiri mwanamke kama anayestahili kuwa mpishi mzuri wa jikoni na kitandani na anayebaki nyumbani huku mumewe akienda kutafuta riziki. Japo ni utamaduni wa jamii, mambo kama hayo yanamweka mwanamume juu na mwanamke chini katika mahusiano ya mamlaka na ukosefu wa usawa huo unatokana na itikadi ya ubabedume.

4.2.2 Mchakato wa kiakili

Tushaona kwamba huu ni mchakato unaohusu hisia na hivyo ni wa kisaikolojia. Mchakato huu ni muhimu maana unahusu utambuzi wa wasemaji katika lugha kuhusu ulimwengu wao wa ndani na nje, unatumika kujenga utambulisho, imani, misimamo na itikadi (Halliday, M.A.K. 2014). Katika ubeti wa tatu kuna huo mchakato wa kiakili katika mshororo wa kwanza: *Mwenzangu huna, ujuzi, mpenz iumemuudhi*. Hapa, Mhisi ni mke wa kwanza aliyeponzwa mume na mume huyo ndiye Finomena. Mwanamke hapa japo hana mamlaka sana kama ilivyo katika mchakato yakini, amepewa uwezo wa kumfanya mwanamume kuudhika kutokana na kutojua namna ya kumtunza. Mchakato mwingine wa kiakili upo katika ubeti wa tano katika mshororo wa kwanza: *Bwana kapata wazimu, kashindwa kuvumilia*. Japo katika kishazi hicho ambacho ni kitenzi

kirai,mwanamume ndiye Mhisi na *wazimu* ndio Finomena, mwanamke amesawiriwa kama mtu mwenye ushawishi na vivutio na hivyo ana uwezo na mamlaka ya kumbabaisha mwanamume kisaikolojia kutokana na vivutio vyake vya mapenzi,urembo na uhodari wa mapishi.Kwa njia nyingine,mwanamke ana uwezo wa kumfanya mwanamume amfuata na kuacha mke wake kutokana na vivutio vyake na hivyo anadhihirisha mamlaka aliyonayo kwa mwanamume.Ingawa mwanamke si mtendaji wa moja kwa moja katika mchakato huo, asemavyo Matei, A.M. (2014), anaponukuu maneno: *Mambo yao ni ya kushangaza* kutoka *Unaitwa Nani?* (Wamitila, 2008) ambapo daktari Zomo anasimulia kisa cha mwanamke wa Uchina alivyomchoma mumewe kwa shuka kitandani kwa kwenda kitandani bila kupangusa miguu yake.Usawiri huu wa wanawake ni wa kuonyesha mambo wafanyayo kuwa ya ajabu kama vile kuwazuga waume katika wimbo huu.Usawiri huu mbaya wa mwanamke kama anayeweza kumzuga, kumdhuru au kumletea mwanamume madhara mengine upo katika riwaya kama *Safari ya Lamu* ya Habwe, J.H. (2011; 111) ambapo kumesemwa: *Mke ni kisu cha makali* na katika riwaya *Barua Ndefu Kama Hii* ya Mariama Ba (1976:36) ambapo mamake Maudu Ba anasema: *Shule inawageza mabinti zetu kuwa mashetani wanaopotosha wanaume*.Licha ya usawiri huo mbaya wa wanawake,muhimu ni kwamba wanawake wanakuwa na mamlaka fulani kwa wanaume katika hali kama ya wimbo huu.

Ubeti wa sita pia una mchakato wa kiakili katika mshororo wa kwanza:

Kapenda yangu nidhamu na utulivu nyumbani
Pamoja na ukarimu, kwa ndugu na majirani,
Ucheshi na tabasamu, kanijalia Maanani
Nimepewa lugha tamu, nyoka hutoka pangoni.

Mhisi hapa ni mume na Finomena ni mke wa pili aliyemtwa mume huyo kutoka kwa mke mwenzake. Japo mwanamume hapa ndiye anayependa kwa kuvutiwa na matendo ya mwanamke huyo, mahusiano ya mamlaka yanaonyesha kwamba mwanamke aliye Finomena ndiye mwenye mamlaka zaidi kwa vile matendo yake ndiyo yaliyoweza kumfanya mumewe kumpenda. Matendo hayo kama vile kuwa na nidhamu, kutulia nyumbani, ukarimu kwa ndugu na jirani za mumewe, ucheshi na tabasamu yamesababisha athari ya hisia za kupenda kutoka kwa mumewe. Mchakato huu wa kiakili unazua swala lingine la kiitikadi kwamba mwanamke kuweza kudumisha mahusiano yake na mwanamume sharti aweze kumfanyia matendo yakini au ya kimwili na yale ya kisaikolojia yanayomfurahisha.

Anwani ya wimbo pia ni mchakato wa kiakili. Mwimbaji ambaye ni mwanamke aliyempokonya mwenzake mume anapomwambia mwenzake kuwa *utalijua jiji*, kejeli hii inanuia kumsawiri na kumtambulisha mwenzake kama mtu mjinga asiyefahamu namna mwanamke anavyopasa kumtunza mume. Kitenzi cha mchakato wa kiakili ni *utalijua*. Mke wa kwanza ndiye Mhisi huku Finomena ikiwa *jiji*. Mhisi anatambulishwa na mke wa pili kama limbukeni katika ulimwengu wa uhusiano kati ya mke na mume. Si ajabu kwamba katika ubeti wa mwisho katika mshororo wa nane anaambiwe : *Mwenzangu huna ujuzi, rudi tena kajifunze*. Kwa kuambiwa arudi tena ajifunze namna ya kumtunza mume ni kana kwamba itikadi ya ubabedume imewafanya wanawake waone hiyo kama kaida na inabdi wajizatiti kuelimishwa namna ya kumtunza mume. Hili linadhahirisha ni kwa nini makungwi wamekuwepo katika jamii ya Waswahili kwa lengo la kuwafunza wasichana wanapobaleghe jinsi ya kumtunza mume kwa kudumisha usafi wa mwili, kupika vyakula vizuri jikoni, kunyenyekea mbele ya mume na kujua namna ya kumridhisha kitandani miongoni mwa mafunzo mengine. Asasi kama hii inakuwa shule ya kuwafunza wanawake

kuwahudumia wanaume na hivyo ni mahali pa kuendeleza mfumo wa ubabedume. Tushaona kwamba mambo haya anapofanya mwanamke,hulenga kumdhibiti mumewe na hivyo licha ya mwanamume kuwa na mamlaka yatokanayo na uwezo wa uchumi umvutiao mwanamke , vilevile mwanamke anadhihirisha uwezo wake wa mamlaka kupitia kwa vitendo hivyo vyenye vivutio.

4.2.3 Mchakato wa kihusiano

Mchakato huu tulishauzeleza katika sura ya kwanza na ya tatu na hakuna haja ya kueleza katika sehemu hii.Muhimu ni kwamba kuna wahusika wawili ambao ni Mbebaji anayekuwa mtu au kitu chenye sifa fulani kisha kuna Sifa ambayo huwa ni sifa hiyo inayohusishwa na Mbebaji.Katika ubeti wa kwanza, mshororo wa kwanza kuna mchakato wa kihusiano: *Kazi yako ufisadi,jeuri,gebe na dobwa*.Katika mshororo huo,kitenzi hakipo maana kimeachwa nje lakini ni kitenzi cha kuwa, *ni*, kinachostahili kuwa kati ya neno *yako* na *ufisadi*. Mwanamke aliyepokonywa mume ndiye Mbebaji na mambo hayo anayoambiwa kuwa ndiyo kazi yake yaani ufisadi, gebe na dobwa ndiyo Sifa. Halliday,M.A.K. (2014:210) , anasema kwamba kazi ya mchakato huu ni kuonyesha sifa za wahusika na namna wanavyotambulishwa.Kwa kutilia hilo maanani,tunaona kwamba mke wa kwanza anamwona mwenzake kuwa hafai kwa lolote katika uhusiano wake na mumewe kwa vile anachojua ni kufanya mambo maovu kama ufisadi na ujeuri kwa mwanamume ,mambo ambayo mwanamume hastahili kufanyiwa.Ubaya huo wa mwanamke huyo unaotokana na kuwa mtu asiye na maadili au tabia nzuri unadhihirishwa zaidi katika ubeti wa tatu ambako kuna mchakato wa kihusiano mwingine: *Mwenzangu huna ujuzi,mpenzi umemuudhi*. Kitenzi *huna*, ndicho kilicho na mchakato huo wa kihusiano na kinaonyesha kwamba mwanamke huyo aliyenyang'anywa mume akiwa Mbebaji hana ujuzi wa kumtunza

mume.Kwa kutumia kitenzi hicho katika hali kanushi, mke wa pili anataka mke wa kwanza atambuliwe kama asiye na ujuzi wowote wa kumtunza mumewe na hilo linatumika kuhalalisha hatua yake ya kumchukua mumewe maana anaona kuwa mume huyo amekuwa akiteswa.

Kibwagizo cha wimbo huu katika mshororo wa mwisho kuna mchakato mwingine wa kihusiano: *Kwake hupati nafasi, mimi ndiye yake pumzi*. Mke wa pili aliyechukua mume wa mwenzake ndiye Mbebaji na Sifa ni *yake pumzi*.Ikizingatiwa kwamba viwakilishi rejeshi *kwake* na *yake* vinamrejelea mume wake ambaye amemtoa kwa mke wa kwanza kwa kutumia vishawishi, mwanamke huyu anaonyesha namna mwanamke anapopata mume hasa kutoka kwa mke mwingine anavyojibidiisha kumtunza kwa kufanya mambo yanayomfurahisha ili amdhibiti kabisa.Kwa kudai kwamba yeye ndiye pumzi ya mumewe, ana maana kuwa kuwepo kwa mumewe kunamtegemea yeye na wala sio mtu au kitu kingine yaani mume huyo anaishi kwa sababu yake. Mke wa pili ambaye ni Mbebaji katika mchakato huu akiwa pumzi ya mumewe basi ana nafasi muhimu katika maisha ya mumewe na hii inakuwa ithibati ya mke huyo kuwa na kiwango fulani cha mamlaka kwa mumewe.Isitoshe, kupitia kwa mchakato yakini katika ukwapi wa mshororo huo ambapo mwanamke huyo anamwambia mwenzake kuwa hawezi kupata nafasi kwa mume wake kunadhihirika kwamba mke wa pili anayempokonya mwenzake mume katika jamii hii huwa na mamlaka na uwezo maana anaweza kumkanya mwenzake ambaye ashampoteza mume kuwa ashampoteza mume wake na hivyo anastahili kuondoka arudi kwao. Mke wa pili hujaribu hata kumshawishi mumewe amwache mke wa kwanza kwa kudai kuwa mke huyo wa kwanza hajui kumtunza.Swala hili linaonyesha kwamba mwanamke hata katika mahusiano ya ukewenza hasa yule wa pili ana mamlaka makubwa kwa vile anaweza kumchukua mume kutoka kwa mke mwenzake kwa kutumia vishawishi vyake kisha akamdhibiti kabisa

kando na kumsuta mke wa kwanza kujiondoa katika ushindanni ndoani. Tunaliona hili pia katika nyimbo zingine kama *Paka Mapepe* ambapo mke wa pilianamtahadharisha mumewe kumwepuka mke wa kwanza kwa sababu anapenda wanaume wenye pesa badala ya kuthamini ndoa na mapenzi halisi kama ilivyo katika ubeti wa pili:

*Paka mapepe usimwandame, mapepe huyo.
Usiache akuchunge, mapepe huyo.
Huyo hamjui mume mapepe huyo.
Mwenye fedha kwake dume mapepe huyo*

Hili vilevile linajitokeza katikawimbo *Tutabanana Hapa Hapa* ambapo mke wa pili anamwambia mke wa kwanza kuwa yuko pale naye katika ukewenza na akizubaa atafurushwa na kutupwa kutoka katika ile ndoa kama ilivyo katika ubeti wa tatu mishororo mitatu ya mwisho:

*Niko nawe sikuachi,
Na ukizubaa hapa nakutoa.
Na ukilegea hapa nitakutupa.*

Ubeti wa mwisho wa wimbo *Utalijua Jijiuna* mchakato wa kihusiano ambao ni kama muhtasari au hitimisho la mahusiano ya mwanamke na mwanamume kimamlaka yalivyo katika jamii hii. Msemaji ambaye ni mke wa pili aliyepokonya mwenzake mume anasema katika mshororo wa tisa wa ubeti huo: *Bibi acha upuuzi, kuishi na mume kazi*. Katika utao wa mshororo huo, kitenzi cha kuwa, ni, hakipo japo kinastahili kuwepo kati ya maneno *mume* na *kazina* ndicho kitenzi kilicho na mchakato wa kihusiano. Mwanamke huyu kwa kujua au kutojua anakubali kuwa chini ya mfumo wa ubabedume kwa kuridhia kwamba mwanamke kuishi na mume ni kazi. Kwa kusema kuwa kuishi na mume ni kazi ana maana kwamba mwanamke anastahili kumfanyia mumewe shughuli za pale nyumbani kama kupika, kuosha vyombo, kusafisha nyumba, kumfurahisha na kumpa mapenzi ya kumridhisha kitandani mambo ambayo si rahisi kamwe. Hili

linadhihirishwa na mishororo mingine inayotangulia huo tuliochambua kufafanua ni kwa nini kuishi na mume ni kazi:

*Wako nishamchukua, kwako harudi tena
Katamka waziwazi, kuwa hakutaki tena
Amenipa nafasi, nimwonyeshe ujuzi
Nami sifanyi ajizi, mpenzi ninamuenzi
Nampikia maandazi, na chai ya tangawizi
Wali wa nazi kwa ndizi, mavitus kama kazi
Kisha natoa dozi, impayo usingizi*

Mke huyu wa pili anafanya mambo haya yote ili kumdhibiti mumewe na hivyo anakuwa na mamlaka kwake katika muktadha huo. Japo kazi yake ya kumdhibiti mume ni ngumu kama ilivyo katika huo mchakato wa kihusiano,, anafaulu kuifanya vizuri lakini haifanyi hivyo bila kujua anacholenga. Anamfanyia mwanamume mambo hayo akijua akilini mwake kwamba ni mkakati wa kuweza kupata fursa ya faida za uchumi ambazo ubabedume umempa mwanamume. Lau hali haingekuwa hivyo, hangejisumbua kulumbana na mke wa kwanza kwa sababu ya mume. Ingawa pia haya yote anayomfanyia mumewe yanaonekana kama mkakati wa mtu “anayejitesa” ili kumfurahisha mume, hatima ya shughuli nzima inaonyesha mgeuko wa mamlaka kwa vile mke huyo anaweza kumfanya mumewe alale na hali ikiwa hivyo basi yeye anakuwa na uwezo wa kumfanyia lolote.

4.2.4 Lugha ya Mafumbo katika wimbo *Utalijua Jiji*

Lugha ya mafumbo hutumika sana katika nyimbo za taarab na lengo lake japo huonekana kama ni mbinu ya tasfida, uchunguzi wa kina wa matumizi hayo ya lugha ya kimaumbo unadhihirisha kuwa ni mbinu muhimu ya kuendeleza itikadi maana asemavyo Fairclough, N. (1989:93), maneno yanabeba itikadi na hivyo maana za kamusi huenda zisisaidie kuelewa kinachosemwa katika diskosi.

Fumbo la kwanza katika wimbo huu ni anwani *utalijua jiji*. Maneno hayo yamekuja kuwa msemo wenye maana yakulazimika kujifunza mambo kwa vile wewe ni mjinga au usiyefahamu yakupasayo. Kwa hivyo, mke wa pili anapomwambia mke wa kwanza kuwa atalijua jiji, anamsuta kuwa yeye ni mjinga na asiyefahamu namna mambo yanavyofanywa jijini hasa mambo ambayo mke anayostahili kumfanyia mumewe. Kama ilivyo katika wimbo huu, mke asiyejua kumtunza na kumvutia mume kwa mapishi, usafi na mapenzi yaliyokolea hana bahati jijini na inabidi aende ajifunze tena namna mke anayoishi na mume kwa vile atapokonywa mume na wanawake wanaojua kumtunza na kumstarehesha ipasavyo. Msemo kama huu ni kejeli kwa mke wa kwanza inayolenga kumdunisha na kumdhalilisha. Sababu ya haya yote ni haja ya mke wa pili kutaka kujipendekeza kwa mume ili pia afaidike kama tulivyokwisha kueleza maana mke hamstareheshi na kumtunza mume bila kuwa na lengo maalum la kuafiki. Msemo huu ushakuwa maarufu sana katika nyimbo za taarab na mazungumzo ya kawaida katika jamii za Waswahili na leo hii umeanza kubadilika na kuwa “utajiju”.

Katika ubeti wa kwanza kumetumika tashbihi ambapo mwanamke aliyepokonywa mume ukali wake umelinganishwa na embe bwabwa: Ukali kama *embe bwabwa*. *Embe bwabwa* likiwa ni embe lililoanza kuoza na hivyo kuweza kutoliwa, ulinganishaji huu wa mwanamke na embe hilo unalenga kumdunisha kwa sababu yeye tabia zake kama vile ukali na ujeuri zimemfanya awe mtu wa kuepukwa na mumewe. Katika ubeti wa nne pia kuna matumizi ya maneno : *chachanduvi tamutamu*. Maneno haya ni sawa na ”*mavitus*” na *dozi* yalilotumiwa katika mshororo wa sita na saba wa ubeti wa mwisho mtawalia. Japo maneno haya yametumika kama maneno ya heshima kwa maana ya ngono, yamebeba itikadi ya ubabedume na kuonyesha mahusiano ya mamlaka yaliyopo kati ya mke na mume. Kinachodhihirika ni kwamba mahusiano kati ya mke na mume

yataidumu tu iwapo mke atatumia ngono na sio kwa njia yoyote tu basi kwa njia inayomridhisha mume. Ngono nzuri kutoka kwa mke ni chambo kinachomvutia mume na kabla ya hilo kama tulivyoona katika wimbo *Zilipendwa*, mume atavutiwa mwanzo na mwili mzuri wa mke, hususan makalio.

4.2.5 Hitimisho

Wimbo *Utaliyua Jiji* kama ulivyoimbwa na Afua Suleimani unahusu malumbano ya ukewenza kati ya mke wa kwanza na mke wa pili. Tumeona kwamba mke wa pili anamsuta mwenzake kwa kusema yeye hajui kumstarehesha mume na hilo limemfanya mumewe kumwacha na kumwendea huyu wa pili. Malumbano hayo yamezua aina mbalimbali za mahusiano kati ya mke na mke mwenzake, kati ya mke wa pili na mumewe na kati ya mke wa kwanza na mumewe vilevile. Kupitia kwa malumbano, kusutana, mabishano na kujipendekeza kwa wake hawa kwa mwanamume, tumeona kwamba maswala ya mamlaka na itikadi yanajitokeza na yanaweza kufafanuliwa kupitia michakato yakini, kiakili na kihusiano pamoja na kuchunguza lugha ya mafumbo ilivyotumika.

Kwa kupitia mchakato yakini kwa mfano, tumeweza kubaini kwamba mke wa pili akiwa Mtendaji anadhihirisha mamlaka kwa mke wa kwanza anayechukua nafasi ya Lengo. Tazama mfano ufuatao kutoka ubeti wa tatu wa wimbo huo.

Pokea chako kibomu, shoganakutumia,
Hata ukinilaumu, wakonishamchukua,

Tumeona kuwa mke wa pili aliye Mtendaji atatumia lugha inayoonyesha mamlaka yaliyozidi ya Lengo. Katika mfano huu, Mtendaji anamwelekezea Lengo maneno ya kumkera kwa kumwambia

alivyomchukua mumewe na hiyo ni adhabu anayostahili. Kwa hivyo, Lengo hapa anakuwa ni mwathiriwa wa vitendo yakini vya Mtendaji na hivyo hana mamlaka akilinganishwa na Mtendaji. Ugomvi na malumbano haya yanayoanzishwa na Mtendaji kuonyesha mamlaka yake ya kumpokonya Lengo mume yanatokana na swala zima la ubabedume. Lau hakungekuwa na faida za kiuchumi zitokanazo na uhusiano kati ya mke na mume, Mtendaji hangejisumbua kulumbana na Lengo kama tulivyokwisha kueleza katika uchanganuzi wetu. Kupitia kwa mchakato wa kiakili pia, tumeona kuwa mke wa pili anaonyesha madharau na kejeli kwa mke wa kwanza kwa kumwambia kauli “utalijua jiji”. Japo mke wa kwanza ndiye Mhisi katika mchakato huu wa kiakili ambao kitenzi chake ni *utalijua*, mke wa pili anayemwambia maneno hayo ndiye mwenye mamlaka katika muktadha huu. Hii inatokana na ukweli kuwa mke huyo wa pili ndiye anayemwamuru mwenzake aepuke ujinga na kujifunza namna mume anayostahili kutunzwa vizuri. Swala la mamlaka limejitokeza katika mchakato wa kiakili kama huo na mingine tuliyochunguza na tumeona kuwa ubabedume ndio itikadi inayosababisha mke wa pili kumdunisha mke wa kwanza ili ajipendekeze kwa mumewe. Vilevile, tumeona kuwa mamlaka na itikadi yanaweza kufafanuliwa kupitia kwa mchakato wa kihusiano. Kwa mfano, mke wa pili anapomwambia mke wa kwanza kuwa, *kuishi na mume kazi*. Katika mchakato huo, kazi ndiyo Sifa, *kuishi na mume* ni Mbebaji huku kitenzi *nikilicho* kapa katika muktadha huu ndicho chenye mchakato wa kihusiano. Mke wa kwanza anakumbushwa na mke wa pili kuwa mke lazima ajibidiishe anapokuwa na mume wake kwa kufanya mambo ya kumfurahisha kama vile kumpikia vyakula vizuri na kumwonyesha mapenzi. Tumeona pia kupitia kwa lugha ya mafumbo maneno kama *dozi* na *mavitus* yakitumika kwa maana fiche ya ngono. Ngono ambayo imefichwa katika mafumbo hayo pamoja na vitendo vya kudhihirisha mchakato wa kihusiano wa *kuishi na mume kazi*, ni njia ambazo mke anatumia ili kumvutia mume kisha kumdhibiti kwa lengo la

kupata faida za kiuchumi kwa vile vitendo hivyo vyote vya kumvutia mume ni kama kuwekeza. Japo, mke wa pilianayeonekana akimtendea mumewe vitendo hivyo aweza kuonekana kama “mtumwa” huku mumewe akiwakama “mtawala” wake, kwa kutumia DCT, tumeona kuwa anayeishia kuwa na mamlaka si mume bali ni mke hasa mume “anapotumwa” usingizini na mkewe. Kwa ujumla, michakato hii ya uelekezi pamoja na lugha ya mafumbo ni mikakati ya kipragmatiki ambayo kama tulivyoona imeweza kuibusha mahusiano ya mamlaka na hata kufichua itikadi fiche katika wimbo huu.

Katika sura inayofuata, tutaeleza kwa ufupi msingi wa utafiti ili matokeo na mahitimisho tutakayotoa katika sura hiyo yawe yaliyofungamana na mada, nadharia iliyotumika, tatizo la utafiti, nadharia tete, malengo na upeo na mipaka ya utafiti. Tutaeleza pia umuhimu wa utafiti huu na mapendekezo ya utafiti zaidi.

SURA YA TANO

MATOKEO, MAHITIMISHO, UMUHIMU WA UTAFITI HUU NA MAPENDEKEZO.

5.1 Muhtasari wa mambo ya kimsingi ya utafiti

Utafiti huu ulihusu mada ya mamlaka na itikadi katika nyimbo teule za taarab na ulikuwa na malengo matatu. Kwanza, kueleza utunzi wa nyimbo teule za taarab na maudhui yanayotawala katika nyimbo hizo kwa lengo la kubaini mafungamano yake na itikadi inayotawala katika nyimbo hizo. Pili, kuonyesha udhihirikaji wa mahusiano ya mamlaka katika nyimbo teule za taarab na mwisho, kueleza mikakati ya kipragmatiki katika nyimbo hizi teule za taarab na mchango wake katika ujenzi wa mamlaka na itikadi. Nadharia tete za utafiti huu zilikuwa tatu vile vile: Kwanza, utunzi wa nyimbo teule za taarab na maswala yanayotawala katika nyimbo hizo ni mambo yanayosababishwa na itikadi ya ubabedume. Pili, mahusiano ya mamlaka hudhihirika katika nyimbo teule za taarab. Tatu, mikakati ya kipragmatiki inahusika pakubwa katika ujenzi ujenzi wa mamlaka na itikadi katika nyimbo teule za taarab. Upeo na mipaka yetu kuhusu kazi hii ulihusu kuchunguza mamlaka na itikadi katika nyimbo teule za taarab ambazo ni *Zilipendwa* uliyoimbwa na Khadija Yusuf na *Utalijua Jiji* uliyoimbwa na Afua Suleimani. Tulitumia mihimili miwili ya nadharia ya DCT yaani mamlaka na itikadi kisha tukatumia mtazamo wa IAK kufafanua mahusiano ya mamlaka kwa kutumia michakato mitatu ya uelekezi: yakini, kiakili na kihusiano. Mbinu zetu za utafiti zilikuwa kuteua nyimbo hizo kutumia sampuli lengwa kisha kuandika maneno ya nyimbo hizo kwa lengo la kuchanganua matini zake. Isitoshe tulikuwa tukichota mifano michache kutoka kwa nyimbo zingine za taarab zilizo katika tapo hili na kazi nyingi za fasihi kwa lengo la kusisitiza jambo fulani kulipokuwa na haja ya kufanya hivyo.

5.2 Matokeo

Kutokana na uchunguzi wa utafiti wetu, tumedhihirisha kwamba utunzi wa nyimbo teule za taarab na maudhui yanayotawala katika nyimbo hizo unaongozwa na itikadi ya ubabedume. Hili linatokana na ukweli kwamba watunzi wengi wa nyimbo za taarab huwa ni wanaume na hivyo hutaka kudumisha mahusiano yao na wanawake kwa nia ya kuwapembeza wanawake. Nyimbo hizo kwa kiwango kikubwa zinamkweza mwanamume kwa kumfanya mtu au rasilmali muhimu sana katika jamiii ambayo wanawake kupitia kwa chuki kati na miongoni mwao, masimango wanayofanyiana, kukubali ukewenza, kufanyia wanaume mambo kama kupika, kuwaogsha, kuwapepea wanapohisi joto, kuwafurahisha kwa kila njia na kuwapa ngono nzuri miongoni mwa mambo mengine. Watunzi hao wa kiume wanapogundua kwambabaaadhi ya wanawake wanakinza swala kama vile ukewenza, huweza kutunga nyimbo hizo kwa lengo la kuwakumbusha kwamba swala hilo lipo na limekubaliwa katika dini ya Kiislamu ambayo ndiyo dini tawala katika utamaduni wa jamii kunakotungwa nyimbo za taarab. Hivyo basi, lengo na nadharia tete ya kwanza zimedhibitishwa kutokana na matokeo hayo.

Lengo na nadharia tete ya pili ilikuwa kuonyesha kwamba mahusiano ya mamlaka hudhihirika katika nyimbo za taarab. Tumbaini hilo katika nyimbo zote mbili. Kuna mahusiano ya mamlaka mbali mbali katika nyimbo hizo na hivyo katika jamii zinamotungiwa. Mahusiano hayo yanahusu mamlaka yaliyopo kati ya jinsia moja na jinsia nyingine tofauti. Katika wimbo *Zilipendwa*, tumeona kwamba mwanamke kupitia kwa michakato ya uelekezi na hasa mchakato yakini ameweza kuonyesha kwamba anaweza kudhihirisha mamlaka yake kwa mwanamume kwa kumfurusha, kumkataa na hivyo mwanamume anakuwa Lengo. Hata katika mchakato wa

kihusiano ambapo anamdunisha mwanamume kwa kumtaja kwa majina ya kumsawiri vibaya anadhihirisha kuwa katika diskosi fulani mwanamke anataka mabadiliko katika mahusiano yake na mwanamume. Hii ni ithibati kwamba mahusiano ya mamlaka kati ya mwanamke na mwanamume yana sifa ya hejemonia na matumizi ya lugha ya mafumbo katika wimbo *Zilipendwa* na uchunguzi wa mchakato wa kihusiano umedhihirisha hilo. Hivyo basi, mwanamke anakinza mahusiano ya mamlaka katika jamii hiyo ambapo mwanamume amepewa uwezo kuhusu uteuzi wa wanawake kwamba anaweza kuwa na wake wengi akiwatema bila kuonekana kama mtu mbaya. Hii ni hatua nzuri na pumzi mpya katika harakati za wanawake kuonyesha haja ya kugeuza chukulizi za wanaume kama wanaostahili kuwanyanyasa wanawake katika mahusiano bila wanawake kufanya chochote. Mahusiano ya mamlaka mengine katika wimbo huo ni kati ya mwanamke na mwanamke mwenzake. Mahusiano ya sampuli hiyo ndiyo yanayotawala katika nyimbo hizo ukiwemo *Utaliyua Jiji*. Katika nyimbo hizi tulizochanganua mke wa pili kupitia kwa michakato yakini, kiakili na kihusiano na kwa kutumia lugha ya mafumbo amedhihirisha mamlaka kwa mke wa kwanza aliyempokonya mume wake kutokana na majigambo anayomfanyia kwa lengo la kuonyesha kwamba yeye ndiye mke bora kwa mumewe. Katika uchunguzi wa aina hii ya mamlaka ya mke wa pili aliye Mtendaji anadhihirisha uwezo wa mamlaka kwa mke wa kwanza aliye Lengo. Vitendo yakini vya Mtendaji vimelenga ujipendekezaji wa Mtendaji kwa mume na vikawa katika hali hiyo vikimdunisha Lengo. Hata hivyo, mamlaka haya ambayo mke wa pili hujaribu kuyadhihirisha kwa mke wa kwanza yanalenga kuendeleza mamlaka mengine ya tatu katika jamii ambapo mume anakuwa na mamlaka zaidi akilinganishwa na mwanamke hata anapokuwa Lengo kwa kutendewa vitendo kama vile kupikiwa na kupewa mapenzi yaliyonoga. Kama tulivyobaini katika hizi nyimbo mbili, mwanamke anapokuwa Mtendaji wa vitendo yakini kama kupika, kumpa mumewe mapenzi,

kumtunza miongoni mwa vitendo vingine, anafanya hivyo ili kumfurahisha mumewe na anafurahia majukumu hayo na kuwa tayari kumsuta mwenzake asiyejua majukumu hayo ipasavyo. Hilo halikujitokeza tu katika mchakato yakini pekee kwani hata katika mchakato wa kiakili, urembo na mwili wa mwanamke vinaelezwa kama nyenzo muhimu za kuwatia wanawake katika mahusiano na wanaume. Miili na hasa makalio makubwa pamoja na urembo vinachukuliwa kama Finomena ambazo zinachochea hisia za wanaume wanaokuwa Wahisi na hivyo wanaodhibiti vitendo hivi vya kuvutiwa na wanawake. Kwa hivyo mwanamume anapewa mamlaka makubwa katika jamii hii kwa kuwa sawa na mfalme huku wanawake wakiwa watawaliwa wake ambao malumbano yao kila siku yanahusu kumfurahisha huyo mfalme. Mwanamke hulenga kumfanyia mwanamume mambo hayo yote ambayo hutaka yaonekane kama mapenzi halisi yanayotokana na nia njema ya kumfurahisha mwanamume lakini kama tulivyobaini, mapenzi hayo yote anayodai mwanamke huwa ni sumaku ya kumnasa na kudhibiti mwanamume ili asiende kwa mke mwingine na pia kwa lengo la kuhakikisha kuwa mwanamume anapokuwepo basi faida za kiuchumi atazipata yule mwanamke. Ndani ya mahusiano ya mamlaka ambapo mwanamume anamfanya mwanamke kama mtumwa, mwanamke vilevile humdhibiti kwa kiwango fulani kupitia kwa mizungu ya mapenzi ambayo humzuga mwanamume na mwanamke huishia kufaidika kutokana na hilo. Hivyo, kunakuwa na mamlaka ya aina yake kwa mwanamke na mwanamume vilevile. Licha ya mwanamke kuwa katika hali sawia na utumwa wa mwanamume, anakuwa na mamlaka fulani ya kuweza kumdhibiti mwanamume kutokana na mizungu ya mapenzi.

Lengo na nadharia tete yetu ya mwisho ilikuwa ni kuonyesha kwamba itikadi ya ubabedume ndiyo inayotawala katika nyimbo teule hizi za taarab. Ama kwa hakika, kama tulivyoeleza hayo

mahusiano ya mamlaka pamoja na kufafanua utunzi wa nyimbo hizi na maudhui yanayotawala, ni wazi kwamba ubabedume umetawala katika nyimbo hizi. Tumeona kwamba japo wanaume ndio hutunga nyimbo hizi mara nyingi kuliko wanawake, hupenyeza itikadi ya ubabedume katika nyimbo hizo. Hutumia nyimbo hizo kama chombo cha kukemea juhudi za wanawake kupinga mambo yanayoendeleza ubabedume na hasa swala la ukewenza. Maudhui mengine katika nyimbo hizo kama chuki, mapenzi, masimango yote hutokana na wanawake kutaka kuonyesha ujuzi wao na ubora wao katika kuwatunza wanaume. Kwa kuchunguza mambo hayo wanayotenda wanawake, yote hulenga kupata fursa ya kuhusiana na mwanamume na hivyo inakuwa kwamba mwanamume katika jamii hii amekwezwa sana ilhali mwanamke amepembeza. Kwa kufanywa mtu wa kutenda mambo ya kumfanya mwanamume kufurahi, mwanamke anakuwa mtegemezi wa mwanamume kwa kiwango kikubwa. Utegemezi huu wa mwanamke kwa mwanamume ndio unaoendeleza itikadi ya ubabedume. Ajabu ni kwamba itikadi hiyo huendelezwa na wanawake wengi bila kujua kwamba wanaiendeleza maana imefanywa kuwa jambo la kawaida kwa kuhalalishwa kupitia kwa maswala ya utamaduni na dini ya Kiislamu. Itikadi hiyo ya ubabedume inaweza kuelezwa kwa kuchunguza namna mamlaka yanavyodhihirika katika nyimbo hizo ambapo hata wanawake wanapokuwa Watendaji katika mahusiano yao na wanawake wenzao au wanaume, matendo yao yanalenga kujipendekeza kwa kudunisha wake wenzao au kuwafanyia wanaume mambo ambayo yatawafurahisha.

5.3 Mahitimisho

Utafiti huu ulihusu kuchunguza swala la mahusiano ya mamlaka na itikadi katika nyimbo teule za taarab. Kutokana na matokeoya utafiti huo, mahitimisho yafuatayo yanaweza kutolewa. Kwanza, kumedhihirika kwamba mikakati ya kipragmatiki ina mahusiko makubwa

katika ujengaji wa itikadi ya ubabedume ambayo inatawala katika nyimbo hizi za taarab. Maswala yote yanayojitokeza katika nyimbo hizo hutokana na ubabedume. Vile vile, mahusiano ya mamlaka yanapatikana katika nyimbo hizo teule za taarab. Mahusiano hayo ya mamlaka hata hivyo yanatofautiana kutoka muktadha mmoja hadi mwingine. Kwa mfano, kuna wakati ambapo mke wa pili ana mamlaka kwa mke wa kwanza katika muktadha fulani kwa kuwa Mtendaji ilhali mwenzake akiwa Lengo mtawalia. Pia mamlaka yanaweza kuwepo kati ya mke na mumewe ambapo mke anakuwa Mtendaji na mumewe anakuwa Lengo. Vilevile mume anaweza kuwa Mtendaji na mkewe akawa Lengo. Kwa hivyo, uhusiano wa mamlaka unakuwa tofauti katika muktadha tofauti na hili lina maana kuwa mamlaka yanahusu malumbano.

Jambo lingine ni kuwa familia au ndoa ndio msingi wa malumbano yanayolenga kudhihirisha ni nani mwenye mamlaka na katika muktadha gani. Jamii ya Waswahili ikiwa inayopendelea ukewenza, wanawake wanajiingiza katika ushindani, malumbano, masuto na majigambo yanayolenga kuwadunisha na kuwadhalilisha wenzao kwa lengo la kujipendekeza kwa waume. Ujipendekezaji huu wa mke dhidi ya mke mwenzake unatokana na matumizi ya lugha yaliyojaa mikakati ya kipragmatiki. Ingawa kumekuwa na tafiti mbalimbali kuhusu mahusiano ya mke na mume katika nyimbo za taarab, mawazo yaliyokuwa yakitawala yamekuwakwamba mke amedunishwa na kunyanyaswa. Tafiti zingine zilizojaribu kumsawiri mwanamke kama anayejaribu kujikomboa ziliongozwa na matokeo mabaya na hivyo mahitimisho yake yakawa ya kupotosha pasi kuelewa kwa kina mahusiano ya mke na mume hujikita kwa nini katika jamii ambazo nyimbo za taarab hutokea. Hata hivyo, kwa kutumia nadharia ya DCT na mtazamo wa IAK, tumegundua kuwa katika nyimbo za taarab, swala la ubabedume ambalo limekuwa likitajwa tu na hivyo kuwekwa pembeni wakati wa kueleza mahusiano kati ya mke na mume, ndilo

linalotawala katika nyimbo hizo na linastahili kupewa kipaumbele. Swala hilo linaweza kufafanuliwa vizuri kwa kutumia mtazamo wa kiisimu wa IAK tuliotumia wenye uwezo wa kuchanganua mahusiano ya mamlaka katika jamii kwa kuishirikisha nadharia ya DCT. Kwa kufanya hivyo, itaeleweka ni kwa nini mke humfanyia mume mambo yanayoonekana kumdunisha kama inavyosemwa. Ila kwetu, japo mke anapomfanyia mumewe mambo kama vile kumpikia, kumfurahisha, kumpelekea maji chooni ili aoge, kumpa mapenzi ya kutosha kitandani, kukorofishana na mke mwenzake hata kutumia njia za ajabu kama kutumia hirizi kutoka kwa waganga, yote haya anayafanya kwa lengo la kufaidika katika mahusiano yake na mumewe ambapo anapata faida za kiuchumi. Kunyenyekea wanakodhani wake hufanya kuonyesha unyonge wao ni mkakati wa kumdhibiti mume kwa njia moja au nyingine ili kupata fursa yakufaidika kiuchumi. Kwa hivyo, nyimbo hizi pamoja na kwamba kwa mtazamo wa nje huonekana kwamba ni nyimbo za kumdhalilisha mwanamke, uchunguzi wa diskosi yake kupitia nadharia ya DCT na mtazamo wa IAK umefichua kwamba hilo ni swala kinyume. Nyimbo hizi ni harakati kubwa ya mapambano ya wanawake kugeuza baadhi ya mahusiano ya mamlaka baina yao na wanaume. Hata hivyo, haina maana kwamba wanaume wanapoteza mamlaka yao kwa vile bado wanapewa kipaumbele katika jamii hii ila wanawake wako tayari kukinza mambo fulani yanayowadunisha.

5.4 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu utawafaidi wasomi wengine wa fasihi ya Kiswahili watakaotaka kuielewa nadharia ya DCT na mtazamo wa IAK katika lugha ya Kiswahili maanake hii ndio kazi ya kwanza katika lugha hiyo. Ingawa tafiti za awali kuhusu nyimbo za taarab zimekuwa zikihusu maudhui na mtindo, utafiti huu umechanganua maswala ya mahusiano ya mamlaka na itikadi yanayotawala

katika nyimbo hizo na hivyo kuweka msingi wa uelewa wa kwa nini maswala mengine yanayotokea katika nyimbo hizo huwa yalivyo. Isitoshe, walimu wa shule za upili na vyuo watapata mtazamo mpya wa uchanganuzi wa kazi za fasihi kutoka kwa ule wa kawaida wa kuchunguza maudhui na mtindo hadi kwa uchanganuzi wa kutumia nadharia za kiisimu kama vile nadharia hii ya kipragmatiki tuliyotumia . Mwisho ni kwamba utafiti huu utakuwa marejeleo kwa watafiti watakaotafiti kuhusu masiala kama uelekezi kwa mtazamo wa IAK,nadharia ya DCT katika Kiswahili,mahusiano ya mamlaka na itikadi katika diskosi, ubabedume na utunzi na maudhui yanayotawala katika nyimbo za taarab.

5.6 Mapendekezo

Utafiti huu ulihusu maswala ya mamlaka na itikadi katika nyimbo mbili za taarab: *Zilipendwa* uliyoimbwa na Khadija Yusuf na *Utaliyua Jiji* uliyoimbwa na Afua Suleimani. Ulitumia nadharia ya DCT na michakato mitatu ya uelekezi yaani yakini, kiakili na kihusiano na pia ukachunguza lugha ya mafumbo katika nyimbo hizo. Matokeo yake na mahitimisho basi yalitokana na upeo huo. Kwa hivyo, huenda mahitimisho na matokeo ya watafiti wengine wakitumia nadharia hii au tofauti yawe tofauti wakichanganua nyimbo zingine za taarab tofauti na hizi maana kama tulivyodokeza awali katika upeo na mipaka, nyimbo za taarab zina migao mbalimbali na hivyo itikadi inayotawala katika nyimbo hizo inaweza kuwa tofauti pamoja na hata mahusiano ya mamlaka. Vile vile, kuna michakato mitatu ya uelekezi ambayo ni yakiusemi, kidhanaishi na kitabia ambayo hatukuchunguza. Labda ikichunguzwa huenda kukawa na matokeo na mahitimisho tofauti na yetu. Kunahaja pia ya kuchunguza swala hili la mamlaka na itikadi katika kazi nyingine za fasihi ya Kiswahili kama tamthilia, ushairi, hadithi fupi na hata riwaya ili kubaini iwapo itikadi ya ubabedume inatawala katika mahusiano ya mamlaka katika jamii za Afrika.

MAREJELEO

- Abdulaziz, M. (1996) *Transitivity in Swahili*. Koln: Koppe: East African Language and Dialects: Vol.51
- Althuser, L. (1971) *Ideology and Ideological State Apparatus" Lenin and Philosophy, and other essays*. Trans. Ben Brewster. London: New Left Books (Pp.127-188)
- Askew, K.M. (2002). *Performing the Nation: Swahili Music and Cultural Politics in Tanzania*. Chicago and London: University of Chicago Press.
- Austin, J.L. (1962) "How to do Things with Words." In Jawoski & Coupland (Editors). *The Discourse Reader* (2nd Edition.) USA: Routledge.
- Ba`, M. (1976) *Barua Ndefu Kama Hii*, Maganga, C. (2009 (mtafsiri.): Dar es Salaam: Mkuki na Nyota Publications.
- Bloor, B & Bloor, T (2004). *The Practice of Critical Discourse Analysis: An Introduction*. London: Hodder Education.
- Chomsky, N (1957) *Syntactic Structures*. The Hague: Mouton & Co.
- Chouliaraki, L & Fairclough, N (1999) *Discourse in Late Modernity: Rethinking Critical Discourse Analysis*. Great Britain; Edinburg University Press.
- Fair, L (2001) *Pastimes and Politics: Culture, Community and Identity in Post-Abolition Urban Zanzibar, 1890-1945*. Athens: Ohio university Press.
- Fairclough, N. (1997) *Language as Social Practice*. London: Sage.
- Fairclough, N (1989) *Language and Power*. London: Longman.
- Fairclough, N (1992) *Discourse and Social Change*. UK: Blackwell.

- Fairclough, N (1993). "CDA and Marketization of Public Discourse", *Discourse and Society*, 4:133-62.
- Fairclough, N (1995) *Critical Discourse Analysis: the Critical Study of Language*.London.
- Fairclough, N (2000) *New Labour, New Language*.London: Routledge.
- Fairclough, N. (1996) "Technologisation of discourse" In,Coulthard, M. and Caldas-Coulthard, C.R (editors), *Texts and Practices*.London: Routledge.
- Fairclough, N. and Wodak, R. (1997) "Critical Discourse Analysis" In Van Dijk, T (ed.) *Discourse as Social Interaction*, London: Sage.
- Foucault, M. (1977) *Discipline and Punish*. London: Allen Lane.
- Foucault, M. (1980) In: Gordon, C., Marshal, J. and Soper, K (editors).*Power /Knowledge: Selected Interviews and Other Writings: 1972-1997*.Brighton: Harvester Press.
- Fowler, R et al (1979) *Language and Control*.London: Routledge & Kegan Paul.
- Gramsci, A. (1971) *Selections from the Prison Notebooks*, London: Lawrence & Wishart.
- Habwe, J.H (2011) .*Safari ya Lamu*.Nairobi: Longhorn.
- Halliday, M.A.K. (1985) .*An Introduction to Functional Grammar*.London: Edward Arnold.
- Halliday, M.A.K. (2014) *An Introduction to Functional Grammar* (3rd edition) Rev. Mathiessen (editor).C. London: Edward Arnold.
- Halliday, M.A.K. (2004) *An Introduction to Functional Grammar* (2nd edition).London: Edward Arnold.
- Hodge, R and Kress, G. (1979) *Language as Ideology*.London: Routledge & Kegan Paul.
- Hodge, R and Kress, G. (1993): *Language as Ideology*. (2nd edition).London: Routledge& Kegan Paul.

- Hymes, D. (1972) "The Ethnography of Speaking" In Gladwin T, Sturtevant W.C. (editors) *Anthropology and Human Behaviour*. Anthropological Society of Washington.
- Igobwa, S.E. (2007) *Taarab and Chakacha in East Africa: Transformation, Appreciation and Adaptation of Two Popular Music Genres of the Kenyan Coast*. A paper presented during Conference on Music in the world of Islam, 8-13 August, 2007, Toronto, Canada.
- Khamis, S. A. M. (2002) *Wondering about Change: The Taarab Lyric and Global Openness*. *Nordic Journal of African Studies* 11, 2: 198-205.
- Khatib, M. S. (1985). *Utenzi wa Mwanakupona*. *Mulika* 17: 46-52.
- Khatib, M.S. (1992). *Taarab Zanzibar*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.
- King'ei, K.G. (1992) *Language, Culture and Communication. The role of Taarab songs in Kenya 1963-1990*, Unpublished PhD thesis, Howard University.
- Labov, W. (1972) *The logic of non-standard English*. In Giglioli 1972.
- Longhorn (2011). *Kamusi ya Karne ya 21*. Nairobi: Longhorn Publishers Ltd.
- Massamba, D. P. B. (2002) *Historia ya Kiswahili: 50 BK hadi 1500 BK*. Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.
- Matei, A.K. (2014) *Discourse, Gender Identity and Gender Power Relations in Fiction: A CDA and SFL Reading of Wamitila's Unaitwa Nani?* Unpublished PhD thesis: University of Nairobi.
- Mazrui, A. (1984) *Kilio cha Haki*. Nairobi. Longhorn.
- Meyer, M & Wodak., R. (2001) *Methods of Critical Discourse Analysis*: London: Sage Publications Ltd.
- Miller, C.L. (1990) *Theories of Africans: Francophone Literature and Anthropology in Africa*, Chicago and London, University of Chicago Press.

- Mnenuka, A. (2012). *Tofauti ya dhana ya mwanamke katika jamii; Mifano kutoka katika taarab (mipasho) na nyimbo za Kibena* katika Swahili Forum 19 (2012); 23-44.
- Mohammed, S.A (1980) *Utengano*. Nairobi: Longhorn.
- Mtobwa, B.R (1998) *Dar es Salaam Usiku*. Dar Es Salaam: Heko Publishers.
- Ntarangwi, M. (2003). *Gender, Identity and Performance*, Asmara: African World Press, Inc.
- Simpson, P (2004) .*Stylistics: A Resource book for students*. London & New York: Routledge.
- Timammy, R. (2002) *Mombasa Swahili Women's Wedding Songs*. Unpublished PhD Thesis: University of Nairobi.
- Timammy, R. (2004) *Uteuzi wa Moyoni, katika Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine {Wamitila, K.W (mhariri)}*. Nairobi: Focus Publishers Ltd.
- Traoré, F. A. (2004). *Continuity and Change in Zanzibar Taarab Performance and Poetry*. *Swahili Forum* 11: 75-81.
- TUKI (2014) *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salaam: TUKI.
- Van Dijk, T (1995). *Discourse Analysis as Ideology Analysis* in Christiina Schaffner and Anita L.Wenden (eds.). *Language and Peace*. Dartmouth: Aldershot. Pp.17-33.
- Van Dijk, T (2001) “*Multidisciplinary CDA: A Plea for Diversity*” In, Wodak & Meyer (eds) *Methods of Critical Discourse Analysis*. London. Sage Publications Limited. Pp.95-120.
- Van Dijk, T. (1986) *Handbook of Discourse Analysis*, Vol.4. Academic Press.
- Van Dijk, T. (1990) “Discourse & Society: a new journal for a new research focus”, *Discourse & Society*, 1, pp 5-16.
- Van Dijk, T. (1991) *Racism and the Press*. London: Routledge.

- Van Dijk, T. (1993) “*Principles of Critical Discourse Analysis*,” *Discourse and Society*, pg:249-83. Reprinted in J.Cheshire and J.Trudgil (eds.) 1988 ,*The Sociolinguistics Reader*, vol. 2 London: Arrol.
- Van Dijk, T. (1996) “Discourse, power and access “, In Coulthard, M. and Caldas-Coulthard, C.R (editors), *Texts and Practices*. London: Routledge.
- Van Dijk, T. (1998) *Discourse and Ideology* (Editorial). *Discourse and Society* 9.3.
- Wa Mberia, K.(1997) .*Natala*. Nairobi: Marimba Publications Ltd
- Wa Mberia, K. (2000). *Kifo Kisimani*. Nairobi: Marimba Publications Ltd.
- Wamitila, K.W. (2008) *Unaitwa Nani?* .Nairobi: Vide-Muwa.
- Weiss, G. & Wodak, R. (2003) *Critical Discourse Analysis: Theory and Interdisciplinarity*. Hondmills: Palgrave Macmillan.
- Wodak, R. (1989) *Language, Power and Ideology: Studies in Political Discourse*. Amsterdam: John Benjamins.
- Wodak, R. (1996) “The genesis of racist discourse in Austria since 1989”, In Coulthard, M. and Caldas-Coulthard, C.R (editors), *Texts and Practices*. London: Routledge.
- Wodak,R.(2001)”*What CDA is about-a summary of its history, important concepts and its developments*” In Wodak,R and Meyer,M(eds) *Methods of Critical Discourse Analysis*. London.Sage Publications Ltd.Pp 1-13.
- Yego, E.K. (2011) .*Nafasi ya Mwanamke: Jinsi Inavyotetewa katika Nyimbo za Taarab Zanzibar*.Tasnifu ya shahada ya uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi.Haijachapishwa.
- Zaja, J.O. (2008) *Publicizing the Private: Feminist Locution in Taarab Songs and Performance*. A Paper presented at the CODESRIA 12th General Assembly on 7th-11th Dec. 2008. Yaounde, Cameroon.

VIAMBATISHO

1. ZILIPENDWA

Mwimbaji: Khadija Yusuf

Kiitiko 1: Zilipendwa zilipendwa, sina haja naye tena
Nimetapika sina hamu tena

1

Sikuambiwa yuko, nimeambiwa wako
Kama umemchukua, saizi yako

2

Na mimi tayari mwingine ninaye
Wasiwasi sina oooh yakhe

3

Niliyajua kitambo, kama huyo bakabaka
Sasa kama kwako yuko, wengine anako anakokwenda.

Kiitiko 2: Hapandi farasi, mzoea punda
Noti si karatasi, dereva si konda

4

Kama huko ni kupata, chukua ufaidike
Halafu usije juta, ukifika mwisho kwake

5

Na wala sitowafuta, awe wako uwe wake
Yupo alonifumbata, alofanya niridhike
Msijibanze na kuta Kivyangu yeye kivyake

Kiitiko 3: Mwenyewe nawatengeza, shoga sina shida hiyo
Malighafi nimejaza, haitaki tochi hiyo

6

Unaniona natamba, na mpenzi wangu sambamba
Kichuna boksi natamba, na hiyo lela sambamba
Bure ghali zilipendwa Bure ghali zilipendwa

7

Sijitie bure pepo, aso mpungaji wake
Huku waambulia hapo, alipokuwa na chake

8

Na watu atokapo, appendeza peke yake
Jicho hubakia kwake, hutaki litoke kwake
Sasa baki haliwepo, hana chake hana lake.

9

Fuataneni niwaone, wala usibabaike
Tena tusalimiane, hisani isivunjike

10

Nimeshapata mwingine, nampenda peke yake

Si mwembamba si mnene, aloshiba kwa mamake

11

Sijanuna sijakereka, vitendo vyake vilinitosha
Zilipendwa kwangu zilipendwa, “Long time” nimemfurusha
Nichanganyie nichekicheki, nachichitiza na mtu unatisha.
Hujatulua hujapepewa, u limbukeni unachekesha

12

Jeuri mwenzio kusudi, hutaki mwenziwe basi
Sina haja ya shahidi, si mvuvi si msasi
Nishamtoa moyoni

13

Aliposema mimi wa nini, kuna walosema watanipata lini
Usione soo, sema naye,
Kwangu noo, sina haja naye
Zilipendwa sina haja naye.

2. UTALIJUA JIJI

Mwimbaji: Afua Suleimani

East African Melody

1

Kazi yako ufisadi jeuri gebe na dobwa
Baraka ya ugaidi, ukali kama embe bwabwa.
Vituko vya makusudi, si bure wewe umerogwa
Badala ya soda baridi, ama juisi ya chungwa,
Ushamba umekuzidi, andazi wanywea togwa.

2

Mwenzangu huna ujuzi, mpenzi umemuudhi,
Kaja kwangu nimempokea, kaja kwangu nimempokea,

3

Pokea chako kibomu, shoga nakutumia
Hata ukinilaumu, wako nishamchukua,
Penzi ulimdhulumu, visa ukamfanyia,
Chachanduvi tamutamu, wala hukumpatia,

4

Bwana kapata wazimu, kashindwa kuvumilia,
Kwangu akatia timu, tiba nikampatia.
Nikampa vitu adimu, kwako hajajionea,
Amri akasalimu, magoti kunipigia,
Huku akijilaumu, kwako kapotea njia,

5

Kwako kaachia ngazi, kwangu kaweka makazi
Sasa bwana kabarizi, kachoka yako maudhi,
Utamaliza mizizi, waganga na waganguzi
Talasamu na hirizi, ongeza na vipodozi,
Kwake hupati nafasi mimi ndiye yake pumzi,

6

Kapenda yangu nidhamu na utulivu nyumbani
Pamoja na ukarimu, kwa ndugu na majirani,
Ucheshi na tabasamu, kanijalia Maanani
Nimepewa lugha tamu, nyoka hutoka pangoni.

7

Sifa hizi ni muhimu, na mengine mengi ndani
Wewe mkaanga sumu, kwako hazipatikani.
Na mapishi yako bomu, kitimutimu jikoni,
Wali wautia ndimu, hayo ni mapishi gani?
Bwana imemwisha hamu, kakutumua nyumbani.

8

Unaningoja njiani, madhila kunifanyia
Usitake ushindani, hunishindi nakwambia
Mimi naletewa ndani, wewe watanga na njia,
Magomeni, Buguruni, ndala zakukatikia,

9

Wasela wa vijiwani, nafuu wajipatia,
Uroda kwa foleni, kwako wajipendelea,
Wewe gumzo mjini, watu wanahadithia,
Umeachika ndoani, kwa yako mbaya tabia,
Unaogea jikoni, bafuni unapikia,

10

Tazama utalijua jiji mwenzangu
Chajio utakunywa uji mwenzangu
Na juisi utakunywa maji mwenzangu
Huyo kwako harudi tena mwenzangu
Najinafasi, najinafasi
Tatijuu wewe utajijuu wee utajiju

11

Wako nishamchukua, kwako harudi tena
Katamka waziwazi, kuwa hakutaki tena
Amenipa nafasi, nimwonyeshe ujuzi
Nami sifanyi ajizi, mpenzi ninamuenzi
Nampikia maandazi, na chai ya tangawizi
Wali wa nazi kwa ndizi, *mavitus* kama kazi
Kisha natoa dozi, impayo usingizi
Mwenzangu huna ujuzi, rudi tena kajifunze
Bibi acha upuuzi kuishi na mume kazi
Mume ataka malezi, sio mambo ya kihuni
Gebe na jeuri zako, leo zimekuishia we mwenzangu.